NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Sita– Tarehe 11 Septemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Hati za kuwasilisha mezani

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka 2018 *[The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018].*

MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 *[The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018].*

MHE. HALIMA J. MDEE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 *[The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018]*

MWENYEKITI: Ahsante, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU– KATIBU MEZANI: Maswali

MASWALI NA MAJIBU

Na. 68

Baadhi ya Raia Kushiriki Uchaguzi Tanzania na Msumbiji

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y. MHE. HAMIDU H. BOBALI) aliuliza:-

Kumekuwa na raia wengi kutoka Msumbiji katika Jimbo la Mchinga hasa Vijiji vya Kilangala B, Butamba, Mvuleni, Kitolambwani na Kikonde ambao wamekuwa wakishiriki uchaguzi katika nchi zote mbili Tanzania na Msumbiji.

(a) Je, raia hao ni Watanzania au wa Msumbiji?

(b) Je, Serikali imepitisha utaratibu wa uraia pacha na kuwapa watu maalum?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania. Aidha, Ibara ya 5(2) ya Katiba hairuhusu mtu mwenye uraia wa nchi nyingine (raia pacha) kushiriki katika shughuli za uchaguzi ikiwemo kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ili mtu aweze kupiga kura lazima awe ameandikishwa kwenye daftari la kudumu la wapiga kura lililoanzishwa chini ya ibara ya 5(3)(a) ya Katiba. Uandikishaji wa wapiga kura unapokamilika, daftari la awali huwekwa wazi kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 ili kukaguliwa na wananchi. Kifungu cha 24(1) cha sheria hiyo kinatoa fursa kwa mtu aliyejiandikisha kuweka pingamizi dhidi ya mtu mwingine aliyendikishwa kwenye daftari ikiwa imebainika kuwa hana sifa ya kuandikishwa kwa kutokuwa raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii, sheria zetu hazijaruhusu uraia pacha na hakuna watu maalum waliopewa uraia wa aina hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali yanaonesha kwamba kumbe Tume ya Uchaguzi haiandikishi watu kwa kufuata vigezo bali inaandikisha yeyote atakatejitokeza na mzigo wa kuangalia nani ana vigezo na nani hana unabaki kwa wananchi kwamba waweke pingamizi, jambo hili siyo zuri.

Sasa Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Tume ya Uchaguzi inapoandikisha wapiga kura ifuate vigezo vilivyoainishwa kisheria? Hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kutokana na harakati za kiuchumi sasa hivi zilivyo duniani Watanzania wanaishi katika mataifa mbalimbali na wangependa kuendelea ku-*enjoy* ule Utanzania (utaifa) wao. Serikali ina mpango gani wa kuruhusu uraia pacha ili Watanzania walio nje na wenyewe waweze kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kama watanzania wanaoishi Tanzania? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA swali la kwanza, si kweli kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikiwa inawaandikisha Watanzania kushiriki kwenye uchaguzi haifuati vigezo vilivyowekwa. Kwa mujibu wa Katiba yetu na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, vigezo vimewekwa vya nani anapaswa kuandikishwa kwenye daftari la kupiga kura na ndiyo maana kifungu cha 24 cha sheria hiyo kimetoa mwanya kwa mtu yeyote ambaye ana pingamizi kwa mtu aliyeandikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake si kwamba tume sasa inamchukua kila mmoja tu lakini kwa mujibu wa kifungu hicho imetoa nafasi hiyo ili yeyote mwenye pingamizi awasilishe pingamizi hilo kwa Tume lifanyiwe kazi na kama mtu hana sifa ataondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uraia pacha limezungumzwa mara zote, suala hili ni la Kikatiba muda utakapofika na itakapoonekana inafaa basi ninaamini sisi sote kama Wabunge na nchi kwa ujumla tutaenda katika mwelekeo huo, lakini kwa hivi sasa Katiba na sheria zetu haziruhusu uraia pacha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kuniruhusu niulize swali la nyongeza katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhusu raia wageni kushiriki mambo ya ndani ya nchi yetu katika Jimbo la Mchinga inafanana sana na hali ilivyo katika kambi za wageni katika Mikoa ya Kigoma na Tabora hasa Ulyankulu na Katumba. Katika maeneo hayo wageni wamekuwa wengi wanafanya maamuzi kwa ajili ya Watanzania waliopo pale. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaangalia wakimbizi wale wasifanye maamuzi yanayohusu Watanzania? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za nchi yetu zimeweka wazi namna ambavyo wageni wataingia nchini na shughuli zao zote zinaratibiwa kwa mujibu wa sheria. Inapotokea kuna wageni wowote wameingia nchini wanafanya mambo kinyume na sheria tafsiri yake ni kwamba wanavunja sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu limeletwa hapa Bungeni, tunalipokea na tutalifanyia kazi kuhakikisha kwamba wageni wote waliopo huko wafuate sheria za nchi yetu na pia tunawaagiza maafisa wetu wa Serikali kuhakikisha kwamba wanalifuatilia jambo hilo ili waweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, bado linaelekezwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Na. 69

Umuhimu wa Serikali Kuzisimamia Taasisi Binafsi Kulipa Mishahara Stahili

MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. GODBLESS J. LEMA) aliuliza:-

Mishahara ya taasisi za umma hupangwa na Serikali. Utaratibu huo wa Serikali kupanga mishahara ya watumishi wake huathiri pia upangaji na ukadiriaji mishahara katika taasisi binafsi.

Je, Serikali haioni haja ya kuboresha mishahara yake na kuzielekeza taasisi binafsi kulipa mishahara inayoendana na hali ya maisha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha mishahara ya watumishi wake wa kada mbalimbali kila mwaka kwa kutoa nyongeza kulingana na kanuni za kiutumishi ikiwa ni pamoja na muda wa kukitumikia cheo au kupandishwa cheo mtumishi. Sambamba na utaratibu huu Serikali imeunda Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara ambayo hufanya utafiti kwa kuzingatia hali halisi ya maisha na uwezo wa kibajeti wa Serikali na kumshauri waziri mwenye dhamana na masuala ya utumishi wa umma kupanga kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 kama ilivyoboreshwa mwaka 2015 imeanzisha Bodi ya Mishahara ya Sekta Binafsi ambayo ina jukumu la kufanya utafiti kwa kuzingatia hali halisi ya gharama za maisha na masuala mengine ya kiuchumi na

kupendekea kiwango cha kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi. Serikali hivi sasa ipo katika hatua za kuiwezesha bodi hiyo kufanya utafiti ili kuhakikisha utafiti huo unakidhi matakwa ya sheria, kanuni na taratibu zinazokubalika hapa nchini na viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kuhakikisha maslahi ya wafanyakazi na ukuzaji wa tija na uzalishaji sehemu za kazi unaboreshwa kila mwaka, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 kama ilivyorekebishwa mwaka 2015, imeweka utaratibu kwa waajiri na wafanyakazi katika sekta binafsi kujadiliana na kufunga mikataba ya hali bora mahali pa kazi kwa lengo la kuboresha maslahi yao ikiwemo mshahara na stahiki nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia utaratibu huu wa kisheria waajiri katika sekta binafsi wanaruhusiwa kuwalipa viwango vya mishahara hata zaidi ya kiwango kinachowekwa kama kima cha chini cha mshahara pale ambapo wanaona kwa kufanya hivyo itaongeza motisha kwa wafanyakazi wao kufanya kazi kwa bidii na kujituma kwa lengo la kuongeza tija katika kuzalisha mali au katika kutoa huduma.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru kwa majibu ya Serikali, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sehemu ya mwisho ya jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba sekta binafsi wanaruhusiwa hata kuongeza kile kiwango ili kuwapa motisha na tunaelewa kwamba motisha ndiyo kila kitu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukatuambia ni kwa nini Serikali mpaka leo haijawalipa watumishi wake *annual increment* ambayo ipo kisheria *(statutory)* na unakiri kwamba hii inasaidia sana motisha na sisi tunajua motisha ndiyo inaweza kusaidia maendeleo ya nchi hii. Je, unaweza kutupa hiyo ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia sekta binafsi pamoja na kwamba wana viwango vya juu lakini pia wana viwango vya chini sana na wale wafanyakzi wa chini wanapata hata pungufu ya shilingi laki moja. Je, Serikali inasema nini kuhusu hili hasa ikizingatia kwamba shilingi laki moja kwa sasa hivi haiwezi kitu chochote? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri fisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Mavunde, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watumishi wa umma na nyongeza ya mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa likisemwa mara kwa mara hapa Bungeni ya kwamba Serikali si kwamba haitambui kwamba kuna umuhimu wa kufanya *annual increment* kwa watumishi wa umma, kilichotokea ni kwamba baada ya zoezi lile la uhakiki kuhakikisha kwamba tunatengeneza kanzi data ya wafanyakazi ambao wapo hawana changamoto zile za kwenye masuala ya uhakiki na maelekezo yameshatoka kwamba kuanzia hapo sasa Serikali itaona namna bora ya kuweza kulitimiza takwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa shughuli hii ilikwama kwa sababu mtakumbuka kwa mwaka 2016/2017 zoezi la uhakiki liliendelea na kanzi data hiyo ikishatengenezwa vizuri naamini kabisa kwamba jambo hilo litatimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusiana na suala la kima cha chini katika sekta binafsi. Kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 kifungu cha 37 kimetoa mamlaka kwa Bodi ya Mishahara iliyoanzishwa kufanya uchunguzi wa kina na utafiti kuhusiana na ongezeko la mishahara ya sekta binafsi na baadaye kumshauri waziri mwenye dhamana ili aweze kutangaza kutokana na hali halisi ya wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nilitangazie Bunge lako kwamba tayari bodi hii imeshaundwa na muda siyo mrefu inaanza kazi yake kuhakikisha kwamba jambo hili wanalifanyia kazi kwa utafiti na baadaye kumshauri Mheshimiwa Waziri ili sasa kuja na viwango vya kima cha mshahara kutokana na hali halisi ya wakati huo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini na linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 70

Eneo la *Tanganyika Packers* Katika Mji wa Mbalizi

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Katika Mji Mdogo wa Mbalizi kuna ardhi ya ukubwa wa zaidi ya ekari 5,000 iliyotengwa kwa ajili ya *Tanganyika Packers* ambayo haijaendelezwa kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita.

(a) Je, ni lini Serikali itawarudishia wananchi wa Mji Mdogo wa Mbalizi eneo hilo kwa lengo la kuliendeleza kwa kubadili matumizi kutokana na kukua kwa kasi kubwa kwa Mji wa Mbalizi?

(b) Pamoja na kubadili matumizi ya ardhi hiyo, je, Serikali ina mpango gani kwa wananchi wanaotumia ardhi hiyo hasa ikizingatiwa kuwa wengi wao hawakupewa fidia yoyote?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba namba 760 lenye hekta 102.4 na shamba namba 761 lenye hekta 1985.4 yaliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambayo kwa pamoja yana ukubwa wa hekta 2,087.8 sawa na ekari 5,219.5 ni mali ya Serikali. Mwaka 1974 Serikali ilijenga Kiwanda cha Kusindika Nyama cha *Tanganyika Packers* kwenye shamba namba 760 na shamba namba 761 lilikuwa maalum kwa ajili ya kupumzisha mifugo na kuilisha vizuri kabla ya kuchinjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uzalishaji kiwandani kusimama kutokana na changamoto kadhaa za kiuendeshaji na kiuchumi, baadhi ya wananchi walivamia maeneo ya mashamba hayo na tarehe 4/3/2016, Halmashauri ya Wilaya iliomba kwa Msajili wa Hazina kubadilisha matumizi ya eneo hilo kuwa makazi na huduma nyingine. Ombi hilo lilikataliwa kwa kuwa nia ya Serikali kuliendeleza eneo hilo kama eneo la viwanda haijawahi kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo maana ili kuona kuwa haki inatendeka Serikali ilifungua kesi Namba 1 ya mwaka 2015 Mahakama Kuu, Kanda ya Mbeya dhidi ya wavamizi ambayo ilihukumiwa tarehe 20/2/2018 kwa Serikali kupewa haki ya kuendeleza eneo lake. Taratibu za kisheria za kuwaondoa wavamizi ili eneo hilo litumike kama ilivyokusudiwa zitakamilishwa hivi karibuni. Serikali haijawahi na haina mpango wa kubadili matumizi ya eneo hilo, kwani kufanya hivyo kwa maeneo kama hayo ni kukwamisha juhudi za kujenga Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo wananchi waliokuwa wanastahili fidia kwa mujibu wa sheria wote walilipwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, na ni nia ya wananchi kuona kuwa eneo hilo linatengwa na

kunakuwepo na viwanda ili wananchi wa Mbeya waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo mikakati mizuri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya kumalizia Kiwanda cha Kuchakata Nyama ambacho kimejengwa na Halmashauri ya Mbeya na ambacho vyombo vyote, vifaa vyote zaidi ya miaka miwili sasa viko mle ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa vile kuna wafugaji wengi katika Kata ya Mjele na tatizo lao kubwa ni mabwawa ya maji, je, ni lini Serikali sasa itapeleka miundombinu ya mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo na binadamu? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Kakunda, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kwamba amekubaliana na majibu ya Serikali kwenye swali la msingi na katika maswali yake mawili ya nyongeza, la kwanza, kuhusu mradi wa kiwanda cha kusindika nyama pale Mbalizi ambao uliwasilishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini TAMISEMI kwa ajili ya kufikiriwa kupewa fedha ni miongoni mwa miradi ya kimkakati katika halmashauri hiyo ambayo imeombewa fedha kwenye dirisha maalum la miradi ambayo ni miradi ya kibiashara.

Kwa hiyo, mchakato wake bado unaendelea, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha miradi hiyo yote bado inafanyiwa upembuzi maalum ili utakapokamilika miradi ile ambayo itapatiwa fedha wahusika wa Halmashauri wataarifiwa. Hata hivyo ninaamini mradi huo ni mzuri na una faida na miradi kama hiyo Mbeya haipo mingi, kwa hiyo, ninaamini utapewa kipaumbele unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusu bwawa kwenye eneo la wafugaji. Najua Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi alitembelea eneo hilo na akatoa ahadi. Mimi nataka nimwambie kwamba Serikali hii ni moja, nitafuatilia mimi mwenyewe kwa Wizara ya Mifugo ili kuhakikisha kwamba Halmashauri na wakazi wa eneo hilo wafugaji wanapata kile ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri alikiahidi. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Yahaya Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyoko huko Mbalizi yanafanana kabisa na yaliyoko katika Halmashauri ya Itigi ambapo shamba la *Tanganyika Packers* eka 45,000 ambalo lipo pale kwa miaka mingi limetelekezwa na Serikali imekuwa na kauli tata juu ya shamba hili wakati tukiliomba lirudishwe kwa wananchi au kuanzishwe mradi mwingine, kwamba litarudishwa, baadae Serikali inasema italichukua. Sasa nini kauli sahihi ya Serikali kwa shamba la *Tanganyika Packers* ambalo limeachwa na limetelekezwa kwa muda mrefu katika Halmashauri ya Itigi?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Kakunda.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisisitize kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kwamba maeneo kama lile la *Tanganyika Packers* Mbeya na maeneo mengine ya aina hiyo Serikali haina nia ya kubadilisha matumizi ya msingi yaliyokusudiwa kwa ajili ya kuendeleza maeneo hayo katika sekta ya viwanda.

Kwa hiyo, maeneo hayo ni lazima yaendelee kutengwa na kutunzwa kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya viwanda. Kwa hiyo, maeneo hayo ni ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndugu yangu Mheshimiwa Yahaya naomba tushirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kuhakikisha kwamba eneo hilo linaendelea kulindwa na miongoni mwa maeneo ambayo ni ya halmashauri ya wilaya ambayo mnatakiwa myalinde kikamilifu kwa ajili ya sekta ya viwanda na uwekezaji kwa ujumla ni eneo hilo, kwa hiyo, naomba sana tushirikiane katika hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya maeneo ambayo kulikuwa kuna viwanda vya *Tanganyika Packers* ni Jimbo la Kawe, Kata ya Kawe ambayo miaka sita iliyopita kwa kushirikiana na Serikali ya Awamu ya Nne tulifanikiwa kuliokoa eneo husika kutoka kwa waliokuwa wawekezaji uchwara na hatimaye Shirika la Nyumba la Taifa likakabidhiwa kupewa jukumu la kujenga Kawe Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tokea Awamu ya Tano imeingia madarakani...

MWENYEKITI: Uliza swali tu Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea Awamu ya Tano imeingia madarakani, mradi ule ambao ulikuwa unahusisha nyumba zaidi ya 50,000 ni kama vile umekwama, matokeo yake eneo lile linakuwa kama sehemu ya genge la majambazi na wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka Serikali iniambie, ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba ujenzi wa Kawe Mpya ya kisasa unafanyika kama ambavyo ilikuwa ni katika mpango wa miaka mitano na mwaka mmoja mmoja wa Serikali?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Angeline Mabula.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mpango wa Serikali kujenga nyumba kama ilivyokuwa imepangwa kwa *National Housing* ulikuwa umepangwa na ulikuwa unaendelea vizuri, lakini mpango ule ulisimama baada ya kuja kuongeza nguvu katika ujenzi wa nyumba za Makao Makuu hapa Dodoma. Hata hivyo, kwa sababu suala zima la ujenzi wa nyumba za hapa Dodoma unaendelea vizuri, miradi mingine yote iliyokuwa imesimama sasa hivi wataanza kuitekeleza kwa sababu utaratibu tayari umeshawekwa vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linakuja kwenye haya mashamba. Katika Jimbo la Mlimba, Kata ya Namwawala, Vijiji vya Idandu, Miomboni na Namwawala sasa hivi kuna hekaheka kubwa kuzuia wananchi kwenda kulima mashamba yaliyokuwa eneo la *Ramsar* na matokeo yake na huku kijijini kwenyewe wanasema kuna uwekezaji wa sukari, lakini mpaka sasa Serikali hawasemi chochote kuhusu wananchi hao na Waziri Mkuu anajua, aliniahidi atakuja kutatua hiyo migogoro ili wananchi wawe kama *outgrowers.*

Je, lini sasa Waziri atakwenda Jimbo la Mlimba katika maeneo haya kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata mahali salama pa kulima na pa kuishi katika Kata ya Namwawala na Mofu?

MWENYEKITI: Umeeleweka Mheshimiwa Susan. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Kakunda, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema yeye mwenyewe, maeneo

ambayo ni mashamba halafu hapohapo akataja jambo kubwa kabisa katika mazingira duniani linaitwa Ramsar, maeneo ambayo yametengwa kama *Ramsar Sites* ni maeneo ambayo hayastahili kuvamiwa au kutumiwa kwa maendeleo ya aina yoyote, yanatakiwa kulindwa, kuhifadhiwa kwa ajili ya mazingira. Mimi nadhani suala hili tutaendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanatunzwa vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa January Makamba.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongeza katika majibu mazuri kabisa yaliyotolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ni sahihi kabisa kwamba uhai wa ikolojia ya Mto Rufiji unategemea sana afya ya maeneo haya yaliyohifadhiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Ramsar. Kwa hiyo matumizi ya maeneo yale lazima yawe uangalifu na Serikali kabla ya kuruhusu kazi za kilimo, ufugaji na matumizi ya kibinadamu, lazima ifanye utafiti wa kutosha na wa kujiridhisha ili tusije tukaharibu mifumo ya ki-ikolojia ya nchi yetu kwa kuruhusu shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ambayo hayastahili kabisa kufanyika shughuli hizo.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, bado linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 71

Kata ya Nkwenda Kujengewa Barabara kwa Kiwango cha Lami

MHE. ANATROPIA L. THEONEST aliuliza:-

Nkwenda I ni kata ya kibiashara yenye wakazi wengi, na Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, wakati wa kampeni

katika Uchaguzi Mkuu wa 2015 aliahidi kujenga barabara kwa kiwango cha lami.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kujenga kilometa kadhaa za lami ili kupunguza adha wanazopata wafanyabiashara hao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliahidi kujenga barabara yenye urefu wa kilometa tano katika Wilaya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kutekeleza ahadi hii zimekwishaanza na katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)* imetenga shilingi milioni mia tatu hamsini kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa moja kwa kiwango cha lami Makao Makuu ya Wilaya ya Kyerwa (Rubwera). Ujenzi huu unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2018. Serikali itaendelea kujenga barabara za lami Wilaya ya Kyerwa kwa awamu ili kutimiza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweke rekodi sahihi; swali langu halijajibiwa, nimeuliza kilometa tano za lami zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni katika Kata ya Kyerwa. Hii ni kata ya mjini, ina wafanyabiashara

wengi, ina shughuli nyingi za kibiashara lakini watu wanateseka na adha ya vumbi inayosababisha ajali mbalimbali za mabasi, boda boda na magari mengine.

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Swali ni lini kilometa tano alizoahidi Mheshimiwa Rais katika Kata ya Nkwenda – kata ya kibiashara – zitajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tumeshuhudia taharuki na bomoa bomoa katika Kata hii ya Nkwenda ambayo hatuoni kama imetengewa bajeti lakini bomoa bomoa na X zinaendelea. Swali, wale wanaowekewa X na kubomolewa nyumba zao watapewa fidia kwa kuwa hakukuwa na ramani ya mpangomji na ramani sasa inawafuata watu wakiwepo pale; watapewa fidia katika maeneo yao ambayo yanakwenda kupitiwa na bomoa bomoa ya ujenzi wa barabara?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika majibu yangu ya msingi, unapoanza kujenga kilometa tano ukaanza na kilometa moja tayari ulishaanza ujenzi kuelekea kilometa tano ambazo Mheshimiwa Rais ilikuwa ahadi yake. Kwa hiyo, nimemhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo wajibu wake ni kutekelezwa ndani ya miaka mitano na kuhakikisha kwamba ahadi hizo zinatekelezwa ndiyo maana tunaanza na kilometa moja. Ukijenga kilometa moja katika tano zinakuwa zimebaki kilometa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia anauliza juu ya wananchi kulipwa fidia. Sheria iko wazi, kwa wale wananchi ambao wameifuata barabara ambayo; hatuwezi wakati huo

huo tukataka maendeleo na wakati huo huo tukataka tubaki katika hali ile kabla ya maendeleo. Kwa hiyo, kwa wale ambao wameifuata barabara hawatalipwa na wale ambao barabara imewafuata watalipwa kwa mujibu wa sheria.

MWENYEKITI: Ahsante; Mheshimiwa Sanga, Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Rais, mgombea wakati ule 2015 aliahidi Makambako Mjini kutupatia kilometa sita za lami; na kwa kuwa Serikali tayari imeanza kutupatia mita 150 ambazo tayari zimeshajengwa na mkandarasi ameondoka; na tayari tena atakuja kujenga mita 150. Kwa nini sasa mkandarasi huyu amekuwa akija mita 150 gharama itakuwa ni kubwa, kwa nini asianze kujenga kilometa sita zote kwa pamoja ili kukwepesha gharama ya Serikali isiwe kubwa?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Jah People* (Mheshimiwa Deo Sanga), Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, ahadi ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Rais wakati akiomba kura kwa Watanzania ziko nyingi, na ziko za aina tofautitofauti. Zile ambazo zinahitaji fedha nyingi zinaratibiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na zile nyingine ambazo ni idadi ndogo ya kilometa ambazo

zinajengwa zinaratibiwa kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI na ndiyo kama hiyo ya Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kama ilikuwa ni kilometa sita na Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba tayari tulishajenga mita 150 na nyingine 150, naomba nimhakikishie kwamba kabla ya miaka mitano kukamilika ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa kilometa sita tutakuwa tumekamilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hussein Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wangu wa nane nikiuliza swali la ahadi ya viongozi wetu ambao wamefika katika Jimbo la Nyang'hwale.

Mwaka 2010, Rais wa Awamu ya Nne alikuja akaahidi katika kampeni zake barabara ya lami kutoka Kahama – Nyang'olongo – Busolwa – Karumwa hadi Busisi, Sengerema kujengwa kwa kiwango cha lami. Mwaka 2015 pia Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli alikuja akaahidi vilevile.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kahama – Nyang'hwale mpaka Busisi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Kwandikwa, Naibu Waziri wa Ujenzi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuratibu ahadi za viongozi wakuu, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema. Tayari tunaendelea kufanya uchambuzi ili kuendelea sasa kujenga katika kiwango cha lami. Hata hivyo, kwa barabara hii Mheshimiwa Mbunge anayoitaja kuja Kahama ni barabara ambayo

kwenye mpango mkakati tumeiweka. Tuwasiliane tu uone namna tulivyojipanga kwa sababu tunaendelea kupata fedha kidogo kidogo ili uweze kuona na wakati mwingine uweze kuwapa taarifa wananchi wa Nyang'hwale kwamba ni lini sasa ujenzi utakuwa umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zile hatua za awali tumeshaanza, tunatambua umuhimu wa barabara hii kuiunganisha kutoka Sengerema kuja Kahama. Pia wananchi wajue kwamba eneo la jirani kabisa kutoka Kahama Mjini kwenda Geita, Bunge limepitisha fedha za kutosha, tutaanza ujenzi wa barabara hii ya lami. Kwa maana hiyo tunatambua umuhimu wa kutekeleza ahadi za viongozi pamoja na llani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwahakikishie tu kwamba tunaendelea kuhakikisha kwamba ujenzi wa barabara unafanyika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru sana kwa kuniona; naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kaliua Mjini pale Mheshimiwa Rais aliahidi kilometa tano za lami ndani ya Mji wa Kaliua, na mwaka jana wakati amekuja kwenye ziara yake pia tulimkumbusha akasisitiza kwamba ahadi hiyo itekelezwe kwa wakati. Naomba kujua Serikali itaanza lini utekelezaji wa kilometa tano za lami ndani ya Mji wa *Kaliua Center?* Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Kandege, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI. Ni lini ahadi ya Rais itatekelezwa, basi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi, ahadi zote za viongozi wakuu wa Kitaifa zitatekelezwa. Kwa

kuanzia naomba niwaagize *TARURA* mkoani kwake na hasa Wilaya ya Kaliua wahakikishe kwamba wanatenga katika mwaka wa fedha 2018/2019 ili ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Ujenzi wa kilometa tano ianze kutekelezwa mara moja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kilolo kuna barabara ambayo inaunganisha na Mkoa wa Morogoro, swali hili nimeshaliuliza zaidi ya mara tatu na ahadi ya Serikali ilikuwepo. Hivi leo ninavyozungumza wananchi wa Kimala, Itonya, Muhanga, Idete na Idunda wanafanya kazi kwa mikono, na mimi kama Mbunge nimechangia na wananchi wengine wamechangia.

Je, sasa Serikali itakuwa tayari na yenyewe kuchangia ili wale wananchi wa Kilolo kwa nguvu zao waweze kupasua barabara kuelekea Morogoro ambako naunganishwa na Jimbo la Mheshimiwa Susan Kiwanga?

MWENYEKITI: Huyo huyo, ahsante majibu kwa swali hilo Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Kandege, Naibu Waziri Ujenzi kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZU NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua umuhimu wa kuunganisha Mikoa. Kwa Mkoa wa Iringa tunao mpango wa kuunganisha eneo hili la Kilolo kuja Mkoa wa Morogoro kupitia Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimpongeze tu Mheshimiwa Mwamoto kwa sababu amekuwa mfuatiliaji mzuri na mwenyewe anafahamu hii barabara kutoka Iringa kuja Kilolo na sehemu ambayo ilikuwa inasumbua kwa maana ule mpango wa Halmashauri kufanya marekebisho ya maana *alignment* ya ile barabara; tumetoa maelekezo ili

waweze kurekebisha ili wananchi ambao walikuwa wamepata usumbufu tatizo lao litakuwa limeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge hii eneo hili tunalolizungumza ni kilomita chache sana, lakini kwa sababu ya *nature* ya eneo tunalifanyia kazi ili tuweze kukuunganisha na eneo la Mlimba.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini na bado linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 72

Kupanua Uwanja wa Ndege wa Magena

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Halmashauri ya Mji wa Tarime imebahatika kuwa na Uwanja wa Ndege wa Magena ambao umekuwa ukitumiwa na watalii wanaokwenda Mbuga ya Serengeti, viongozi mbalimbali na hata Mgodi wa Acacia. Miundombinu ya uwanja pamoja na barabara zake ni mbovu sana.

(a) Je, ni lini Serikali itapanua uwanja huu na kurekebisha miundombinu yake ili ndege nyingi ziweze kutua kwa ajili ya watalii waendao Serengeti?

(b) Je, ni kwa nini Serikali haijajenga jengo la Uhamiaji katika uwanja huo ili kutoa urahisi wa watalii wanaotumia uwanja huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege Magena kinachomilikiwa na Halmashauri ya Mji wa Tarime kina urefu wa mita 1,470 na upana wa mita 120. Kiwanja hicho kimekodishwa kwa mwekezaji ambaye ni Kampuni ya *Coastal Aviation* kwa mkataba wa kuilipa Halmashauri kiasi cha milioni 20 kila mwaka. Halmashauri imefanya ukarabati wa baadhi ya miundombinu ya kiwanja ikiwemo kujenga barabara yenye urefu wa kilometa 1.2 kutoka barabara ya Tarime – Sirari kwa kiwango cha changarawe ili kuboresha mazingira ya uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia halmashauri ya Mji wa Tarime ina mpango wa kujenga Ofisi za Uhamiaji ili kuweka utaratibu mzuri wa kuingia na kutoka kwa watalii wanaokwenda hifadhi ya taifa ya Serengeti.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hili swali la kuuliza kuhusu uwanja wa ndege na kuiomba Serikali ione umuhimu wa kuupandisha hadhi huu uwanja utoke kwenye Halmashauri na uende kwenye *Tanzania Aviation Authority*; kwa sababu kwa sasa hivi ilivyo kumkodisha *Coastal Aviation* kwa milioni 20 kwa mwaka anakuwa ana-*monopolize* na kodi ambazo anawataja *aviation* zingine wanavokuja kutoa pale ni nyingi sana; kwa hiyo Serikali tunapoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, ni kwa nini sasa Serikali haioni umuhimu wa kupandisha hadhi huu uwanja na kuukarabati kwa sababu tunapata watalii kutoka maeneo mbalimbali, lakini pia unaweza kutumika kwa ndege kutoka pale kwenda hata nchi jirani ya Kenya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwa nini sasa wameeleza hapa kwamba wamekarabati barabara ya kilometa 1.2, lakini kuna barabara ya kutoka Tarime kupita Magena unaenda mpaka Kata ya Mwema kule ambapo kuna daraja la Mto Moli ni bovu sana hata *Clouds Tv* walionesha.....

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. ESTHER N. MATIKO: ...linahatarisha maisha watu wanaotumia ile barabara. Ni lini sasa Serikali itaweza kujenga daraja lile la Mtomoli sambamba na ile barabara ambayo inaenda Magena kwenye huu uwanja?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Josephat Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kuomba kupandishwa uwanja huu kuchukuliwa na iwe miongoni mwa viwanja ambavyo vinamilikiwa kitaifa haina ubaya. Hata hivyo ni vizuri tukajua chimbuko la uwanja huu. Uwanja huu mwanzo ulikuwa unatumiwa na kampuni hii ambayo inajiita *COGFA* ambao wanajenga barabara ya kutoka Sirari kwenda Makutano. Na wao baada ya kumaliza matumizi yake walimkabidhi Mkuu wa Wilaya, lakini baadae bali katika kugawanyika Halmashauri ya Mji na halmashauri ya *Tarime Town Council* na *DC* ikaonekana kwamba uwanja ule ambao uko kilometa tisa ubaki chini ya umiliki. Ukitazama katika mkataba wao ambao ni suala la wao ndani ya Halmashauri, kwa sababu mkataba umeingiwa kati ya *Coastal Aviation* na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo linaongeleka, kwa kadri watakavyopisha kwenye vikao vyao na wakaridhia kwamba sasa *ownership* ihame sisi kama Serikali hatuna ubishi na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya swali la pili la kujenga daraja, kama ambavo tumekuwa tukitengeneza miundombinu kwa kadri bajeti inavyoruhusu, naomba nimehakikishie Mbunge bajeti ikiruhusu tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba mazingira rafiki kwa ajili ya watalii kwenda mbuga yanajenga, ni pamoja na kujenga kwa daraja.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ndumbaro kwa kifupi sana, swali.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tatizo la uwanja ambalo limeongelewa na Mheshimiwa Matiko ni sawa sawa kabisa na tatizo la Uwanja wa Ndege wa Songea, uwanja ambao unahudumia Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Njombe. Tangu mwezi wa tatu mwaka huu uwanja huo umefungwa na hautumiki tena. Jitihada za Serikali kuleta ndege hazisaidii kwa sababu ndege haziwezi kutua katika uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni, je, ni lini uwanja huo utafanyiwa ukarabati na kuanza kutumika ili kuwanufaisha wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Njombe?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua umuhimu wa huduma hii ya usafiri wa ndege katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliarifu tu Bunge kwamba tulishapata mkandarasi wa kufanya ukarabati wa uwanja huu; taratibu za manunuzi zilikuwa zinakamilishwa ili ujenzi kwa haraka ufanyike. Sambamba na ukarabati wa uwanja huu wa Songea tutafanya pia uwanja wa ndege wa Iringa ili lengo sasa la kuweza kufanya haya mashirika ya ndege yaweze kujiendesha kwa faida kwa maana ya viwanja vyote vitatu cha Mtwara, Ruvuma pamoja na Iringa kwa pamoja tukikarabati tutafanya na wao waweze kufanya kazi kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa vuta subira, tuko tayari kufanya matengezo kwenye uwanja huo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa nataka majibu yawe mafupi, Mheshimiwa Bura uliza kwa kifupi, upate jibu fupi.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya upanuzi wa uwanja wa ndege wa Dodoma na wananchi ambao wanaishi karibu na uwanja ule nyumba zao ziliwekwa alama ya "X" kwa maana kwamba zile nyumba zitavunjwa kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege. Hata hivyo baadhi ya wananchi wamelipwa na baadhi ya wananchi hawalipwa fidia kutokana na nyumba zao kuwekwa alama "X". Naomba kujua ni lini wananchi ambao hawalipwa watalipwa fidia ili waende wakayafanye maendele ya ujenzi wa nyumba kwenye maeneo mengine?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi, Ujenzi Mawasiliano, Uchukuzi *Engineer* Nditiye, lini?

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimtaharifu Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia kesho hao wananchi ambao wanadai fidia zao wataanza kulipwa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako ya uhakika na mafupi, Mheshimiwa Mwalongo.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Njombe una uwanja wa ndege lakini wa nyasi; lakini katika ule uwanja kuna wananchi wana nyumba pembezoni mwa ule uwanja. Hakuna mipaka ya uwanja na hawaruhusiwi kuendeleza maeneo yao. Je ni lini Serikali itaenda kufanya utambuzi na kuwalipa fidia wale wananchi ili wapishe ule uwanja?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalongo jirani yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua changamoto zilizokuwepo kwenye Uwanja wa Ndege wa Njombe na hata hivi karibuni Mheshimiwa wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano amefika Njombe kwa ajili ya kuona namna bora ya kuweza kukamilisha na kuweka mipaka katika eneo hili. Kilichokuwa kimetuchelewesha ilikuwa pia ni wazo la Mkoa kuweza kuomba kuhamisha uwanja katika eneo hili. Hata hivyo baada ya mazungumzo nafikiri sasa tuko tayari kuweka mipaka hiyo ili na ukarabati wa uwanja huu kati ya viwanja 11 uweze kufanyika.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa Mbunge wa...

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya wananchi wa Biharamulo...

MWENYEKITI: ...subiri Mheshimiwa, mbona una kasi sana, sijakuita bado; una nia njema linaulizwa na Mheshimiwa na Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi na lina ulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Na. 73

Miradi ya Jeshi la Kujenga Taifa Kuunganishwa na Jitihada za Vijana

MHE. OSCAR R. MUKASA aliuliza:-

Je, ni lini Jeshi la Kujenga Taifa litakuja na mkakati wa kuwa na miradi itakayounganishwa na jitihada za vijana

wasiokuwa na ajira Wilayani Biharamulo na kwingineko kwa namna isiyohitaji uwekezaji mkubwa wa kujenga Kambi za Kijeshi?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua hitaji kubwa la kuanzishwa Kambi za JKT kwenye Mikoa na Wilaya ambazo hazina Kambi za JKT ikiwemo Biharamulo. Jeshi la Kujenga Taifa limeeleka nguvu kwenye vikosi vilivyoanzishwa awali na baadaye kusitisha shughuli za kuchukua vijana mwaka 1994. Aidha, JKT inaanzisha kambi mpya katika maeneo mbalimbali kwa awamu kwa kadri bajeti yake itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Jeshi la Kujenga Taifa limejikita katika kutoa mafunzo ya stadi za kazi kwa vijana waliojiunga na JKT kwa kujitolea. Lengo ni kuwa endapo vijana hawa watakosa ajira katika vyombo vya Ulinzi na Usalama waweze kujiajiriwa na taasisi nyingine za Serikali, sekta binafsi au wajiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijana wanaopata fursa hii ya kujiunga na JKT kwa kujitolea ni wachache kulingana na mahitaji; wazo la Mheshimiwa la kulitaka Jeshi la Kujenga Taifa kuanzisha miradi iliyohitaji uwekezaji mkubwa na kuwashirikisha vijana wasio na ajira katika maeneo mbalimbali yasiyokuwa na kambi za JKT ikiwemo Biharamulo ni wazo zuri ambalo tunalipokea na tunaahidi kulifanyia kazi ili kuona uwezekano wa kulitekeleza.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa Serikali imeonesha nia ya kufanyia kazi wazo hili na kwa kuwa Biharamulo tuko tayari, Mheshimiwa

Waziri uko tayari kwa hivi karibuni tuje mimi na Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi kwa ajili ya kuanza mazungumzo na wataalam wako wa Jeshi la Kujenga Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Waziri uko tayari kututembelea ili kabla ya maongezi haya hayajaanza uone fursa zilizopo ili maongezi yawe yamesheheni ushahidi na mambo ambayo tumeyaona kwa pamoja?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutembelea niko tayari kufanya ziara katika eneo hilo ili kutambua fursa ambazo zinaweza zikashughulikiwa ili kutoa ajira kwa vijana hao.

Kuhusu mazungumzo na wataalamu wake nina shauri nipate fursa kwanza ya kujadiliana suala hili na wataalam wa JKT ili kuona uwezekano wake na watakapokuwa wao tayari kuja basi wenzao hawa wawe tayari kwa ajili ya mazungumzo haya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya halafu Mheshimiwa Masoud.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza niwapongeze vijana wote wa JKT wanaoendelea kujitolea. Kumekuwa na malalamiko ya kubaguliwa katika upande mzima wa suala la kupewa ajira kwa vijana wanaomaliza JKT hasa ajira ambazo zimetokea kwenye Jeshi la Polisi na hasa katika Operesheni ya Jakaya Kikwete.

Sasa swali langu, nini tamko la Serikali kuhusiana na tabia hii ya kibaguzi, na wapo vijana wa jimboni kwangu?

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kuamua kwa makusudi kujiunga na Mfunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa akiwa hapa Bungeni, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la malalamiko ya ubaguzi wakati wa ajira, nataka nimfahamishe kwamba mara zote kuna kuwa kuna uhaba wa idadi ya vijana wanaoajiriwa ukilinganisha na wale walioko kwenye kambi. Kwa mfano katika kipindi kilichopita jeshi la Ulinzi liliajiri vijana 2,000 kati ya vijana 9,000 waliokuwepo kule; bila shaka wale 7,000 wataona kwamba wamepaguliwa, lakini ukweli ni kwamba nafasi zinakuwa chache wakati wao wako wengi. Ni kweli hivi karibuni Jeshi la Polisi lilitoa ajira, lakini vile vile idadi ya vijana walioajiriwa ni chache sana ukilinganisha na vijana waliokuwepo katika Kambi za JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati mwingine vigezo vya ajira vinaweza vikafanana lakini kwa sababu ya idadi imekuwa ndogo basi kuna wengine bilashaka wataachwa ndiyo hayo yanasababisha malalamiko.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; nina swali moja la dogo la nyongeza.

Serikali au JKT inatoa stadi za kazi ikiwemo suala zima la ushonaji; na Serikali kwa mara kadhaa kwa miaka mingi imesema ina mkakati kabambe wa kuongeza viwanda vya ushonaji nguo na hasa sare zile za jeshi, lakini imeonekana kwamba...

MWENYEKITI: Swali rafiki yangu, uliza swali tu.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: ...inaonekana kwamba kunakuwepo na kusua sua kwenye shughuli hizi, swali, je, Serikali ina mkakati gani wa ziada kuona kwamba

ahadi yake ya muda mrefu ya kuongeza viwanda vya ushonaji nguo sambamba na Tangamsino mbali ya Kamesuma?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunao mkakati wa kuongeza idadi ya viwanda vya kuzalisha nguo katika jeshi letu na tunavozungumza tuna viwanda viwili tayari, kimoja kiko pale katika Kambi ya Mgulani na kingine kipo katika Kambi ya Ruvu. Vinafanya kazi na lengo ni kuviboresha kwanza hivi kabla hatujaanzisha vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ukifika pale kwenye kambi ya Mgulani utaona kwa macho yako kwamba kwa kweli juhudi kubwa zimefanyika. Sasa hivi nguo za kombati kwa mfano hatuagizi kutoka nje zina vitambaa vinanunuliwa hapa na zinashonwa hapa. Kwa hiyo, tumeanza na juhudi hiyo na hatua kubwa imepigwa na tutaendelea kuendeleza juhudi hizo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 74

Umuhimu wa Rasilimali Watu Katika Uchumi wa Viwanda

MHE. JUMA OTHMAN HIJA aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuandaa rasilimali watu ili kufanikisha azma nzuri ya uchumi wa viwanda kwa nchi?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutoa fursa sawa ya elimu kwa wote Serikali mpaka sasa inatumia takribani shilingi bilioni 23.85 kwa mwezi sawa na shilingi trilioni 1.14 kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2018/2019 kwa ajili ya kuwaandaa vijana kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne yaani elimu bure. Pia kutoa ruzuku pamoja na mikopo ya takribani trilioni 1.81 kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2018/2019 kwa wanafunzi wa taasisi ya elimu ya juu ili kuwandaa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imeandaa Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi kwa Sekta za Vipaumbele kwa Vijana ambapo kwa sehemu kubwa mafunzo hutolewa kwa vitendo mahali pa kazi. Programu hii hutekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa utatu yaani Serikali, vyama vya waajiri na sekta binafsi na vyama vya wafanyakazi. Utekelezaji wa programu hiyo ulianza mwaka wa fedha 2015/2016 kwa kutumia mifumo ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo kwa vitendo mahali pa kazi kwa njia ya mafunzo ya kukuza ujuzi kupitia wanangezi *(apprenticeship)*, kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo usio rasmi wa mafunzo *(recognition of prior learning skills),* mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kwa wahitimu *(internship)* na mafunzo ya kukuza ujuzi kwa walio makazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar pia kupitia Kituo cha Kulelea Wajasiriamali *(Entrepreneurship Incubation Centre)* kilichopo chini ya Wizara ya Kazi baadhi ya vijana, makundi ya walemavu na watu wenye uhitaji maalum, hupatiwa mafunzo ya ujasiriamali, ambapo Taasisi ya *COSTECH* iliwawezesha jumla ya shilingi milioni 206 ili

kuanzisha kituo hicho na mpaka sasa jumla kimewanufaisha wajasiriamali 875 wengi wao wakiwa ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ujuzi mbalimbali kulingana na mahitaji ukiwepo ujuzi wa uzalishaji viwandani kuhakikisha nchi yetu inajitosheleza hatua kwa hatua katika eneo hili. Napenda kutoa wito kwa vijana kujitokeza na kushiriki katika fursa hizo za mafunzo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Othman Hija.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake marefu lakini ambayo hayakujibu swali langu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la msingi ni kwamba nilikuwa naulizia matayarisho ya rasilimali watu ambao watakuja kuendesha viwanda vyetu. Mheshimiwa Waziri amenijibu mambo ya mikopo, elimu na kadhalika. Nilichokuwa naulizia hapa ni kwamba sisi sasa hivi tuna siasa ya kuendesha viwanda. Je, tuna matayarisho gani ya kuja kuendesha hivi? Tuna matayarisho kwamba kwa mfano, mtu anaweza akawekeza viwanda lakini baadaye viwanda vile vikaja vikaendeshwa na watu kutoka nje ya nchi. Je, sisi Watanzania tuna matayarishoi tgani ya kuja kuendesha viwanda hivi? Hilo ndiyo swali langu lilikuwa la msingi lakini siyo suala hili ambalo Mheshimiwa Waziri amenijibu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya msingi aliyoanza nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/2015 Serikali ilifanya tafiti kubwa mbili muhimu sana kwneye nchi yetu. Utafiti wa kwanza ni kujua aina ya nguvukazi tuliyonayo na

utafiti wa pili ni aina ya ujuzi uliopo katika nguvukazi tuliyonayo wa kuweza kukidhi uchumi kwenye sekta za vipaumbele ambavyo vimewekwa kwenye mpango wa maendeleo, na hasa kwenda kwenye uchumi huo wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya tafiti mbili hizo kubwa kufanyika mpaka sasa ndani ya nchi yetu tunajua mahitaji ya ujuzi katika uchumi wa viwanda yanapungukiwa kwenye maeneo yapi. Ndiyo maana Ofisi ya Waziri Mkuu baada ya kugundua hayo mahitaji ya ujuzi unaohitajika kwenye viwanda na Waheshimiwa Wabunge kila mwaka mmekuwa mkitutengea bajeti ya shilingi bilioni 15; sasa bilioni 15 hizo ndizo zinazotumika kwenye programu tano alizozisema Mheshimiwa Naibu Waziri na nyingine za kujenga ujuzi kwa mahitaji ya viwanda vilivyoko katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Wabunge jambo hilo tunalielewa na tunalifanyiakazi vizuri sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khadija Nassir.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya uchumi ya nchi yoyote inatakiwa kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na sekta wezeshi kama sekta ya elimu ili kuweza kuleta matokeo chanya. Sasa Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kubadilisha mitaala yetu ya elimu ili kuweza kuendana na sera ya uchumi wa viwanda?

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, mitaala ibadilishwe.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze

Mheshimiwa Khadija kwa kufungamanisha sera hii ya uchumi na namna ya kuwezeshwa kupitia elimu; na ndiyo maana hata kwenye majibu ya msingi tunazungumza hayo. Ni kwamba tunapozungumzia kufanya uwezeshi katika ujenzi wa uchumi ni lazima huyu mtu awe ameandaliwa kielimu lakini vile vile kimafunzo ya ujuzi.

Kwa misingi hiyo sera zetu zote sasa hivi zimekuwa zikifanya kazi kwa pamoja kuangalia maeneo gani yanaweza yakaongezewa nguvu na pia kuangalia kwamba sera zetu zinazungumza na kuweza kuleta matokeo chanya. Kwa hiyo, kupitia Wizara ya elimu vilevile kuna mafunzo ambayo yamekuwa yakitolewa katika vyuo vyetu vikuu, lakini vilevile katika vyuo vya ufundi ili kuwezesha kuona kwamba hawa wahitimu wanatekeleza majukumu yao vizuri katika ujenzi wa uchumi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Selasini.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya nchi yetu ya Tanzania imekuwa kama ni laana kwa mwanafunzi kufeli darasa la saba au *form four,* lakini India, mainjinia leo wanaoendesha mitambo ya *gas and petroleum* ni wale waliofeli darasa la saba.

Je, Serikali yetu lini itaona umuhimu wa kuwaendeleza vijana waliofeli darasa la saba na *form four* ili na wao waje kuwa mainjinia katika viwanda vyetu na mitambo yetu Nchini?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, *Engineer* Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali na nchi

kwa ujumla inathamini kila rasilimali ya mwananchi iliyopo nchini na ndiyo maana kupitia vyuo vyetu vya *VETA,* kupitia *FDC,* kupitia mafunzo yasiyo rasmi imekuwa ikiendelea kutoa mafunzo ili kuhakikisha kwamba vijana hao wanaendelea kuajirika na kujiajiri wao wenyewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkazo uliwekwa vizuri sana katika elimu ya msingi na elimu ya sekondari tulipojenga shule nyingi sana za kata. Mkazo pia umewekwa kwa elimu ya juu kwa maana ya vyuo vikuu. Hata hivyo vijana wengi sana baada ya kumaliza *form four* na *form six* wana-*hang* hapa katikati hawana pa kwenda na viwandani wanahitajika sana...

MWENYEKITI: Uliza swali sasa Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: ... kama mafundi mchundo na kadhalika. Sasa, je, Serikali ina mkakati gani na vijana hawa kuwapa elimu ambayo baadae itawasaidia kuwa mafundi mchundo na kazi nyingine za viwandani badala ile elimu ya chuo kikuu ambayo inatengeneza mameneja zaidi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Injinia Manyanya Stella.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika ngazi za kati hatuna mafundi wa kutosha kama ambavyo ameeleza Mheshimiwa Selasini, lakini niseme tu kwamba jitihada zimeendelea na kama tutakumbuka mara ya mwisho kupitia Bunge lako tukufu tuliweza hata kupitisha uwezekano wa makundi hayo kupewa mkopo ili kuweza kuziba hayo

mapengo. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kufanyiakazi ili kuweza kuona kwamba maeneo hayo yanaimarishwa na vijana wengi zaidi wanapatikana kutoka katika makundi hayo.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki nab ado linaenelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 75

Ujenzi wa Soko la Kimataifa Kata ya Mwangenza

MHE. ALLAN J. KIULA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga soko la kimataifa katika Kata ya Mwangenza kwa ajili ya kuweka katika madaraja vitunguu vinavyolimwa maeneo hayo ili kuvisafirisha katika masoko ya ndani na nje ya nchi?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimniwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wakulima wa zao la vitunguu katika Wilaya ya Mkalama na Iramba wanakabiliwa na ukosefu wa miundoimbinu rafiki ya soko. Katika hatua ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto hii, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imetenga eneo la ukubwa wa mita za mraba 19,600 kwa ajili ya kujenga soko maalum la vitunguu. Eneo hilo lipo katika Kijiji cha Dominic na linamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa bajeti wa mwaka 2017/2018 kupitia fedha za ruzuku ya maendeleo *(Capital Development Grants),* Halmashauri ilipewa jumla ya shilingi milioni 40 ambazo zimetumika kuanza ujenzi awamu ya kwanza kwa kujenga uzio wa soko, vyoo kwa ajili ya wafanyabiashara na sehemu maalum ya kuanikia vitunguu yaani vichanja kwenye soko hilo. Kwa sasa eneo hilo linaendelea kutumika kama soko la vitunguu na Halmashauri hiyo imenunua mzani mmoja kwa ajili ya kupima uzito wa bidhaa hizo hivyo kusaidia wakulima kuachana na vipimo vya lumbesa ambavyo vimekuwa vikiwakandamiza kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi matakwa ya masoko makubwa na maalum ya ndani na nje ya nchi, Wizara yetu kupitia wakala wa vipimo imeshauri Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI wanapoanza ujenzi wa soko awamu ya pili uhusishe sehemu ya vifaa vya kuweka madaraja na kufungasha vitunguu kwa viwango vya kimataifa.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa soko ni kitu muhimu sana hasa ukizingatia eneo hili vijiji vinavyozunguka Miganga, Mwanga na Nkalakala vinalima sana vitunguu na kilimo ni uti wa mgongo, na tunakwenda kwenye uchumi wa kati na uchumi huo lazima uwe *supported (to be supported)* na kilimo. Je, Serikali lini itatoa uwekezaji wa kutosha kuweza kujenga soko kubwa na la kisasa maana hapa tumeanza tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; upangaji wa madaraja na ufungashaji wa vitunguu unakwenda sambamba na utangazaji wa bidhaa hiyo ambayo ni vitunguu. Serikali inachukua hatua gani kutangaza bidhaa hii ambayo tunatambua kwamba inakwenda katika nchi

jirani za Kenya, Mauritius na Sudan Kusini. Ni lini Serikali itachukua hatua za kutangaza bidhaa hii?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Baishara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Allan Kiula ambavyo tumekuwa tukishrikiana katika suala hili. Niseme tu kwamba naishauri Halmashauri wakati wa bajeti itakapokuja tutenge fedha za kutosha na sisi kwa upande wetu Wizara tutaangalia kila uwezekano unapojitikeza kuweza kusaidia soko hili liweze kupata fedha za kutosha na kulifikisha katika kiwango cha kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu kutangaza vitunguu vya maeneo hayo, niseme tu kwamba ni kweli vitunguu vinavyotoka kwa ujumla wake katika Mkoa wa Singida ni vizuri sana. Niwaombe Watanzania wote kutumia vitunguu hivyo, lakini pia tutaendelea kutangaza kimataifa na wakati wa shughuli za Sabasaba zinapojitokeza waje pia katika maonesho ili kutangaza vitunguu hivyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jadi Mgeni.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa swali la nyongeza.

Kwa kuwa viwanda vingi vimejengwa Nchini ili kuleta uchumi wa viwanda lakini viwanda vingi havifanyikazi kwa ukosefu wa malighafi.

Je, ni viwanda vingapi vilivyojengwa vya kuchakata ili kuondoa tatizo hili na kuipa Serikali mzigo kuagizia malighafi kutoka nje?

MWENYEKITI: Ahsante, jibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kimsingi ni swali la kitakwimu, lakini vilevile niseme tu kwamba kwa hali ya sasa, katika usindikaji wa mazao wananchi wenyewe wamekuwa msitari wa mbele katika kujifunza na kisindika mazao na kwa kutumia taasisi zetu kama *SIDO* wamekuwa wakipewa mafunzo ili kusindika mazao hayo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Soko la Kimataifa la Lemagwi ambalo lilikuwa limejengwa na baadaye kutelekezwa, liko Wilayani Tarime, ambalo lingeweza kusaidia kuuza mazao mbalimbali. Tungependa kujua, ni lini Serikali itamaliza kujenga hilo soko ambalo limetumia zaidi ya *billions* za Watanzania na baadae limetelekezwa?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu ni lini mtakamilisha ujenzi wa soko hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali wka kuzitaka halmashauri zote ambazo zina miradi ya kimkakati ambazo wana uhakika katika uwekezaji pesa inakwenda kupatikana ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya kwao, ni vizuri wakahakikisha kwamba andiko linakamilika ili kama kuna sehemu ambayo Serikali inahitaji kuwekeza nguvu yake tujue *exactly* nini ambacho tunakwenda kukipata kama halmashauri kabla ya nguvu kubwa haijawekezwa huko.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maria Kangoye.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Vijana na wanawake wengi wa Kitanzania wamekuwa na jitihada kubwa sana katika kilimo hususani cha mbogamboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imefanya jitihada zipi za kuhakikisha kwamba bidhaa za shamba zinasindikwa nchini?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu kwa kifupi sana, ni lini.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kama ambavyo nimezungumza hapo awali, kwa kupitia miradi ambayo *SIDO* imekuwa ikiendeleza pamoja na wadau mbalimbali, kwa kweli usindikaji wa mazao sasa hivi umekuwa ni mzuri zaidi. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, inapotokea katika maonesho ya saba saba tafadhalini hebu mpitie muone bidhaa ambazo sasa hivi hawa Watanzania wanazifanya. Ziko katika viwango vya hali ya juu na tutaendelea kuwezesha kuona kwamba wajasiriamali hao wanapata ubora zaidi katika bidhaa zao.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea; swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Susana Chogisasi Mgonukulima, Viti Maalum, linaelekezwa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na. 76

Huduma Zitolewazo kwa Faru Fausta

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA aliuliza:-

Serikali inamhudumia Faru Fausta kwa gharama ya shilingi milioni 64 kwa mwezi na ambae hazalishi kutokana na kuwa ni mzee sana lakini Serikali hiyo haiwezi kumhudumia mwananchi aliyezeeka ambae hawezi kufanya shughuli zozote za kujikimu maisha na hana mtu wa kumsaidia.

Je, ni kipi kilicho muhimu zaidi kwa Serikali kati ya Faru Fausta au mwananchi mzee asiyeweza kufanya lolote na hana wa kumsaidia?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonukulima, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Faru Fausta amekuwepo eneo la Hifadhi ya Ngorongoro tangu mwaka 1965. Kwa sasa Faru huyu ndiyo mwenye umri mkubwa kuliko wote duniani. Kutokana na uadimu wa wanyama hao, uwepo wa Faru Fausta umekuwa kivutio kikubwa kwa watalii na watafiti wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia kwa kiwango kikubwa mapato ya hifadhi ya Ngorongoro na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzee, Faru Fausta alijeruhiwa na fisi tarehe 9 Septemba, 2016 hivyo kulazimisha atunzwe kwenye kizimba *(cage)* kwa ajili ya uangalizi maalum ambao unahusisha matibabu, chakula na ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa iliyokuwepo kipindi ikilichopita ilitokana na hali ya dharura iliyohitajika ikiwemo miundoimbinu, ulinzi, matibabu na malisho maalum ambapo matumizi kwa mwezi yalikuwa ni takribani shilingi 1,435,571. Kwa sasa afya ya Faru Fausta inazidi kuimarika kadri siku zinavyozidi kwenda hivyo gharama za uangalizi zimeshuka hadi kufikia shilingi 285,000 kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Faru Fausta si kwamba ni muhimu kuliko binadamu wazee bali uamuzi wa kumtunza kwenye kizimba ulifanyika kwa lengo la kunusuru maisha yake ili hatimaye aendelee kuwa kivutio cha utalii na kuingiza fedha za kigeni nchini. Fedha zote hizo zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonukulima.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu ya Waziri naomba niulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu ya Waziri, utunzwaji wa Faru Fausta umewezesha kulitumikisha taifa kwa gharama kubwa kuliko wazee wa Tanzania waliofanyakazi ya kuleta haki na amani katika Taifa hadi Faru Fausta kuonekana ni wa muhimu ni kwa ajili ya amani iliyopatikana kwa wazee hawa. *(Makofi)*

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni ni wakati sasa wa kuhakikisha wazee wa taifa hili wanatunzwa kama vile gharama zote anavyotunzwa faru Fausta ili waweze kuleta amani katika nchi hii?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuwa kwa majibu ya Waziri amesema anahifadhiwa na ana ulinzi mkali, hivyo hata watalii hawamuoni, hizo fedha za kigeni zinazopatikana zinatokana na nini na wakati amehifadhiwa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na Utalii.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niweke *record* vizuri kwa dada yangu Mheshimiwa Mbunge kwamba wanyama wana haki sawa kama binadamu wengine na huyu mnyama kutokana na uadimu wake, na kwamba ni moja ya wanyama ambao wapo hatarini kutoweka ndiyo maana tumemweka kwenye ulinzi maalum. Kutokana na umuhimu wake huo na kutokana na jinsi ambavyo ameliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na kutokana na kwamba watu wengi wanataka kujua maisha yake kwamba ataishi miaka mingapi, maana mpaka sasa hivi ana miaka 53 ndio maana tumeamua kumweka kwenye ulinzi huo sawa na binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo llani ya Chama cha Mapinduzi inasema Wazee wote sasa hivi tunawatambua ili kutengeneza sera nzuri ya kuweza kuwasaidia na kuwalipa pensheni. Kwa hiyo, watalipwa sambamba na faru huyu, Faru Fausta ambaye ndiyo sera inavyosema ya Chama cha Mapinduzi, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Dkt.Ndugulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii naomba niongeze maelezo kidogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2017 Serikali inatambua mchango na kuthamini mchango wa wazee na tumeweka utaratibu wazee wote ambao wako zaidi ya miaka 60 watapata matibabu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka mkakati sasa hivi kuhakikisha kwamba wazee wanatambuliwa na kupewa vitambulisho vya kupewa matibabu na tumeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba, katika vituo vyetu vyote vya kutolea huduma za afya wazee wanapewa kipaumbele cha kwanza. *(Makofi)*

Kwa hiyo pamoja na majibu yote ambayo ametoa Naibu Waziri mchango huu ambao unapatikana katika mapato ya utalii katika sekta hii ya utalii ndio haya yanayoingia kwenye Mfuko Mkuu wa Taifa na kwenda kuwahudumia wazee hawa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa Mbunge wa Lupa linaelekeza kwa Waziri wa Kilimo.

Na. 77

Kurekebisha Sheria ya Tumbaku

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni muswada wa kurekebisha Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2004 ambayo imepitwa na wakati?

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Omary Mgumba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Jimbo la Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la tumbaku hapa nchini husimamiwa na Sheria ya Tumbaku Na. 24 ya mwaka 2001, Sura ya 202 ya Sheria za Tanzania (Tangazo la Serikali Na. 296 la mwaka 2000) pamoja na Kanuni za Sheria ya Tumbaku za mwaka 2012 (Tangazo la Serikali Na. 392 la mwaka 2012). Kabla ya Sheria ya mwaka 2001 zao la Tumbaku lilikuwa likisimamiwa na Sheria ya Bodi ya Tumbaku ya mwaka 1984 yaani *The Tobacco Processing Marketing Board*, pamoja na kanuni zake za mwaka 1997 ambazo zilifutwa kwa Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2001 na kanuni zake za mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya urazinishaji wa bodi za mazao, Sheria ya Sekta ya Tumbaku ilifanyiwa marekebisho na Bunge mwaka 2009 kupitia Sheria Na. 20 ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mazao ya mwaka 2009. Pamoja na mambo mengine, Sheria ya Tumbaku iliweka majukumu ya pamoja, majukumu ya usimamizi, ugharamiaji wa majukumu pamoa na mkutano wa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sheria na kanuni hizo zinaweka masharti ya msingi kwa ajili ya kuzingatiwa na

mkulima, mnunuzi na msindikaji wa tumbaku ili kuhakikisha kuwa tumbaku inayozalishwa na kusindikwa hapa nchini inakidhi ubora unaokubalika kimataifa na hivyo kuwezesha kupata soko la uhakika pamoja na kumlinda mlaji au mtumiaji wa bidhaa ya tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Wizara inatarajiwa kufanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali za mazao ikiwemo Sheria ya Tasnia ya Tumbaku. Kwa sasa Wizara inaendelea kupitia sheria zinazosimamia sekta ya kilimo ili kuimarisha na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mazao mbalimbali hususani mazao ya biashara.

Kuhusu Sheria ya Tumbaku Wizara kwa kushirikianna wadau inaendelea kupitia na kuainisha changamoto zilizopo katika sheria hiyo na baada ya zoezi hilo kukamilika, marekebisho ya sheria hii yatawasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, sheria hiyo haijapitwa na wakati, bali marekebisho yanayokusudiwa kufanyika ni kwa ajili ya kuboresha sheria hiyo ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa zao la tumbaku.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwambalaswa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Serikali imekiri kabisa katika majibu haya kwamba sheria iliyopo sasa hivi ni ya mwaka 2001 na kanuni za mwaka 2012. Ni ya zamani kweli kweli, lakini vilevile mwaka 2006 Serikali ilisaini Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku na mwaka 2008 Bunge lako liliridhia mkataba huo. Sasa hivi ni ziadi ya miaka 10, mkataba huo bado haujawa *domesticated* ndio maana nasema sheria hii haijaletwa hapa Bungeni ili iweze kurekebishwa.

Je, majibu haya ya Serikali ni kweli mwaka huu wataleta sheria hiyo Bungeni hapa sio kuniridhisha mimi? La kwanza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwa bahati mbaya sana zao la tumbaku uzalishaji wake unashuka kila mwaka badala ya kupanda bahati mbaya sana na mwaka huu imekuwa mbaya zaidi kwamba hivi ninavyoonge viko vyama vya msingi vya wakulima ambavyo havijapata makisio. Kwa hiyo hawajui kwamba mwaka huu watalima tumbaku au hawatalima na mwezi huu wa tisa ni wa mwisho wa matayarisho.Kwa mfano, Jimboni kwangu kuna Chama cha Msingi cha Upendo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali, Mheshimiwa uliza swali sasa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: ... na Kikola. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu jambo hili?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Omary Mgumba kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na namshukuru Mheshimiwa Mwambalaswa kwa swali nzuri. Ni kweli kama Serikali tuliridhia mkataba huo tamko hilo kwa ajili ya kupunguza matumizi ya tumbaku duniani ikiwemo Tanzania na ni kweli kwamba Serikali kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba tuko kwenye mchakato wa kufanya marekebisho mbalimbali na tumedhamiria mchakato huu ukikamilika tutaileta haraka iwezekanavyo katika Bunge lako hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwamba ni kweli matumizi ya tumbaku au mahitaji ya tumbaku kila mwaka yanaendelea kupungua kutokana na hili hili azimio ambalo tulilisaini na nchi nyingi ambao wamelisaini pia. Kwa hiyo, zao la tumbaku lina masharti mengi sana sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka jana tulitakiwa kwamba Tanzania kuzalisha tani 72,000 lakini

mwaka huu ni tani 55,000 tu kwa sababu tumepata masharti mapya, sasa hivi uzalishaji wa tumbaku kwamba sharti mojawapo kwamba yale mabani yatumie muda miti iliyopandwa na mzalishaji mwenyewe. Na wameshatoa *notice* ikifika mwaka 2020 kama bado tumbaku yetu tunakausha kwa kutumia miti ya asili maana yake tunaharibu mazingira hawatanunua tumbaku yetu hata kilo moja.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa wakulima wote tuzingatie sheria hii kwa sababu tumesharidhia, tuanze kupanda miti yetu ya kisasa kwa ajili ya kufanya ukaushaji wa tumbaku hiyo, la sivyo, soko hilo tutakuwa tumelipoteza kabisa na kilimo hichi kitakuwa kimekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ni vizuri tukafanya *diversification of crops* yaani tukaangalia na mazao mengine kulima. Kwa sababu zao hili kila siku linaendelea kupigwa vita na wahitaji wenyewe, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Na. 78

Wananchi Wanaonufaika na Mikopo ya Kilimo Zanzibar

MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA aliuliza:-

Zipo benki zinazotoa mikopo ya kilimo hususan Benki ya Kilimo Tanzania:-

Je, kwa upande wa Zanzibar ni wananchi wangapi wanaofaidika na mikopo ya kilimo?

MWENYEKITI: Ahsante majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya wananchi walionufaika na mikopo inayotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kwa wananchi wa Zanzibar hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2018 ni 3,000. Kati ya hao wanaume ni 1,800, wanawake 900 na vijana wa kike na kiume ni 300. Aidha, jumla ya mikopo iliyotolewa kwa idadi hiyo ya wananchi wa Zanzibar hadi kufikia tarehe 31Julai, 2018 ni shilingi bilioni 6.50.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma.

MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali inatumia vigezo gani kwa wananchi kupata hiyo mikopo?

Swali la pili, atakubaliana na mimi Mheshimiwa Naibu Waziri akiongozana na watalaam wake waende Jimboni kwangu kwenda kutoa elimu na kwa sababu wananchi wanataka kukopa fedha hizi ili wananchi na wao waondokane na umaskini. Je, Serikali lini watakwenda Jimboni kwangu Bububu ili kwenda kutoa mikopo? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa kifupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lako la kwanza kuhusu vigezo, kigezo kikubwa ambacho benki yetu ya kilimo inaangalia ili iweze kumkopesha mkulima ni kuangalia kama mradi ule unaotekelezwa na mkulima unaweza kukopesheka yaani *valuable agricultural activity* ambayo inaweza akawekeza na akapata faida yake na akaweza kurejesha mkopo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakatika hili ndio maana Benki Kuu imetoa maelekezo kwa mabenki yetu yote kuhakikisha kwamba wakopeshwaji ambao wanaomba mikopo wanakuwa ni wale ambao taarifa zao zinaonesha wameweza kukopa na wakarejesha mikopo ili kuondokana na tatizo la mikopo chechefu ambayo mabenki yetu mengi yanapambana nayo. Serikali yetu ya Awamu ya Tano imepanga kuhakikisha wakulima wetu wanafikiwa na mikopo hii ya benki ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, namuahidi Mheshimiwa Mwantakaje baada ya Bunge hili mimi na watalaam wangu wa Benki yetu ya Kilimo tutakuja Jimboni kwako Bububu kuja kuwatembelea wakulima wa Bububu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea muda sio rafiki, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 79

Elimu ya Msingi Nchini

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Kumekuwepo na mkanganyiko wa elimu ya msingi nchini ambapo kuna sera inasema Elimu ya Msingi ni kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba na nyingine inasema elimu ya msingi ya Mtanzania ni kuanzia darasa la kwanza mpaka la kumi na mbili.

Je, Serikali inasema nini juu ya suala hilo?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hili, kwa niaba Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, *Engineer* Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu Tanzania ni utaratibu uliowekwa ili kufikia malengo na dira ya elimu katika maeneo husika. Mfumo unajumuisha elimu ya awali ambayo ni miaka miwili, elimu ya msingi miaka saba, elimu ya sekondari miaka minne na elimu ya juu miaka miwili na miaka mitatu au zaidi elimu pia ya ya juu. Aidha, kwa sasa mfumo wa elimu wa Tanzania unasimamiwa kwa Sheria Na. 25 ya mwaka 1978 Sura Namba 353. Sheria hii inabainisha wazi kuwa elimu ya msingi ni kuanzia darasa la awali hadi darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusisitiza kuwa kwa sasa Serikali inaendelea kutekeleza na kusimamia elimu kwa kutumia sheria hiyo ambapo elimu ya msingi ni kuanzia darasa la awali hadi darasa la saba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Taska Mbogo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa wapo watoto ambao wanamaliza elimu ya msingi hawajui kuandika wala kusoma. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kila mtoto wa Tanzania anapomaliza elimu ya msingi ambayo ni darasa la saba anajua kusoma na kuandika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa wapo watu wazima wenye umri na wazee labda umri kama wangu

pia hawajui kusoma kutokana na mazingira labda waliyokuwa labda maeneo yao yalikuwa hayana shule. Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha elimu ya watu wazima iliyokuwepo hapo zamani miaka 1973 ili watu hawa waweze kusoma na kuandika?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa niaba kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbogo kwa maswali yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize tu kwamba Serikali imeendelea kutoa hamasa na kuwafuatilia walimu, lakini vilevile kuhakikisha kuwa watoto waweze kusoma na kuandika pale wanapokuwa hasa elimu ya msingi na hivyo kwa sasa mtoto inapofikia darasa la tatu ikigundulika hajui kusoma na kuandika imekuwa akipewa mpango maalum wa kumsaidia na kumuwezesha kuweza kumudu masomo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu ya watu wazima nikubaliane naye kwamba kweli Tanzania bado tunalo kundi kubwa takribani 20% ambao hawajui kusoma na kuandika. Kuna programu mbalimbali ambazo zimekuwa zikiendelea kupitia elimu ya watu wazima ambapo wanapewa baadhi ya mafunzo ya kujitegemea, lakini vilevile nipende kusisitiza kwamba kila Mtanzania ambaye hajui kusoma na kuandika awe na kiu ya kuweza kujifunza kusoma na kuandika kwa sababu sasa elimu imeshakuwa karibu kila mahali hasa katika maeneo yetu tunayoishi.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni linaulizwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 80

Vigezo Kupata Mikopo ya Elimu ya Juu

MHE. USSI SALUM PONDEZA aliuliza:-

(a) Je, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, ni vijana/ wanafunzi wangapi walikosa vigezo vya kupata mkopo wa elimu ya juu?

(b) Je, Serikali inatumia utaratibu gani kuwatambua wanafunzi wanaotoka katika familia maskini katika utaratibu wa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa niaba.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa masomo 2017/2018, jumla ya wanafunzi 46,131 waliomba mikopo. Maombi ya mkopo ya wanafunzi hawa yalichambuliwa ili kupima uhitaji wao kwa kuzingatia Sheria ya Bodi ya Mikopo Sura ya 178 na mwongozo wa utaoji wa mikopo kwa mwaka 2017/2018.

Baada ya uchambuzi wa maombi hayo kukamilika, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo iliwapangia mikopo wanafunzi 33,920 wa mwaka wa kwanza ambao maombi yao yalikidhi vigezo na sifa zilizoainishwa katika sheria na mwongozo uliotolewa 2017/2018. Waombaji wengine 12,211 hawakupangiwa mkopo kwa sababu hawakukidhi vigezo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu na sifa za utoaji mikopo ya elimu ya juu unaongozwa na sheria iliyoanzishwa na Bodi nya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura namba 178. Kwa mujibu wa sheria hii mikopo ya elimu ya juu inapaswa kutolewa kwa Watanzania wahitaji na wenye sifa yaani *need and eligible*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu namba 17 cha sheria ya Bodi ya Mikopo kimetaja sifa kuu kuwa ni Utanzania, aliyedahiliwa katika Taasisi ya Elimu ya Juu inayotambulika na Serikali, asiwe na vyanzo vingine vinavyogharamia masomo yake na kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo wawe wamefaulu mitihani yao kuwawezesha kuendelea na mwaka unaofuata

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sheria inaipa mamlaka Serikali kupitia Bodi ya Mikopo kuandaa utaratibu na mwongozo wa utoaji mikopo kwa wahitaji wenye sifa. Katika mwaka wa masomo 2017/2018, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo iliandaa mwongozo unaopatikana katika tovuti ya Bodi ya Mikopo *(www.heslb.go.tz).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo pia ulitoa kipaumbele kwa makundi maalum kama yatima, wenye ulemavu, au wenye wazazi wenye ulemavu na wale ambao masomo yao ya sekondari ya stashahada yalifadhiliwa na wafadhili mbalimbali.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Pondeza.

MHE. USSI SALUM PONDEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake marefu, hata hivyo, nataka nimuulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, nataka nimwambie elimu ya juu ni suala la Muungano na amejibu katika majibu yake ya msingi kwa wanafunzi ambao wameweza kupata kwa mwaka huu ni 33,920. Nataka nimuulize, je, kati ya hao Wazanzibari ni wangapi nataka nijue? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda niipongeze sana Serikali kwa kuweka vigezo vya kuwatambua zaidi yatima na watu wenye hali ngumu katika mikopo hii. Kuna taarifa ambazo zipo na ambazo zina ushahidi, wengi ambao wanaokosa basi ni hawa yatima na hawa wenye hali ngumu. Hii inapelekea kuomba kwetu sisi Wabunge ili tuweze kuwawezesha waweze kupata elimu hii ya juu. Je, Serikali inasemaje kuhusu hili? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili kwa kifupi tu sijui kama utakuwa na takwimu kwa swali la kwanza.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza sifa za upatikanaji wa mikopo hapo awali sifa kuu ni hizo ambazo niliziainisha na kwa kweli tumekuwa hatusemi zaidi kwamba nani Mzanzibari nani Mtanzania bara, na hiyo ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hata kwa hali iliyopo katika maisha yetu ya kawaida ni vigumu sana hata kuwatenganisha hawa wanafunzi kwa sababu unaweza kukuta kuna mwanafunzi wa Zanzibar yuko Tanzania Bara na anasoma na mwanafunzi wa Tanzania Bara anasoma Zanzibar. Kwa hiyo tunachoangalia zaidi ni vile vigezo na sifa zinazostahiki waweze kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika suala hili la hawa wenye uhitaji maalum kukosa mikopo, niseme tu kwamba Serikali imekuwa ikizingatia sana na kwa wale ambao wana mazingira hayo ninayoyasema ikithibitika watasaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano katika mwaka huu wa 2017/2018, jumla ya wanafunzi 7,073 waliopata mikopo kati yao 1,224 ni wale ambao wenye mzazi mmoja na 5,849 ni wale ambao pia walikuwa hawana wazazi, lakini wenye ulemavu ni 626 kwa hiyo kimsingi niseme tu kwamba Serikali imekuwa ikizingatia sana uhitaji. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 81

Kivuko cha MV Mafanikio

MHE. HAWA A. GHASIA aliuliza:-

Je, ni lini Kivuko cha *MV* Mafanikio kitalala upande wa Msangamkuu ili kuwezesha dharura zinazojitokeza za wagonjwa hasa akinamama wajawazito kuhudumiwa wakati wa usiku?

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. JOHN E. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahaman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kivuko cha *MV* Mafanikio ambacho hutoa huduma ya kuvusha magari na abiria kati ya Msangamkuu na Mtwara Mjini eneo la Msemo, wakati wa usiku kinaegeshwa kwenye boya lililopo upande wa Mtwara Mjini. Kivuko hiki huegeshwa upande wa Mtwara Mjini kutokana na eneo hilo kuwa na kina kirefu cha maji hivyo kufanya kivuko kuwa salama wakati wa kupwa kwa maji ya bahari *(low tide)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* imenunua boti ndogo iitwayo *MV* Kuchele yenye uwezo wa kubeba abiria nane ambayo inatumika kutoa huduma ya dharura kati ya Msangamkuu na Mtwara Mjini nyakati za usiku, ikiwemo huduma ya kuvusha akinamama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Boti hiyo kwa sasa huegeshwa upande wa Mtwara Mjini kwa sababu za kiusalama na endapo huduma ya dharura itahitajika upande wa Msangamkuu, mawasiliano hufanywa kwa njia ya simu ili boti hii iweze kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati wa Serikali ni kuweka miundombinu itakayowezesha boti hiyo kuegeshwa upande wa Msangamkuu wakati wa usiku ikiwemo nyumba ya kulala kwa ajili ya Nahodha wa boti hiyo .

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri na niipongeze Serikali kwa kununua boti ndogo ya *MV* Kuchele. Hata hivyo, *MV* Kuchele itatumika vizuri sana kama Serikali itajenga majengo katika pande zote mbili au itajenga upande wa Msangamkuu ili kuwezesha kuwa na mtu ambaye analala pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo sasa hivi kama kuna mgonjwa ni lazima ile simu ipigwe na Mganga wa kituo cha Msangamkuu na wakati mwingine mganga wa Msangamkuu anakuwa hayupo Msangamkuu hivyo kuleta changamoto kubwa sana kwa wagonjwa kuweza kuvushwa upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata huu upande wa pili hakuna nyumba ambayo kuna mtu analala pale, huyo ambaye anavusha kwenye hiyo boti analala nyumbani kwake na yeye kama binadamu huwa inachukua muda mrefu sana kuweza kutatua changamoto hiyo. Swali je, Serikali ni lini itajenga hiyo nyumba ya kuwezesha kulala mtu pale upande wa Msangamkuu ili dharura inavyojitokeza iweze kutatuliwa kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa nini upande huu wa Msangamkuu ambapo *MV* Kuchele na *MV* Mafanikio

zinalala kwa nini kusiwe na mtu analala pale ili simu inapopigwa aweze kuvuka kwa haraka na kuweza kutatua changamoto inayojitokeza?

MWENYEKITI: Ahsante majibu Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano *Eng*ineer Kamwele.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeingia Bungeni lakini wakati tunamaliza Bunge lililopita nilikuwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji leo hii ni Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake nimeendelea kumwomba anielekeze na kuniongoza nitende yaliyo mema yanayompendeza. Pili nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini, lakini tatu, nijibu sasa hoja za Mheshimiwa Mbunge*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kutokana na uzoefu alionao, aliyoyataja ndio ambayo sasa hivi tunayapanga, kwamba tuliona changamoto ya kivuko kilichokuwepo kwamba ni kikubwa na ule upande wa Msangamkuu wakati mwingine maji yanakuwa yapo chini sana, tukanunua kivuko kidogo ambacho kinabeba watu nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kivuko hiki usiku kina-*park* upande wa Mtwara Mjini, lakini ni kweli tunajipanga kujenga nyumba ili walinzi wakae upande wa pili kuweza kuondoa hili tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge analizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ndio nimeingia nitampa majibu Mheshimiwa Mbunge kabla hatujatoka katika hili Bunge kuangalia fedha ambazo tumetenga kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ili nyumba iwepo askari wakae pale na kuangalia jinsi gani kile kivuko sasa kitakaa ule upande wa pili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata bado tupo Wizara hiyo hiyo, linaulizwa na Mheshimiwa Martin Alexander Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini.

Na. 82

Barabara ya Mbinga hadi Mbambabay

MHE. MARTIN A. M. MSUHA aliuliza:-

Je, ujenzi wa barabara ya Mbinga hadi Mbambabay kwa kiwango cha lami unatarajiwa kukamilika lini?

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO – (MHE. JOHN E. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martin Alexander Msuha Mbunge wa Mbinga Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Mbinga Mbambabay yenye urefu wa kilometa 66 umeanza ambapo tarehe 3, Aprili, 2018 Wizara yangu kupitia Wakala wa barabara Tanzania *TANROADS* ilisaini mkataba wa ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii na kampuni ya China *Henan International Corporation group company limited (CHICO)* ya nchini China kwa gharama ya Sh,129,361,352,517.84 na muda wa ujenzi wa miezi 33 hadi tarehe 2 Januari, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ujenzi inasimamiwa na mwandishi mshauri *SMES International Limited* wa nchini Australia kwa gharama ya Dola za Kimarekani 1,818,649.42 na fedha za kitanzania Sh.7,179,356,000.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msuha.

MHE. MARTIN A. M. MSUHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri yenye kutia moyo

wananchi wa Mbinga na Nyasa nina maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga kwa kiwango cha lami barabara inayotoka Mbinga kwenda Litembo hospitali kupitia Kijiji cha Muyangayanga, Kindimba na Mahenge, je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali kupitia swali namba 438 lilojibiwa hapa Bungeni tarehe 27 Juni, 2016 ilisema kwamba taratibu za kumpata mwandisi mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa barabara inatoka Kitai hadi Lituhi ulikwishakamilika, je, barabara hii ya kutoka Kitai hadi Lituhi itajengwa lini kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Yote ni lini majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. JOHN E. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali tunaendelea kuratibu ahadi za viongozi ili kuhakikisha kwamba ahadi hizi zinatekelezwa. Yako maeneo ambayo kwa kiasi kikubwa ahadi zimeshatekelezwa na yako maeneo ambayo pia tunaanza kufanya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge na kwa vile amekuwa mfuatiliaji mzuri labda saa nyingine tuonane kwa sababu ninalo kabrasha ambalo linaonesha hatua mbalimbali ya hizi barabara ambazo zimeahidiwa na viongozi ili tuweze kuona lakini aweze kuwa na uhakika na hatimaye awaeleze wananchi wa eneo la Mbinga Vijijini juu ya hatua ambayo tumeshaifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kwamba amewahi kujibiwa hapo awali kwa ujenzi wa barabara hii ya Kitahi – Lituhi, nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge kwamba ziko barabara nyingi ambazo usanifu wake umekamilika, Serikali inajipanga kutafuta fedha ili kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo barabara hii ya Kitahi - Lituhi nimeipita kwa sababu najua pia tunajenga daraja kubwa katika Mto Luhuhu, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mbinga ni kwamba kwanza barabara hii tumeiboresha sana kuhakikisha inapitika na kwa umuhimu wa ujenzi wa hili daraja kubwa tunapitisha *material* mbalimbali katika eneo hili kuliko kuzunguka kupitia kule Madaba. Kwa hiyo, tunaendelea kuiangalia kwa makini barabara hii lakini wakati huo tunatafuta fedha ili kiweza kujenga barabara katika kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, barabara ya kutoka Isandula, Magu inayopita Bukwimba kuja Ngudu mpaka Gungumalwa ni ahadi ya siku nyingi kwamba itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Tungependa kujua sasa kwa sababu mwanzo tuliambiwa kwamba upembuzi yakinifu umeshakamilika, upembuzi wa kina umeshakamilika, wananchi wa Magu, Kwimba wanataka kujua sasa barabara hiyo itaanza kujengwa lini kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ni lini kama hamko tayari bado sema bado.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. JOHN E. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mara nyingi sana amekuwa akifuatilia barabara hii. Niseme tu kwa ufupi kabisa upembuzi wa kina unaendelea kukamilishwa, ni hivi tu jana Meneja wa *TANROAD,* Mkoa wa Mwanza amepokea *report* ya awali ya usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo tunafanya mapitio ili sasa tuweze kukamilisha zoezi hili. Zoezi hili likikamilika litatuwezesha kujua gharama za mradi ili sasa tuiweke kwenye bajeti na hatimaye tutafute fedha kwa ajili ya kuijenga barabara hii kutoka Isandula Magu kupitia Bukwimba kuja Hungumwalo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Serikali imeanza kujenga barabara ya Bariadi na barabara ya Magu Ndagalu tumejenga vipande viwili, hapa katikakati barabara ya Magu – Ndagalu - Bariadi ni lini itakamilishwa kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. JOHN E. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Bariadi, Magu tuna miradi mingi ambayo inaendelea kujengwa na Mheshimiwa Mbunge anatambua pia tunajenga daraja la Sukuma kwa nia ya kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu *network* ya barabara katika eneo hili ni kubwa, tuonane ili angalau nimpe hatua ambayo tumefikia, lakini ni dhamira ya Serikali kuhakikisha maeneo haya yanaunganishwa vizuri ili wananchi waweze kujiimarisha kuchumi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja. Kwa kuwa tayari Serikali imeshakubali kujenga barabara ya lami kutoka Mpwapwa kwenda Kongwa, ninachotaka Mheshimiwa Naibu Waziri awathibitishie wana

Mpwapwa ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa na kiasi gani kimetengwa kwa sababu ni muda mrefu, sasa ni mwezi wa Tisa?*(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO – (MHE. JOHN E. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi barabara hii ya kutoka Mpwapwa kuja Kongwa ni sehemu hii ya barabara ambayo inakuja mpaka eneo la Mbande na kwa kiasi kikubwa barabara hii inaendelea na ujenzi. Najua *concern* ya Mheshimiwa Mbunge ni ule ujenzi wa barabara hii sasa kuwa na kasi kubwa kutokea Mpwapwa kuja Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kiasi cha fedha ambacho kimetengwa, najua tumetenga fedha, tuwasiliane tu na Mheshimiwa Mbunge ili angalau basi tuone kwa undani kwamba ni kiasi gani kimetengwa. Nimhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mpwapwa eneo la Mpwapwa nimelitembelea tumejipanga ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Mpwapwa wanaunganika vizuri na Makao Makuu ya Nchi hapa Dodoma.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sijafurahi na matumizi ya muda wetu kwa leo na mnaelewa kwa nini, naendelea kuwaomba sana Waheshimiwa Mawaziri majibu yasiwe marefu leo angalieni majibu mliyopata marefu kwelikweli. Pia tatizo la kutouliza swali moja kwa moja bado ni shida, naelewa Kiswahili kina utamu wake, lakini ndani yake ndio kinatulia muda.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Harisson Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wakiongozwa na ndugu Michael Salali. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni kumi na wawili wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana na Ajira) ambao ni washindi wa maonesho ya ubunifu wa kisayansi katika Chuo Kikuu cha St. John's cha Jijini Dodoma, wakiongozwa na ndugu Sophia Yusuph Abeid aliyeshika nafasi ya kwanza kwa kugundua mfumo wa kutunza kumbukumbu za mafaili ya ofisi. Mko wapi? Hongereni sana, Sophia hongera sanasana endelea na kazi hiyo, ongeza jitihada zaidi, unaweza ukafanya makubwa zaidi ya hapo.

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga Mbunge Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ndugu Imani Benard Mwaipaja ambaye ni Mwalimu kutoka Jijini Dar es Salaam. Mwalimu mwaipaja karibu sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, ambao ni viongozi wa Chama cha Soka cha Mkoa wa Ruvuma Faru, sio Fausta Faru wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama hicho ndugu Golden Sanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Esther Matiko Mbunge ambao ni Watoto wake wawili ndugu Nicole Mukami na ndugu Nicolson Mukami pamoja na kaka zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Kemilembe Lwota, ambao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoani Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 108 wa Mheshimiwa Joshua Nasari na Mheshimiwa Zubeda Sakuru ambao ni wanafunzi wa awali na msingi kutoka Shule ya Msingi Tumaini *Mission* iliyopo Kata ya Imbaseni, Wilayani Arumeru, Mkoani Arusha wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo na Namnyaki Leningida, mko wapi? Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Pia wameambatana na Diwani wa Kata ya Imbaseni, Mheshimiwa Gadiel Mwamba. Karibu sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye ni mtoto wake kutoka Mkoani Morogoro ndugu Nazareth Mwampeta. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 44 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana wanamaombi. *(Makofi)*

Wageni 27 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba Mbunge ambao ni Kwaya ya Uinjilisti ya Kanisa la KKKT, Ipagala, hapa Jijini Dodoma. Karibuni sana Wanakwaya. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Rukia Kassim, ambao ni Watoto wake kutoka Zanzibar Ndugu Mohammed Seif Zahran, ndugu Ghazila Masoud na Ndugu Rehema Suleiman. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile kuna wageni 22 wa Mheshimiwa George Simbachawene, ambao ni wapiga Kura wake kutoka Kijiji cha Mtama Jimbo la Kibakwe wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Nicholaus Mkungie. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Bulaya ambao ni watoto wake kutoka Jimboni kwake Bunda Mkoani Mara ndugu Brighton Babile, Ndugu Ethan Mashili na dada yake Ndg Mwanjaa Bakari. *(Makofi)*

Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania *TWPG*, Mheshimiwa Susan Lyimo, anaomba niwatangazie Wabunge Wanawake, Wajumbe wa Chama hicho kuwa leo tarehe 11 Septemba, 2018, kutakuwa na Semina kwa ajili ya Wabunge Wanawake wote. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana. Wanawake tu basi na nyie wanaume mwende. *(Makofi)*

Tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa imani ya Kikristo, Mwenyekiti wa ibada Mheshimiwa Anna Lupembe, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, mnaombwa kuhudhuria ibada katika ukumbi wa Pius Msekwa *Chapel* wa pale juu ghorofa ya pili, leo Jumanne mara tu baada ya shughuli za Bunge kusitishwa mchana. Katika ibada hiyo kutakuwa na Kwaya ya Uinjilisti kutoka kanisa la KKKT Ipagala Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndio matangazo niliyokuwa nayo hapa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa kanuni ya 46(1). Ulinipatia kuuliza swali la nyongeza kuhusiana na Soko la Kimataifa la Lemagwi, majibu aliyoyatoa Naibu Waziri wa TAMISEMI ni majibu yasiyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Kimataifa la Lemagwi lilijengwa na sekta ya maendeleo ya kilimo, wakafikisha miundombinu yake ikabaki kidogo tu kumalizia. Ambapo walikabidhi Wizara ya Kilimo na ikasema wanaweza kulijenga likakamilika. Tangu mwaka 2015 alikuja Mkandarasi toka Arusha ili amalizie, baadaye Serikali wakashindwa kulipa fedha, akaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo lile soko limetelekezwa na ni soko lipo kimkakati, liko mpakani mwa Kenya na Tanzania. Sasa majibu aliyotoa Mheshimiwa Kandege kwamba halmashauri ndiyo iweze kuona kama kuna tija ipeleke barua ni kuonesha kwamba Serikali haiko makini kabisa kufatilia fedha ambazo zimeshawekeza za mabilioni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ni kwa nini sasa usielekeze Serikali, TAMISEMI na hiyo Wizara ya Kilimo wahakikishe kwamba wanakwenda kumalizia hilo

Soko la Kimatifa ili kuweza kuanza kutumika na kuweza kukuza uchumi wa Tarime na Tanzania kwa ujumla.

MWENYEKITI: Wamekusikia, wafuatilie tu itakaa vizuri, maana ni pesa za umma zilitumika haziwezi kupotea bure.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 (*The Public Private Partnership (Amendment) Bill,* 2018)

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt Mipango aweze kuwasilisha Muswada ulio mbele yetu. Karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(The Public Private Partnership Amendment Bill,* 2018*)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa Mara ya Pili na ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa shukurani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gorge Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. Aidha, katika kipindi chote cha majadiliano, Kamati ilitoa michango na changamoto nyingi kwa Serikali kuhusu ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Vilevile Muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya wadau mbalimbali kutoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Adeladus Kilangi pamoja na Wataalam wake wa Uandishi wa Sheria wakiongozwa na Bi. Sara Barahomoka kwa kuandaa vizuri Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho ya Sheria ya Ubia, baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, ili kuimarisha mfumo wa kitaasisi na kisheria katika usimamizi wa miradi ya ubia na pia kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa miradi ya *PPP* ili kurahisisha uibuaji, uidhinishaji na utekelezaji wa miradi ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Muswada unakusudia kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha, mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Sera sheria na kanuni za *PPP* Kufuatia mabadiliko ya mamlaka ya usimamizi wa *programme* ya *PPP*, kupitia Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri Namba 144 ya mwaka, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu ni kutatua changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa programme ya *PPP* nchini ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kutungwa kwa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi mwaka 2010, Serikali imefanikiwa kuwajengea uelewa wadau

mbalimbali kuhusu dhana ya ubia. Pia imefanikiwa kutekeleza miradi ya *PPP* ambayo imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa uendeshaji wa huduma ya usafiri Jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza, yaani *Dar Rapid Transit Project Phase one* ambao upo katika hatua ya uendeshaji chini ya kampuni binafsi ya *UDART* kama mtoa huduma wa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuna miradi ambayo ipo katika hatua za mwisho za upembuzi yakinifu ikiwa pamoja na mradi wa ujenzi na uzalishaji wa madawa muhimu na vifaa tiba utakaotekelezwa na Bohari Kuu ya Madawa na Mradi wa ujenzi wa uendeshaji wa vyuo kumi vya ufundi ya Nchini ya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna miradi ambayo iko katika hatua ya kuandaa taarifa ya awali yaani *pre-feasibility studies* ikiwa ni pamoja na mradi wa kusambaza gesi nchini unaoandaliwa na *TPDC;* Mradi wa kujenga *hostel* za wanafunzi unaoandaliwa na CBE; na mradi wa kujenga Taasisi ya Taifa ya *Cancer* unaotekelezwa na Taasisi ya Taifa ya *Cancer*. Miradi hii itakapokamilika itatekelezwa kwa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sheria ya *PPP* kuna changamoto mbalimbali zinazosababisha kuwepo na hitaji la marekebisho ya sheria hii ili kuleta tija na ufanisi katika kutekeleza na kusimamia miradi ya *PPP*. Baadhi ya changamoto nimeziorodhesha katika hotuba yangu aya ya saba, kwa sababu ya muda naomba nisizisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Muswada huu changamoto zilizobainishwa zitaondolewa na hivyo kuongeza ushirika wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa *PPP*

na hivyo kuleta ufanisi wa bajeti ya maendeleo ikiwemo kuongezeka kwa huduma za kiuchumi na kijamii zenye ubora na kuongezeka kwa kodi na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala muhimu katika Muswada; baadhi ya masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu pamoja na yafuatayo:-

(i) Waziri mwenye dhamana na *PPP* kuwa na Mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Sera na kanuni za sheria ya *PPP;*

(ii) Kamati ya Maamuzi *(Steering Committee)* ya ubia kuwa na jukumu la kuidhinisha miradi ya *PPP* pamoja na kusimamia na kuidhinisha matumizi ya Mfuko wa Uwezeshaji wa ubia;

(iii) Kuondoa Mamlaka ya Kamati ya Taifa ya Uwekezaji ya kuhakiki miradi iliyoidhinishwa kwa lengo la kupunguza mlolongo mrefu wa uidhinishaji;

(iv) Waziri mwenye dhamana na masuala ya *PPP* kuwa na Mamlaka ya kuwaelekeza Maafisa Masuuli wa Wizara au Taasisi kuidhinisha miradi midogo ya ubia yaani *Small Scale PPP Project;*

(v) Kumhusisha Mjumbe kutoka kwenye chombo chenye mamlaka na masuala ya Mpango wa Taifa, kuwa Mjumbe wa katika Kamati ya Maamuzi ya masuala ya *PPP*. Mabadiliko haya yanalenga kuendana na muundo wa Kamati ya Maamuzi ya masuala ya *PPP* kwa sasa;

(vi) Wizara au Taasisi za Serikali zinazotekeleza miradi ya *PPP* kuwa na wajibu wa kuwasilisha andiko la mradi

au taarifa ya upembuzi wa awali wa mradi badala ya utaratibu wa sasa wa kuzitaka kuwasilisha orodha ya mradi;

(vii) Wizara au Taasisi zinazotekeleza miradi ya *PPP* kuwa na jukumu la kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya *PPP*, taarifa za nusu mwaka za utekelezaji wa miradi kupitia kituo cha *PPP;*

(viii) Miradi ya *PPP* kujumuishwa katika mchakato wa bajeti;

(ix) *PPRA* kuwa na Mamlaka ya kuandaa miongozo ya kusimamia ununuzi wa Wataalam Waelekezi wa kuandaa maandiko ya miradi ya *PPP*, pamoja na wabia wa kutekeleza miradi kwa kushirikiana na kituo cha ubia;

(x) Ni kuweka vigezo vya kuruhusu baadhi ya miradi ya kipekee inayoibuliwa na sekta binafsi kutoshindanishwa; na

(xi) Ni kutofautisha utaratibu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli kushiriki katika ubia wa kumiliki hisa yaani *joint venture* na ubia chini ya Sheria ya *PPP* usiohusisha umiliki wa hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo ya marekebisho kupitia Muswada huu, masuala muhimu yanayohusiana na mapendekezo ya Muswada huu yatazingatiwa katika kanuni zitakazoandaliwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpangilio wa Muswada; Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza, inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili, yenye ibara ya pili (2) hadi ya 15 inahusu marekebisho ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya pili (2) ya Muswada kama ilivyorekebishwa katika jedwali la marekebisho, inapendekeza marekebisho ya kiujumla kwa kufuta maneno Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha, popote yatakaposomeka na badala yake yasomeke Wizara. Mapendekezo haya yanakusudia kuipa Wizara yenye dhamana na *PPP* Mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ibara hii inapendekeza kufuata maneno Kamati ya Kitaalamu ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi na badala yake yasomeke Kamati ya Kusimamia Miradi ya *PPP (Steering Committee)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya tatu (3) ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupita jedwali la marekebisho, inapendekeza kurekebisha kifungu cha tatu cha sheria ili kufuta tafsiri ya maneno Waziri na Wizara ambayo ilikuwa ikihusisha Wizara na Waziri mwenye dhamana na masula ya Uwekezaji na kuziandika upya na kufuta tafsiri ya maneno Kamati ya Taifa ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya kwanza ni kuweka tafsiri mpya ili tafsiri ya Waziri na Wizara ndani ya sheria ihusishe Wizara na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha na hivyo kuwezesha Masula ya *PPP* kusimamiwa na Wizara na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuindoa Kamati ya Taifa ya uwekezaji katika kuidhinisha miradi ya *PPP*. Kamati

hii inaondolewa kwa lengo la kupunguza mlolongo wa mamlaka za maamuzi katika usimamizi wa *programme* ya *PPP*. Aidha, kifungu hiki kinapendekeza kuongeza tafsiri mpya ya miradi midogo ya *PPP* ili kuwezesha utekelezaji wa sheria kuhusu miradi hiyo midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya nne (4) ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha nne, kwa lengo cha kukihamisha kituo cha ubia kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda kwenye Wizara ya dhamana na masuala ya PPP ili kwenda sambasamba na Hati ya Mgawanyo ya Majukumu ya Mawaziri Namba 144 ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili Kituo cha Ubia kitakachosimamiwa na Wizara inayohusika na masuala ya *PPP* kuwa na jukumu la kufanya mapitio ya miradi ya kipaumbele ambayo ipo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa na kuiwasilisha katika Kamati ya Kusimamia Miradi ya *PPP (Steering Committee).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya tano (5) ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kufanya marekebisho kifungu cha tano ili kwanza kukiwezesha Kituo cha Ubia kuwa na jukumu la kuwasilisha taarifa za upembuzi yakinifu, wazabuni watakaopendekezwa na mikataba ya miradi ya *PPP* kwenye Kamati ya Kusimamia Miradi ya *PPP* kwa ajili ya kuidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Uwekezaji kupewa jukumu la kuandaa program ya kuweka mazingira wezeshi katika uwekezaji kupitia utaratibu wa *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii inalenga kukabiliana na changamoto za kiutendaji katika utekelezaji wa miradi ya *PPP* ikiwemo mikakati ya kujenga uwezo wa

Sekta Binafsi nchini kushiriki katika kuwekeza kwenye miradi ya *PPP,* uimarishaji wa soko la hisa na mitaji pamoja na Sekta ya Fedha katika kutoa mikopo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya sita (6) ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7(1) cha sheria ili kuiwezesha mamlaka yenye dhamana na mipango kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kitaalam ya *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya saba (7) ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 7A katika vifungu vidogo vya (1) na (2) na kufuta kifungu kidogo cha (3) ili kwanza kuipa Kamati ya Kitaalam ya *PPP* mamlaka ya kuidhinisha taarifa ya upembuzi yakinifu wazabuni watakaopendekezwa na mikataba ya miradi ya *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuongeza muda wa kufanya uchambuzi wa nyaraka hizo kutoka siku 15 hadi siku 21 kwa kuzingatia uhalisia wa utendaji kazi, wigo wa miradi ya *PPP* na umakini mkubwa unaohitajika katika uchambuzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya nane (8) ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kukifuta kifungu cha 7B cha sheria na kukiandika upya ili kubainisha mamlaka ya Waziri katika kuidhinisha matumizi ya fedha pamoja na ushiriki wa Serikali kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi inayohitaji msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ibara hii inapendekeza kwamba idhini hiyo ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha itolewe ndani ya siku 21 kuanzia siku ya maombi hayo yanapowasilishwa kwake. Aidha, Ibara ndogo ya (5) na (6) ya Ibara 7B katika Muswada zinapendekezwa kuhamishiwa katika Ibara mpya ya 7C

ambayo inabainisha mamlaka na majukumu ya Waziri kama ifuatavyo:-

(i) Ni kusimamia vihatarishi vinavyohusiana na masuala ya kifedha katika mikataba ya utekelezaji wa miradi ya *PPP;*

(ii) Kuelekeza Afisa Masuuli anayehusika na mradi wa *PPP* kupitia na kuidhinisha miradi midogo ya *PPP;* na

(iii) Ni kutangaza kwenye vyombo vya habari miradi yote ya *PPP* iliyoidhinishwa chini ya sheria ya *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya nane (8) kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 8A kwa kukifanyia marekebisho kifungu cha 10 kwa kuongeza kifungu kidogo cha 4(a) ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya *PPP* kuandaa kanuni au kubainisha masuala ya ziada ya kuzingatiwa katika andiko na upembuzi yakinifu kwenye miradi ya *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya tisa (9) ya Muswada inapendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha 10A(2) ili kukiwezesha Kituo cha Ubia kufungua akaunti ya Mfuko wa Uwezeshaji wa Miradi ya *PPP* katika Benki Kuu ya Tanzania badala ya Benki ya Uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 10 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 15 ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha kuruhusu baadhi ya miradi ya kipekee inayoibuliwa na Sekta Binafsi kutoshindanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Muswada umebainisha vigezo vya kuzingatiwa katika miradi ambayo haitashindanishwa. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa Serikali kupata miradi yenye sifa inayoibuliwa na Sekta Binafsi lakini ambayo haihitaji mchango wowote wa

kifedha au dhamana kutoka Serikalini na ambayo ina tija na manufaa mapana kwa nchi. Vilevile kifungu hiki kinapendekeza masharti ya kuzingatiwa katika kuziwezesha kampuni za ndani za wazawa kushiriki katika mchakato wa ununuzi wa miradi ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, inapendekezwa kufuta kifungu cha 15(3) na kukiandika upya ili kuainisha kuwa baada ya andiko la awali la mradi unaowasilishwa na mbia wa Sekta Binafsi yaani *unsolicited proposal* kupitishwa na Serikali, mbia atatakiwa kuweka dhamana yaani *commitment deposit* ya kiasi kisichozidi asilimia tatu ya gharama za mradi ambacho kitarejeshwa kwa mwekezaji. Lengo la hatua hii ni kupata wawekezaji makini na miradi yenye tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 11 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kukifuta na kukiandika upya kifungu cha 20 cha sheria ili kubainisha kwamba mikataba ya *PPP* pamoja na marekebisho yake ni sharti yahakikiwe na Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya kukubaliwa na Kamati ya Maamuzi ya *PPP.* Vile vile inapendekezwa kurekebisha Ibara ya 11 ya Muswada kwa kuongeza Ibara ya 11A inayorekebisha kifungu cha 22 ili kuainisha kuwa migogoro ya miradi ya *PPP* itaamuliwa na vyombo vya kisheria vya Tanzania na kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 23A ili kubainisha jukumu la Afisa Masuuli wa Taasisi inayotekeleza miradi ya *PPP* kuwasilisha Kituo cha Ubia taarifa ya nusu mwaka ya utekelezaji. Aidha, kifungu hiki kinabainisha jukumu la Kituo cha Ubia kujumuisha taarifa hizo na kuziwasilisha kwa Waziri. Lengo la Ibara hii ni kuongeza uwajibikaji kwa taasisi zinazotekeleza miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho,

inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 25A na kukiandika upya kwa lengo la kukiboresha ili kuweka sharti kwa miradi ya *PPP* inayohusiana na umiliki wa maliasili na rasilimali za nchi kuzingatia sheria za *The National Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017* na *The Natural Wealth and Resources (Contract Review and Renegotiation) of Unconscionable Terms Act, 2017* ili kuepuka kuingia mikataba ambayo haina maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inarekebisha Ibara ya 27 ya Muswada kwa kuifuta na kuiandika upya ili kubainisha *fine* ya adhabu kwa makosa chini ya Sheria ya *PPP* kuwa isiyopungua Sh.5,000,000 na isiyozidi Sh.50,000,000 au kifungo kisichopungua kipindi cha miezi mitatu na kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 15 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 28 cha sheria ili kumpa Waziri mamlaka ya kuandaa kanuni zinazotoa mwongozo wa uwezeshaji wa wazawa kiuchumi katika miradi ya *PPP* ikiwemo ununuzi wa bidhaa na huduma za wajasiriamali wa Tanzania, kuwapa mafunzo na teknolojia na uwajibikaji wa makampuni kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya Muswada yenye Ibara ya 16 hadi 23 inahusu marekebisho ya sheria mbalimbali zitakazoathiriwa na marekebisho yanayopendekezwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 16 na 17 ya Muswada zinapendekeza kurekebisha Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38 ili kurekebisha kifungu cha 5(4)(c) cha sheria ili kuondoa mamlaka ya Kamati ya Taifa ya Uwekezaji ya Kuhakiki Miradi ya Ubia Iliyoidhinishwa. Lengo la marekebisho hayo ni kupunguza mamlaka ya maamuzi katika utekelezaji wa miradi ya *PPP.* Aidha, Kamati ya Taifa

ya Uwekezaji itabaki kuwa na jukumu la kutoa miongozo ya ujumla ya kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji wa miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 18 na 19 zinapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 ili kuipa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma *(PPRA)* jukumu la kuandaa miongozo ya kusimamia ununuzi wa wataalam elekezi na wabia wa kutekeleza miradi ya *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20 na 21 zinapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 ili kujumuisha miradi ya *PPP* katika Bajeti ya Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuzitaka Mamlaka za Serikali kuzingatia kikamilifu miradi ya *PPP* wakati wa maandalizi ya bajeti ya Serikali ili kuchochea kasi ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 22 na 23 zinapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Mafuta, Sura 392 kwa kufuta kipengele cha kwanza ili kutofautisha miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa *joint venture* na utaratibu wa *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; baada ya maelezo haya, naomba kuwasilisha ili Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada huu na hatimaye kukubali kuupitisha kuwa sheria itakayosimamia masuala ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunashukuru sana.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BILL SUPPLEMENT

No.5 ***8th June, 2018***

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.23. Vol.99 dated 8th June, 2018
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP (AMENDMENT) ACT, 2018

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.

PART II
GENERAL AMENDMENTS

2. General amendments.
3. Amendment of section 3.
4. Amendment of section 4.
5. Amendment of section 5.
6. Amendment of section 7.
7. Amendment of section 7A.
8. Repeal and replacement of section 7B.
9. Amendment of section 10A.
10. Amendment of section 15.
11. Amendment of section 20.
12. Addition of section 23A.
13. Addition of section 25A.
14. Amendment of section 27.
15. Amendment of section 28.

PART III
CONSEQUENTIAL AMENDMENTS

(a) Amendment of the Tanzania Investment Act, Cap. 38

16. Construction.

17. Amendment of section 2.
18. Amendment of section 5.

(b) Amendment of the Public Procurement Act, Cap. 410

19. Construction.
20. Amendment of section 9.

(c) Amendment of the Budget Act, Cap.439

21. Construction.
22. Amendment of section 7.

(d) Amendment of the Petroleum Act, Cap.392

23. Construction.
24. Amendment of section 9.

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
7 June, 2018

JOHN W. H. KIJAZI
Secretary to the Cabinet

A BILL
for

An Act to amend the Public Private Partnership Act.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title

Cap.103

1. This Act may be cited as the Public Private Partnership (Amendment) Act, 2018 and shall be read as one with the Public Private Partnership Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

PART II
GENERAL AMENDMENTS

General amendments

2. The principal Act is amended generally by deleting the phrase "Ministry responsible for finance" wherever it appears in the Act and substituting for it the word "Ministry".

Amendment of section 3

3. The principal Act is amended in section 3, by -

(a) deleting the definitions of the terms "Minister" and "Ministry" and substituting for them the following:

""Minister" means the Minister responsible for public private partnership;

"Ministry" means the Ministry responsible for public private partnership;";

(b) deleting the definition of the term "National Investment Steering Committee"; and

(c) adding in the appropriate alphabetical order the following new definitions:

"small scale PPP project" means a PPP project approved under this

Act on the basis of scope, type, value and other conditions as may be prescribed in the regulations;";

(d) by adding after the term "public private partnership" the words "or known in its acronym as "PPP"";.

Amendment of section 4

4. The principal Act is amended in section 4, by -

(a) deleting subsection (2) and substituting for it the following:

"(2) The PPP Centre shall be under the general supervision of the Ministry.";

(b) adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) There shall be such other number of departments as the Executive Director may, upon approval of the authority responsible for establishment in the public service, determine.";

(c) renumbering subsections (3) to (5) as subsections (4) to (6) respectively;

(d) in subsection (4) as renumbered by deleting the word "list" and substituting for it the words "concept note or prefeasibility study"

(e) in subsection (6) as renumbered by adding a proviso as follows:

"Provided that, the potential public private partnership project complies with the national development priorities."

(f) adding immediately after subsection (6) as renumbered the following:

"(7) The PPP Centre shall within twenty one working days analyse the potential public private partnership project received in terms of subsection (6).

(g) deleting subsection (7) as renumbered and substituting for it the following:

Cap.439

"(8) In this section, the term "budget cycle" shall have the meaning ascribed to it under the Budget Act."; and

(h) deleting the reference to subsection (7) appearing in subsection (6) as renumbered and substituting for it the reference to subsection (9).

Amendment of section 5

5. The principal Act is amended in section 5, -

(a) by deleting subsection (3);

(b) by deleting subsection (4) and substituting for it the following:

"(4) The PPP Centre shall, upon completion of analysis under subsection (2), submit the feasibility study, selection of preferred bidder and PPP agreements to the Public Private Partnership Technical Committee for approval.";

(c) renumbering subsections (4) to (6) as subsections (3) to (5) respectively.

(d) by adding immediately after subsection (5) as renumbered the following:

"(5) The Minister shall, for the purpose of ensuring investment in PPP projects and in consultation with the Minister responsible for investment, prepare programmes for development and maintenance of favourable environment for investment through public private partnership arrangement.".

Amendment of section 7

6. The principal Act is amended in section 7(1) by deleting paragraph (e) and substituting for it the following:

"(e) a representative of authority responsible for national planning;".

Amendment of section 7A

7. The principal Act is amended in section 7A-

(a) in subsection (1), by-

(i) deleting paragraph (c) and substituting for it the following:

"(c) consider and approve PPP projects, feasibility study, detailed project report and design, selection of preferred bidder, public private partnership agreement and any amendment to the agreement;".

(ii) deleting the words "or the Treasury" appearing in paragraph (d);

(iii) adding immediately after paragraph (e) the following:

"(g) oversee the management and operations of the PPP Centre."

(b) by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

"(2) Subject to the recommendation made by the PPP Centre, the Public Private Partnership Technical Committee shall, within twenty one working days, approve feasibility studies, detailed project report and design, selection of preferred bidder, agreements and amendment to agreements."

(c) by deleting subsection (3);

(d) by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) The Minister shall, for the purpose of this section, issue guidelines for-

(a) oversight by Public Private Partnership Technical Committee;

(b) contents of detailed project report and design to be submitted by private party."

Repeal and replacement of section 7B

8. The principal Act is amended by repealing section 7B and replacing it with the following:

"Powers of Minister

7B.-(1) Notwithstanding the provisions of section 7A, the Public Private Partnership Technical Committee shall, where a project requires public funding, any other government support or determination of matters of policy, refer the matter to the Minister for determination.

(2) The matter submitted to the Minister in terms of subsection (1) shall be processed and determined within twenty one working days from the date of submission.

(3) Where a project to be undertaken requires public financing, the Minister shall initiate funding process.

(4) The Minister shall, through the official *Gazette*, newspaper of wide circulation or public media, notify the general public of all approved projects under this Act.

(5) The Minister shall monitor and manage fiscal risks and other financial matters relating to the implementation of PPP projects in accordance with the respective agreement;

(6) The Minister may, by order published in the *Gazzette*, direct the accounting officer of a contracting authority to analyse and approve a small scale PPP Project in such manner and procedure as may be prescribed."

Amendment of section 10A

9. The principal Act is amended in section 10A(2) by deleting the words "an account with a reputable investment bank" appearing in subsection (2) and substituting for them the words "a bank account".

Amendment of section 15

10. The principal Act is amended in section 15, by -

(a) adding immediately after subsection (1) the following:

"(2) Notwithstanding subsection (1), the Minister may exempt procurement of an unsolicited project from competitive tendering where it meets the following criteria:

(a) the project shall be of priority to the Government at the particular time and broadly consistent with the government strategic objectives;
(b) the private proponent does not require Government guarantee or any form of financial support from the Government;
(c) the project shall have unique attributes that justify departing from a competitive tender process and that others could not deliver a similar project with the same value for money outcome;
(d) the project is of significant size, scope and financing as per conditions provided in the regulations;
(e) the project shall demonstrate value for money, affordability and shall transfer significant risks to the private proponent;
(f) the project has wide social economic benefits including improved services, employment and taxation; and
(g) the proponent commits to bear cost of undertaking a feasibility study.

(3) Upon approval of the project concept, the private proponent shall make a commitment to undertake the project by depositing an amount of money prescribed by the Minister in the regulations.".

(b) renumbering subsection (2) as subsection (4);
(c) adding immediately after subsection (4) as renumbered the following:

"Cap. 410

"(5) The regulations under this section, shall among other things, prescribe the following-

(a) inclusion of local firms and experts in consultancy contracts;
(b) use of local goods and experts in works and non-consultancy services;
(c) preference to local goods in process of evaluation;
(d) capacity building of local firms; and
(e) any other matter relating to empowerment of local company and Tanzanian citizens.

Amendment of section 20

11. The principal Act is amended in section 20, by adding immediately after the word "Committee" the words "and vetted by the Attorney General".

Addition of section 23A

12. The principal Act is amended by adding immediately after section 23 a new section 23A as follows:

"Periodic performance reports

23A.-(1) An accounting officer shall submit to the PPP Centre quarterly performance reports on the implementation of public private partnership projects in the manner prescribed in the Regulations.

(2) The PPP Centre shall consolidate quarterly performance reports of contracting authorities and submit the report to the Minister."

Addition of section 25A

13. The principal Act is amended by adding immediately after section 25 the following:

"Projects relating to natural wealth and resources Acts Nos 5 of 2017 6 of 2017

25A. The public private partnership project that relates to natural wealth and resources shall take into account the provisions of the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act and the Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act."

Amendment of section 27

14. The principal Act is amended in section 27, by-.

(a) deleting the words "five million" and substituting for them the words "fifty million, in addition to any illicit monies gained"; and
(b) adding immediately after the words "three years" appearing at the end of that section the words "or both.".

Amendment of section 28

15. The principal Act is amended in section 28-

(a) in subsection (2), by-
  (i) deleting paragraph (g) and substituting for it the following:
    "(g) the manner in which the empowerment of citizens of Tanzania may be implemented

including provision of goods and services by Tanzanian entrepreneurs, training and technology transfer, employment of Tanzanians and corporate social responsibility;

(h) process and procedure for scrutiny and analysis of projects that require provision of Government support;";

(ii) renaming paragraph (h) as paragraph (j).

(b) deleting the words "in consultation with the Co-ordination Unit" appearing in subsection (3).

PART III
CONSEQUENTIAL AMENDMENTS

(a) Amendment of the Tanzania Investment Act, Cap. 38

Construction Cap. 38

16. This Part shall be read as one with the Tanzania Investment Act hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 5

17. The principal Act is amended in section 5(4), by deleting-

(a) the word "including" appearing in paragraph (a) and substituting for it the word "and";

(b) the words "approved public private partnership projects and" appearing in paragraph (c).

(b) Amendment of the Public Procurement Act, Cap. 410

Construction Cap. 410

18. This Part shall be read as one with the Public Procurement Act hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 9

19. The principal Act is amended in section 9(1) by deleting paragraph (c) and substituting for it the following:

"(c) regulate procurement of consultancies, transaction advisors and private party in respect of public private partnership projects in accordance with the regulations made under the Public Private Partnership Act and guidelines issued by the Authority in collaboration with the PPP Centre."

(c) Amendment of the Budget Act, Cap.439

Construction Cap. 439

20. This Part shall be read as one with the Budget Act hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 7

21. The principal Act is amended in section 7(3) by deleting the words "public private partnership" appearing in the fourth line.

(d) Amendment of the Petroleum Act, Cap.392

Construction Cap.392

22. This Part shall be read as one with the Petroleum Act hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 9

23. The principal Act is amended in section 9(2) by deleting paragraph (i) and substituting for it the following:

"(i) participate in the-

(i) joint venture project for optimisation of shareholder value under strategic partnership arrangements; and

Cap. 103

project under public private partnership arrangements in accordance with the Public Private Partnership Act;".

OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes to amend the Public Private Partnership Act, Cap.103 to empower the Minister responsible for finance to manage the implementation of Public Private Partnership (PPP) Policy, Law and Regulation. It further aims at removing legal challenges under the Act for better implementation of Public Private Partnership Program.

The Bill is divided into Three Parts. Part I deals with Preliminary provisions which include the title of the Bill and the manner in which various provisions of the Act are proposed to be amended. Part II deals with general amendments and Part III deals with consequential amendments.

Section 2 is proposed to be amended by deleting the words "Minister responsible for finance" wherever they appear and substituting for them the word 'Ministry'. The amendment aims at empowering the Ministry responsible for PPP to manage the implementation of PPP Policy, Law and Regulations.

Section 3 is proposed to be amended by deleting the definitions of the terms "Minister" and "Ministry" and substituting for them new definitions, with the purpose of empowering the Minister responsible for PPP to oversee the implementation PPP program. The section is further proposed to be amended by deleting the definition of the term National Investment Steering Committee with the purpose of removing its mandate to approve PPP projects. The section further proposes to add the definition of the term "small scale PPP project" for better implementation of the Act.

Section 4 is proposed to be amended to transfer the PPP Centre from the Prime Minister's Office to the Ministry responsible for PPP in order to comply with the Ministers (Discharge of Ministerial Functions) Instrument, G.N. No. 144/2016 which empowers the Minister responsible for finance to oversee the management of PPP Policy, Law and Regulations. The section is further proposed to be amended to make provisions for determination of potential public private partnership project by the PPP Centre with the view to align the projects with national development plan.

Section 5 is proposed to be amended to give the PPP Technical Committee mandate to approve the feasibility study reports, selection of preferred bidders and PPP agreements.

Section 7 is proposed to be amended by deleting subsection (1)(e) so as to empower the authority responsible for National Planning to be a member of the PPP Technical Committee.

Section 7A is proposed to be amended in subsection (1) by adding functions of the Technical Committee's is power of approving feasibility study reports, selection of preferred bidders and PPP agreements. It is further proposed that the period of analysing those documents be extended from fifteen working days to twenty one working days due to scope and complexity of analysing PPP projects. The section is further proposed to be amended by adding new paragraph under subsection (1) so as to give the PPP Technical Committee mandate to oversee the PPP Centre and empowering the Minister to prepare oversight guidelines for PPP Technical Committee to oversee the PPP Centre.

Section 7B is proposed to be repeated and replaced so as to make provisions for powers of Minister in policy, fiscal risk and other financial matters relating PPP projects .

Section 10A (2) is proposed to be amended to require the PPP Centre to open a bank account for PPP Facilitation Fund with the Bank of Tanzania instead of opening it in a reputable investment bank.

Section 15 is proposed to be amended by adding a new subsection (3) so as to empower the Minister to exempt some unique projects proposed by the private sector from being subjected to the competitive tendering process subject to the fulfilment of conditions. The objective of the proposed amendment is to increase magnitude of unique projects proposed by private sector which have value for money to the Government including projects that do not require government guarantee or financial support from the Government. The section is further proposed to be amended by adding a new subsection (5) that makes provisions for consideration of local content matters to be considered in the procurement process.

Section 20 is proposed to be amended by transferring the mandate of reviewing and amending the PPP agreements from the PPP Technical Committee to the Minister and the Attorney General.

The Bill also proposes to add a new section 23A to require the accounting officers of the contracting authorities to submit quarterly performance reports to the PPP Centre. The section

further requires the PPP Centre to consolidate the quarterly performance reports submitted by the contracting authorities and submit them to the Minister. The proposed amendment aims at improving efficiency and accountability of the implementing agencies.

The new section 25A is proposed to be added for the purpose of making provisions for recognition and safeguarding of natural wealth and resources .

Section 27 is proposed to be amended by increasing the fine from Five Million to Fifty Million Tanzania Shillings and three years imprisonment or both. The objective of this amendment is to improve efficiency and accountability of public officers in enforcing PPP laws and Regulations.

Section 28(2) is amended by adding a new paragraph (g) with the view to empower the Minister to make Regulations detailing on the empowerment of citizens including provision of goods and services by Tanzania entrepreneurs, training and employment of Tanzania and corporate social responsibility. .

Section 5(4)(c) of Tanzania Investment Act, Cap 38 is proposed to be amended by relieving the National Investment Steering Committee of the mandate to scrutinize the approved PPP projects. The objective of the proposed amendment is to minimize the approval organs in the implementation of PPP projects.

Section 9(1)(c) of Public Procurement Act, Cap.410 is proposed to be amended to give Public Procurement Regulatory Authority the mandate to develop guidelines to regulate procurement of consultants, transaction advisors and private party in relation to PPP projects.

Section 7(3) of Budget Act, Cap.439 is proposed to be amended so as to include PPP projects in the Government budget. The objective of the proposed amendment is to require the contracting authorities to consider PPP projects during preparation of Government budget so as to enhance implementation of PPP projects.

Section 9(2) of Petroleum Act, Cap.392 is proposed to be amended for purposes of differentiating projects implemented through joint venture approach and projects implemented under PPP arrangement.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kurekebisha Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura ya 103 kwa ajili ya kuwezesha Waziri wa Fedha kusjimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za ubia. Mapendekezo ya marekebisho yanakusudia kuimarisha mfumo wa kitaasisi na kisheria katika usimamizi wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) na pia kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa miradi ya PPP. Aidha, Muswada unakusudia kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya PPP mamlaka ya kisheria

ya kuidhinisha miradi ya ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa miradi ya PPP.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali ya Sheria yanavyopendekezwa kurekebishwa. Sehemu ya Pili inahusu Marekebisho ya Jumla na Sehemu ya Tatu inahusu Marekebisho ya Sheria mbalimbali zitakazoathiriwa na marekebisho yanayopendekezwa.

Kifungu cha 2 kinakusudiwa kurekebishwa kwa kufuta maneno "Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha" popote yatakaposomeka na badala yake yasomeke "Wizara". Mapendekezo haya yanakusudia kuipa Wizara yenye dhamana na masuala ya PPP mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za PPP.

Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kufuta tafsiri ya maneno "Waziri" na "Wizara" na kuziandika upya; pia kufuta tafsiri ya neno "Kamati ya Taifa ya Uwekezaji". Lengo la marekebisho haya ni kubainisha mamlaka ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya PPP pamoja na kuindoa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji katika kuidhinisha miradi ya PPP. Kamati hii inaondolewa kwa lengo la kupunguza mlolongo wa mamlaka za maamuzi katika usimamizi wa Programu ya PPP. Kifungu kihi pia kinapendekeza kuongeza tafsiri ya miradi midogo ili kuweka maana kamili ya masharti ya sheria.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kukihamisha Kituo cha Ubia kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda Wizara yenye dhamana na masuala ya PPP kwenda sambamba na Hati ya Mgawanyo ya Majukumu ya Waziri Na. 144/2016. Aidha, kifungu hicho kinalenga pia kubainisha jukuma la kituo cha ubia kufanya mapitio ya miradi ambayo ipo kwenye mpango wa maendeleo.

Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha jukumu la Kamati ya Kitaalam ya PPP kuidhinisha Taarifa za Upembuzi Yakinifu,Wazabuni watakaopendekezwa na Mikataba ya miradi ya PPP.

Kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (1)(e) na kukiandika upya ili kuiwezesha mamlaka yenye dhamana na mipango kuwa mjumbe wa Kamati ya Kitaalam ya PPP.

Kifungu cha 7A kinapendekezwa kurekebishwa katika vifungu vidogo vya (1), (2) na (3) ili kuipa Kamati ya Kitaalam ya PPP jukumu la kuidhinisha taarifa za upembuzi yakinifu, wazabuni watakaopendekezwa na mikataba ya miradi ya PPP pamoja na kuongeza muda wa kufanya uchambuzi wa nyaraka hizo. Muda wa uchambuzi wa nyaraka husika kutoka siku kumi na tano hadi siku ishirini na moja kwa kuzingatia uhalisia wa utendaji kazi, wigo wa miradi ya PPP na umakini mkubwa unaohitajika katika uchambuzi wa miradi hiyo. Aidha, kifungu kinapendekeza kurekebisha ili kuibainisha jukumu la Kamati ya Kitaalam ya PPP la kuwa mwangalizi wa Kituo cha Ubia na kumpa Waziri jukumu la kuandaa Miongozo itakayotumiwa na Kamati katika uangalizi wa Kituo hicho.

Kifungu cha 7B kinapendekeza kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti ya kumpa Waziri mamlaka ya kusimamia sera pamoja na kushughulikia masuala yote yanayohusiana na fedha katika utekelezaji wa miradi ya PPP.

Kifungu cha 10A (2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kukiwezesha Kituo cha Ubia kufungua Akaunti ya Mfuko wa Uwezeshaji wa Miradi ya PPP katika Benki Kuu ya Tanzania badala ya Benki mahiri ya Uwekezaji.

Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) ili kuweka vigezo vya kuruhusu baadhi ya miradi ya kipekee inayoibuliwa na sekta binafsi kutokushindanishwa. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza fursa kwa Serikali kupata miradi inayoibuliwa na sekta binafsi ambayo ina sifa za kipekee ikiwa ni pamoja na kutohitaji msaada wa kifedha kutoka serikalini au dhamana ya Serikali, na ambayo ina tija na manufaa mapana kwa nchi. Kifungu hiki pia kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kidogo cha 5 kwa lengo la kubainisha ushiriki wa wazawa kuzigatiwa wakati wa mchakato wa ununuzi.

Kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya Kamati ya Wataalam ya PPP ya kupitia na kurekebisha Mikataba ya PPP na badala yake mamlaka hayo anapewa Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marekebisho ni sambamba na mabadiliko ya usimamizi wa Sera, Sheria na Kanuni za PPP yanayopendekezwa.

Muswada unapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 23A kwa lengo la kubainisha jukumu la Afisa Masuhuli wa taasisi inayotekeleza miradi ya PPP kuwasilisha kwenye Kituo cha Ubia, taarifa ya robo mwaka ya utekelezaji. Aidha, kifungu hiki kinabainisha jukumu la Kituo cha Ubia kujumuisha taarifa hizo na kuziwasilisha kwa Waziri. Lengo la kifungu hiki ni kuongeza uwajibikaji kwa taasisi zinazotekeleza miradi.

Kifungu kipya cha 25A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kutambua na kulinda rasilimali za nchi.

Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza adhabu ya faini kutoka shillingi milioni tano hadi shillingi milioni hamsini, na adhabu ya kifungo cha miaka mitatu au vyote kwa pamoja. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa watendaji kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria na Kanuni za PPP.

Kifungu cha 28(2) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza aya (g) kwa lengo la kumpa mamlaka Wazairi kutunga kanuni za kunufaika kwa wazawa katika shughuli za ya PPP ikiwemo utoaji wa huduma na bidhaa kwa wajasiliamali wa kitanzania, mafunzo na ajira kwa watanzania na uwajibikaji wa makampuni kwa jamii.

Kifungu cha 5(4)(c) cha Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya Kamati ya Taifa ya Uwekezaji ya kuhakiki miradi ya ubia iliyoidhinishwa. Lengo la marekebisho hayo ni kupunguza mamlaka za maamuzi katika utekelezaji wa miradi ya PPP.

Kifungu cha 9 (1)(c) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma jukumu la kuandaa Miongozo ya kusimamia ununuzi wa Wataalam Elekezi na Wabia wa kutekeleza miradi ya PPP.

Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha miradi ya PPP katika bajeti ya Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuzitaka mamlaka za serikali kuzingatia kikamilifu miradi ya PPP wakati wa maandalizi ya bajeti ya Serikali hivyo kuchochea kasi ya maendeleo nchini.

Kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Mafuta, Sura ya 392 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta kipengele cha (i) kwa lengo la kutofautisha miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa *Joint Venture* na utaratibu wa PPP.

Dodoma,
18 Mei, 2018

PHILIP I. MPANGO
Waziri wa Fedha na Mipango

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. PHILIP MPANGO, THE MINISTER FOR FINANCE AND PLANNING AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP (AMENDMENT) ACT 2018"

Made under S.O.86(10)

A Bill entitled "The Public Private Partnership (Amendment Act), 2018 is amended generally as follows:

A: By deleting Clause 2 and substituting for it the following:

"General amendment

2. The principal Act is amended generally by-

(a) deleting the words "Ministry responsible for finance" wherever it appears in the Act and substituting for it the word "Ministry"; and

(b) deleting the words "Public Private Partnership Technical Committee" wherever it appears in the Act and substituting for it the phrase "Public Private Partnership Steering Committee."

B: In Clause 3 by-

(a) deleting the definition of the term "small scale PPP project" appearing in paragraph (c) and substituting for it the following:

"small scale PPP project" means a PPP project approved under this Act of an amount not exceeding twenty million US dollars;" and

(b) deleting paragraph (d) and substituting for it the following:

"(d) in the definition of the term "Public Private Partnership" by inserting between the words "Public Private Partnership" and "means" the words "or known in its acronym as "PPP"".

C: By deleting Clause 4 and substituting for it the following:

"Amendment of section 4

4. The principal Act is amended in section 4-

(a) by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

"(2) The PPP Centre shall be under the general supervision of the Ministry.";

(b) by adding immediately after subsection (2) the following:

"(2A) There shall be such other number of departments as the Executive Director may, upon approval of the authority responsible for establishment in the public service, determine.";

(c) in subsection (6) by-

(i) deleting the word "list" and substituting for it the words "concept note or prefeasibility study"; and

(ii) adding at the end of subsection (6) the following proviso:

"Provided that, the potential public private partnership project complies with the national development priorities.";

(d) adding immediately after subsection (6) the following:

"(6A) The PPP Centre shall, within twenty one working days, analyse the potential public private partnership project received in term of subsection (6) and forward to the Public Private Partnership Steering Committee";

(e) in subsection (7) by deleting the word "list" and substituting for it the words "concept note or prefeasibility study"; and

(f) deleting subsection (8) and substituting for it the following:

"(8) In this section, the term "budget cycle" shall have the meaning ascribed to it under the Budget Act.".

Cap. 439

D: In Clause 5 by-

(a) introducing a new paragraph (a) as follows-

"(a) deleting the words "and forward to the Ministry responsible for finance" appearing in subsection (2)";

(b) renaming paragraphs (a) to (d) as paragraphs (b) to (e) respectively.

E: In Clause 7-

(a) in paragraph (a) by-

(i) deleting subparagraph (i) and substituting for it the following:

"(i) deleting paragraph (c) and substituting for it the following:

"(c) approve feasibility study, detailed project report and design, selection of preferred bidder, public private partnership agreement or any amendment to the agreement;""

(ii) deleting subparagraph (iii); and

(b) by deleting paragraph (d).

F: By deleting Clause 8 and substituting for it the following:

"Repeal and replacement of section 7B

8. The principal Act is amended by repealing section 7B and replacing for it the following:

"Public funding and other support of PPP project

7B.-(1) Notwithstanding the provisions of section 7A, the Public Private Steering Committee shall, where a project requires public funding, any other government support or determination of matters of policy, refer the matter to the Minister for determination.

(2) The Minister shall, within twenty one working days from the date of receipt of matters from the Public Private Partnership Steering Committee in terms of subsection (1)-

(a) in the case of matters requiring public funding, process the matter in the manner prescribed under the Government Loans, Guarantees and Grants Act;

Cap. 134

(b) in the case of matters requiring any government support or determination of matters of policy, make determination and direct the Public Private Partnership Steering Committee accordingly.

(3) Notwithstanding subsection (2), the Minister shall, where a matter has not been determined within twenty one working days, notify the Public Private Partnership Steering Committee with reasons thereof.

Powers of Minister generally

7C.-(1) The Minister shall, through the official *Gazette*, newspaper of wide circulation or public media, notify the general public of all approved projects under this Act.

(2) The Minister shall monitor and manage fiscal risks and other financial matters relating to the implementation of PPP projects in accordance with the respective agreement.

(3) Subject to the provisions of this Act, the Minister shall issue directives to accounting officers of contracting authorities on the analysis and approval or disapproval of small scale PPP projects.""

G: By adding after Clause 8 a new Clause 8A as follows:

"Amendment of section 10

8A. The principal Act is amended in section 10 by adding immediately after subsection (4) the following:

"(4A) Without prejudice to the provisions of subsection (2), the Minister may, by regulations, prescribe additional or detailed contents of a concept note and feasibility study as may be required under a PPP project.""

H: In paragraph (a) of Clause 10 by-

(a) deleting the words "competitive tendering" appearing in the opening phrase of the proposed subsection (2) and substituting for it the words "competitive bidding process";

(b) deleting the words "and that others could not deliver a similar project with the same value for money outcome" appearing in the proposed paragraph (c) of subsection (2);

(c) inserting the words "requires substantial" between the words "and" and "financing" appearing in the proposed paragraph (d) of subsection (2);

(d) deleting the proposed subsection (3) and substituting for it the following:

"(3) Upon approval of project concept for unsolicited proposals, the private proponent shall make a commitment to undertake the project by depositing a refundable amount of not exceeding three percent of the estimated cost of the project to be conducted."

(e) by adding immediately after the proposed subsection (3) the following:

"(3A) The Minister may make regulations prescribing procedure for refund of commitment deposits under subsection (3).

I: By deleting Clause 11 and substituting for it the following:

"Amendment of section 20

11. The principal Act is amended by deleting section 20 and substituting for it the following:

"Amendment of agreements

20. Subject to section 7B, an agreement may be reviewed and amended by parties if the review or amendment is consented to by the Public Private Partnership Steering Committee and vetted by the Attorney General.""

J: By adding immediately after Clause 11 the following:

"Repeal and replacement of section 22

11A. The principal Act is amended by repealing section 22 and replacing for it the following:

"Dispute resolutions

22. Any dispute arising during the course of the agreement shall-

(a) be resolved through negotiation; or

(b) in the case of mediation or arbitration, be adjudicated by judicial bodies or other organs established in the United Republic and in accordance with laws of Tanzania.""

K: In Clause 12 by deleting the words "quarterly performance reports" appearing in the proposed section 23A(1) and substituting for them the words "mid-year performance report".

L: By deleting Clause 14 and substituting for it the following:

"Amendment of section 27

14. The principal Act is amended in section 27 by deleting the words "not exceeding five million shillings or to imprisonment

for a term not exceeding three years" and substituting for it the phrase "not less than five million shillings and not exceeding fifty million shillings or to imprisonment for a term of not less than three months and not exceeding three years or both."

M: In Clause 15(a) by deleting sub paragraph (ii) and substituting for it the following:

"(ii) renaming paragraphs (h) and (i) as paragraphs (i) and (j) respectively."

N: In Clause 23 by deleting the proposed paragraph (i) and substituting for it the following:

"(i) participate in-

(i) joint venture projects for optimization of shareholder value under strategic partnership arrangement; or

(ii) projects under public private partnership arrangement in accordance with Public Private Partnership Act;".

Cap. 103

Dodoma, **PIM**

……, 2018 *MFP*

FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. PHILIP MPANGO, THE MINISTER FOR FINANCE AND PLANNING AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP (AMENDMENT) ACT, 2018"

(Made under S.O 88(6))

A Bill entitled "The Public Private Partnership (Amendment) Act, 2018 is further amended as follows:

A: In paragraph C: which amends Clause 4 by deleting paragraph (c) and substituting for it the following:

"(c) deleting subsection (6) and substituting for it the following:

"(6) Every contracting authority shall, at the beginning of every budget cycle, submit to the PPP Centre concept note and prefeasibility study of potential public private partnership projects:

Provided that-

(a) the potential public private partnership project complies with the national development priorities; and

(b) the concept note and prefeasibility study of potential public private partnership projects is approved by the respective Minister.""

B: In paragraph H: which amends Clause 10 by deleting the proposed subsection (3A) appearing in paragraph (e) and substituting for it the following:

"(3A) The Minister may make regulations prescribing procedure for deposit and refund of commitment deposits under subsection (3)."

Dodoma, **PIM**

……, 2018 *MFP*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti iliyopelekewa Muswada huu kuufanyia uchambuzi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Simbachawene. *(Makofi)*

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilifanya kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada husika, ambao unakusudia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura ya 103 wa Mwaka 2010 kama ulivyorekebishwa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu ni kuimarisha mfumo wa Kitaasisi na Kisheria katika usimamizi wa miradi ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Tarehe 26 na 30 Agosti, 2018, Kamati ilifanya mkutano na wadau mbalimbali ili kupokea maoni kuhusu Muswada huu kabla ya kuanza majadiliano na Serikali. Wadau walioshiriki walikuwa ni pamoja na *The Tanganyika Law Society*, *Stallion Attorneys*, *Confederation of Tanzania Industries (CTI)* pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania *(TPSF)* ambao walitoa maoni yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mojawapo ya kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara bila kutegemea Bajeti ya Serikali pekee. Njia hii ya uwekezaji inahamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma katika maeneo ambayo yana mvuto wa kibiashara ili fedha za Serikali zielekezwe katika maeneo ambayo hayavutii uwekezaji kwa Sekta Binafsi. Aidha, utekelezaji wa

miradi kwa njia ya ubia duniani umeonekana kuwa na manufaa makubwa hasa katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ambapo Sekta Binafsi ina mchango mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada. Muswada huu unalenga kuoanisha mabadiliko ya mgawanyo wa majukumu uliyosababisha kuhamishwa kwa majukumu ya kusimamia masuala ya uwekezaji kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na kuyahamishia Wizara ya Viwanda na Biashara. Hivyo, imelazimu kufanya mabadiliko katika sheria hii ili kuleta uwiano wa kiutendaji katika kuidhinisha utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu pia una lengo la kupunguza mlolongo wa uidhinishwaji wa miradi ya ubia. Kabla ya mabadiliko haya, miradi ya ubia ilitakiwa kupita katika mamlaka tano hadi kufikia hatua ya utekelezaji. Mradi ulitakiwa kuanzia Wizara, Idara, Wakala au Mamlaka za Serikali za Mitaa *(contracting authorities)* na baadaye kupelekwa kwenye Kituo cha Uwekezaji *(TIC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya hapo mradi ulitakiwa kwenda kituo cha *PPP* kilichokuwepo Ofisi ya Waziri Mkuu ambacho baada ya uchambuzi kilitakiwa kuwasilisha mradi huo katika kitengo *PPP-Unit* kilichokuwa Wizara ya Fedha na Mipango ili kuangalia masuala ya fedha *(financial viability)* na baadaye Kamati ya Uwekezaji ya Taifa *(National Investment Steering Committee - NISC)* ili kuidhinishwa. Utaratibu huu, ulikuwa ni mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umefupisha utaratibu huo ambapo hivi sasa mradi utapita katika hatua kuu nne za uidhinishaji hadi utekelezaji wake bila mgongano uliosababisha ucheleweshaji. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi utaandaliwa na Wizara, Idara, Wakala au Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(ii) Mradi utapelekwa katika Kituo cha Ubia *(PPP Centre)* kilichopo Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi;

(iii) Mradi kuwasilishwa kwa Kamati ya Uidhinishaji *(PPP Steering Committee);* na

(iv) Utapelekwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya uidhinishaji lakini atafanya hivyo baada ya kushauriana kwanza na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiambatanisho Na.1 kimeonesha kwa muhtasari utaratibu wa uidhinishwaji wa miradi ya ubia unaopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya pia yanalenga kuweka ukomo wa muda wa kila hatua ya uidhinishaji ili kupunguza ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, limewekwa sharti la kumtaka Waziri wa Fedha na Mipango kutoa sababu kwa Kamati ya Uidhinishaji wa Miradi *(PPP Steering Committee)* endapo siku 21 zilizowekwa kisheria zitakapomalizika. Sharti hili litasaidia kuondoa ucheleweshaji usiokuwa na tija katika uidhinishaji wa miradi ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi iliyoidhinishwa na Bunge mwaka 2010 pamoja na mabadiliko yake yaliyofanyika mwaka 2014 ilikuwa inataka miradi yote inayoibuliwa na sekta binafsi *(unsolicited projects*) kupitishwa katika hatua ya ushindani *(competitive tender bidding).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utaratibu huu pia sio tu kwamba ulikuwa unakatisha tamaa wabunifu wa miradi mbalimbali, lakini vilevile ulikuwa unaleta mkwamo katika utekelezaji wa miradi. Muswada huu umeweka vigezo pamoja na hatua mbalimbali ambazo endapo mradi

utakidhi masharti yaliyowekwa, Waziri mwenye dhamana ya *PPP* amepewa mamlaka ya kuondoa sharti la kushindanisha mradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu pia umelenga kuweka sharti kwa Wizara, Idara, Wakala au Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya ubia *(Compliance Report*) kila nusu ya mwaka. Mabadiliko haya yanaenda sambamba na mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine la msingi ambalo Muswada huu umekusudia kufanya mabadiliko ni kutoa maana ya miradi midogo ya ubia (*PPP small scale projects).* Katika sheria ya awali kiwango kilichokuwa kimebainishwa katika kanuni ni kuanzia dola za Marekani milioni 20 hadi 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Muswada huu kiwango hicho kimewekwa katika sheria na kitakuwa kiwango kisichozidi dola za Marekani milioni 20 ambayo ni sawa na takribani Shilingi za Kitanzania bilioni 46. Kiwango hiki kitatoa fursa kwa wawekezaji wa ndani kuweza kushiriki katika miradi ya ubia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 11 cha Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuongeza kifungu cha 11A. Kifungu hicho kina lengo la kuweka utaratibu wa kisheria wa usuluhishi na utatuzi wa migogoro inayotokana na miradi ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali, imekubalika kwamba utaratibu wa usuluhishi wa migogoro uwe na nyanja mbili: Kwanza njia ya makubaliano (*negotiation);* na pili endapo itaonekana kuna haja ya mgogoro kwenda kwenye mamlaka za usuluhishi au Mahakama, basi mamlaka za usuluhishi na Mahakama zitakazotumika ni zile zilizopo hapa nchini na kwa

kutumia Sheria za Tanzania. Lengo hasa la mabadiliko haya ni kuhakikisha maslahi ya Taifa yanalindwa wakati wa utatuzi wa migogoro na kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na Mapendekezo ya Kamati. Kamati imeridhika na inaunga mkono marekebisho yaliyofanywa na Serikali ambayo kimsingi yamejumuisha maoni na ushauri wa muda mrefu uliotolewa na Wabunge na wadau wa sekta binafsi. Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na baadaye kushauriana na Serikali kuhusu vifungu vyote vya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mashauriano ya kina na kupitia kifungu kwa kifungu cha Muswada huu, Kamati ilibaini umuhimu wa kufanya marekebisho kadhaa. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imezingatia kwa kiwango kikubwa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ambayo yatawasilishwa na Serikali kupitia Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha nia hii njema ya Serikali ya kuanza kutekeleza miradi ya ubia kwa ajili ya maendeleo ya Taifa, Kamati ina maoni yafuatayo ambayo endapo yatazingatiwa yatasaidia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya ubia:-

(i) Mazingira Bora ya Uwekezaji na Ufanyaji Biashara Nchini. Ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ni uwekezaji kama ulivyo uwekezaji mwingine. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Mwongozo *(Blue Print)* wa kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara utakaoongoza uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. Kamati inaishauri Serikali kutumia mwongozo huu ipasavyo ili kuhakikisha mabadiliko haya yanakuwa na tija.

(ii) Mfuko wa Uwezeshaji wa Miradi ya Ubia *(PPP Facilitation Fund).* Ili Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka ya

Serikali za Mitaa ziweze kuandaa miradi kwa kufanya utafiti wa awali, upembuzi yakinifu na kuandaa maandiko ya awali zinahitajika fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaishauri Serikali iwezeshe mfuko huu ili uweze kukidhi mahitaji ya msingi katika utekelezaji wa miradi ya ubia. Aidha, Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinashauriwa kutenga fedha katika bajeti zao ili kutekeleza hatua za awali za maandalizi ya miradi hii.

(iii) Uanzishwaji na Uendelezaji wa Benki za Uwekezaji na Rasilimali. Kwa uzoefu miradi ya ubia inachukua muda mrefu kurejesha fedha zilizowekezwa katika miradi, hali hii inasababisha ugumu kwa sekta binafsi kupata mikopo kutoka katika benki za biashara ambazo muda wake wa urejeshwaji mikopo ni mfupi. Hivyo, kuna haja ya Serikali kuona umuhimu wa kuweka mazingira wezeshi, ili kuongeza benki za uwekezaji nchini, ili kuchochea miradi ya ubia. Hali ilivyo sasa hapa nchini, ipo benki moja tu ya uwekezaji ya *TIB.*

(iv) Mafunzo Kuhusu Utekelezaji wa Miradi kwa Njia ya Ubia. Kamati imebaini kwamba kwanza, ili miradi ya ubia iweze kufanikiwa ni lazima kwanza kuwe na nia ya dhati ya kuingia ubia ili kuwezesha upatikanaji wa huduma; na pili, kuwepo na uelewa wa kutosha kuhusu uwekezaji kupitia njia ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba, ni muhimu Kituo cha Ubia *(PPP Centre)* kuwa na mpango mkakati wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ili waweze kujengewa uwezo na hatimaye kuweza kushiriki ipasavyo katika uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa miradi ya ubia.

(v) Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi Kupitia Sheria ya Ubia. Ibara ya 10 ya Muswada inalenga kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Ubia ili

kuweka masharti ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Hivi sasa kumekuwa na utaratibu wa kuweka maudhui ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwenye sheria mbalimbali, kama vile Sheria ya Madini Na.14 ya Mwaka 2010, Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura 410 ya Mwaka 2011 na Sheria ya Mafuta, Sura 392 ya Mwaka 2015.

Kamati inaishauri Serikali kwamba, kwa kuwa, ipo Sera na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni wakati sasa Serikali ikafanya mabadiliko katika Sera na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ili sera na sheria hiyo izingatie uwezeshaji wananchi kiuchumi katika miradi yote ya ubia. *(Makofi)*

(vi) Kuimarisha Soko la Dhamana na Mitaji. Imeonekana kwamba soko letu la mitaji na dhamana halijaweza kukidhi mahitaji ya mitaji nchini. Hii inasababisha kuwa na mwamko mdogo wa wananchi kushiriki katika soko hilo pamoja na uelewa duni.

Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuangalia taratibu nyingine zitakazoweza kusaidia upatikanaji wa mitaji kupitia masoko ya kimataifa ya uwekezaji. Njia mojawapo ya kufanikisha suala hili ni kutoa unafuu wa kodi kwa mitaji inayopatikana kutoka katika masoko mengine ya kimataifa.

(vii) Mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya *PPP* Kuwekwa katika Sheria Moja. Kamati imebaini kuwa mabadiliko yote yaliyofanyika katika Sheria ya *PPP* hayajajumuishwa katika sheria moja. ivyo basi, kwa kuwa, sheria hii inahusu uwekezaji na itatumiwa na watu mbalimbali wa ndani na nje ni vyema ikajumuishwa pamoja *(consolidated)* mabadiliko yote yaliyowahi kufanyika kwa nyakati tofauti ili yawe pamoja kwa ajili ya urahisi wa rejea.

(viii) Kuwajengea Uwezo Wataalam Watakaohusika katika Uandaaji wa Mikataba ya Ubia. Uwekezaji kwa njia ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta

binafsi bado ni tasnia changa nchini. Hivyo, kuna haja ya kuhakikisha kwamba, tunajenga uwezo wa wataalam watakaoshiriki katika mazungumzo na uandaaji wa mikataba, ili kuhakikisha Taifa linanufaika. Aidha, bado kuna haja ya kubadilishana uzoefu na nchi nyingine ambazo zimefanya vizuri katika uwekezaji kwa njia ya ubia. *(Makofi)*

(ix) Ushirikishwaji wa Waziri wa Sekta katika Mchakato wa Uidhinishwaji wa Miradi ya Ubia. Kamati inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4(5) cha Sheria, ili kuweka sharti kwa Wizara, Idara, Mamlaka za Serikali za Mitaa kumjulisha Waziri husika kuhusiana na orodha ya miradi ya ubia itakayopendekezwa kabla ya kuiwakilisha katika Kituo cha Ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa na kuniteuwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Pili, niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa kunichagua kwa kauli moja kuwa Mwenyekiti wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Kibakwe kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono katika kutekeleza shughuli za maendeleo katika Jimbo letu la Kibakwe. Hapa naomba nitambue uwepo wa wananchi wangu wa kutoka Jimbo la Kibakwe, wanaotoka Kijiji cha Mtamba katika Tarafa ya Rudi, ambao wamekuja kwa shughuli za kutembelea Bunge. Niwaombe tu tuendelee kupendana na kushirikiana kwa maendeleo ya jimbo letu, pamoja sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu. Marekebisho haya yamekuja wakati muafaka na utekelezaji wake utaenda sambamba na miongozo *(Blue Print)* iliyoandaliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Kamati pia, inawashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuweza kuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kwa ajili ya muda nisiwatambue kwa majina wajumbe wote, lakini kwenye *Hansard* watasomeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndugu Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Godfrey Godwin, Emmanuel Robi, Matamus Fungo, Lilian Masabala na Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba kuunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA UBIA BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI (THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP (AMENDMENT) BILL, 2018) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya **86(5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 napenda kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (The Public Private Partnership (Amendment) Bill) 2018.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilifanya kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada husika, ambao unakusudia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura ya 103 ya Mwaka 2010 kama ulivyorekebishwa Mwaka 2014. Lengo la Muswada huu ni kuimarisha mfumo wa Kitaasisi na Kisheria katika usimamizi wa miradi ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Tarehe 26 na 30 Agosti, 2018 Kamati ilifanya Mkutano na Wadau mbalimbali ili kupokea maoni kuhusu Muswada huu kabla ya kuanza majadiliano na Serikali. Wadau walioshiriki walikuwa ni pamoja na The Tanganyika Law Society (TLS), Stallion Attorneys, Confederation of Tanzania Industries (CTI) pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ambao walitoa maoni yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mojawapo ya kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara bila kutegemea Bajeti ya Serikali pekee. Njia hii ya uwekezaji inahamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma katika maeneo ambayo yana mvuto wa kibiashara ili fedha za Serikali zielekezwe katika maeneo ambayo hayavutii

uwekezaji kwa Sekta Binafsi. Aidha, utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia duniani umeonekana kuwa na manufaa makubwa hasa katika utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Taifa ambapo sekta binafsi ina mchango mkubwa.

1.1. Madhumuni ya Muswada

1.1.1. **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unalenga kuoanisha mabadiliko ya mgawanyo wa majukumu yaliyosababisha kuhamishwa kwa majukumu ya kusimamia masuala ya uwekezaji kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na kuyahamishia Wizara ya Viwanda na Biashara. Hivyo, imelazimu kufanya mabadiliko katika Sheria hii ili kuleta uwiano wa kiutendaji katika uidhinishaji na utekelezaji wa miradi kwa njia ya Ubia.

1.1.2. **Mheshimiwa Spika,** Muswada huu pia una lengo la kupunguza mlolongo wa uidhinishwaji wa Miradi ya Ubia. Kabla ya mabadiliko haya Miradi ya Ubia ilitakiwa kupita katika mamlaka tano hadi kufikia hatua ya utekelezaji. Mradi ulitakiwa kuanzishwa na Wizara, Idara, Wakala au Mamlaka za Serikali za Mitaa yaani (Contracting Authorities) na baadae kupelekwa Kituo cha Uwekezaji (TIC), baada ya hapo mradi ulitakiwa kwenda kituo cha PPP kilichokuwepo Ofisi ya Waziri Mkuu ambacho baada a uchambuzi kilitakiwa kuwasilisha mradi huo katika kitengo cha Ubia (PPP-Unit) kilichopo Wizara ya Fedha na Mipango ili kuangalia masuala ya fedha (Financial Viability) na baadae kamati ya Uwekezaji ya Taifa (National Investment Steering Committee - NISC) ili kuidhinishwa. Utaratibu huu, ulikuwa ni mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umefupisha utaratibu huo ambapo hivi sasa mradi utapita

katika hatua kuu nne za uidhinishaji hadi utekelezaji wake bila mgongano uliosababisha ucheleweshaji. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:

i. Mradi utaandaliwa na Wizara, Idara, Wakala au Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
ii. Mradi utapelekwa katika kituo cha Ubia (PPP Centre) kilichopo Wizara ya fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi;
iii. Mradi kuwasilishwa kwa Kamati ya uidhinishaji (PPP Steering Committee); na
iv. Waziri wa Fedha kuidhinisha mradi huo kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kiambatisho namba 1 Kimeonyesha kwa muhtasari utaratibu wa uidhinishwaji wa miradi ya ubia unaopendekezwa.

1.1.3. **Mheshimiwa Spika,** Mabadiliko haya pia yanalenga kuweka ukomo wa muda wa kila hatua ya uidhinishaji ili kupunguza ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, limewekwa sharti la kumtaka Waziri wa Fedha na Mipango kutoa sababu kwa Kamati ya uidhinishaji wa miradi (PPP Steering Committee) endapo siku 21 zilizowekwa kisheria zitakapomalizika. Sharti hili litasaidia kuondoa ucheleweshaji usiokuwa na tija katika uidhinishaji wa miradi ya ubia.

1.1.4. **Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi iliyoidhinishwa na Bunge mwaka 2010 pamoja na Mabadiliko ya mwaka 2014 ilikuwa inataka miradi yote inayoibuliwa na Sekta Binafsi (unsolicited projects) kupitishwa katika hatua ya ushindani yaani (competitive tender bidding). Utaratibu huu sio kwamba tu ulikuwa unakatisha tamaa

wabunifu wa miradi mbalimbali, lakini vilevile ulikuwa unaleta mkwamo katika utekelezaji wa miradi. Muswada huu umeweka vigezo pamoja na hatua mbalimbali ambazo endapo mradi utakidhi masharti yaliyowekwa, Waziri mwenye dhamana ya PPP amepewa mamlaka ya kuondoa sharti la kushindanisha mradi husika.

1.1.5. **Mheshimiwa Spika,** Muswada huu pia umelenga kuweka sharti kwa Wizara, Idara, Wakala au Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Ubia (Compliance Report) kila nusu mwaka. Mabadiliko haya yanaenda sambamba na mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015.

1.1.6. **Mheshimiwa Spika**, jambo jingine la msingi ambalo muswada huu umekusudia kufanya mabadiliko ni kutoa maana ya miradi midogo ya ubia "*PPP small scale projects".* Katika sheria ya awali kiwango kilichokuwa kimebainishwa katika kanuni ni kuanzia Dola za Marekani Milioni 20 hadi 75. Kwa muswada huu kiwango hicho kimewekwa katika Sheria na kitakuwa kiwango kisichozidi Dola za Marekani Milioni 20 ambayo ni sawa na takribani Shilingi za Kitanzania Bilioni 46 kwa kutumia kiwango cha kubadilisha fedha cha shillingi 2,286. Kiwango hiki kitatoa fursa kwa wawekezaji wa ndani kuweza kushiriki katika miradi ya ubia.

1.1.7. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 11 cha Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuongeza kifungu cha **11A**. Kifungu hicho kina lengo la kuweka utaratibu wa kisheria wa usuluhishi na utatuzi wa migogoro inayotokana na miradi ya ubia. Baada ya majadiliano ya kina kati ya Kamati

na Serikali, imekubalika kwamba utaratibu wa usuluhishi wa migogoro uwe na nyanja mbili; kwanza njia ya makubaliano yaani "*negotiation*" na pili endapo itaonekana kuna haja ya mgogoro kwenda kwenye Mamlaka za usuluhishi na Mahakama, basi Mamlaka za usuluhishi na Mahakama zitakazotumika ni zilizopo hapa nchini na kwa kutumia Sheria za Tanzania. Lengo hasa la mabadiliko haya ni kuhakikisha maslahi ya Taifa yanalindwa wakati wa utatuzi wa migogoro na kupunguza gharama.

2.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na inaunga mkono marekebisho yaliyofanywa na Serikali ambayo kimsingi yamejumuisha maoni na ushauri wa muda mrefu uliotolewa na Wabunge na wadau wa Sekta Binafsi. Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na baadaye kushauriana na Serikali kuhusu vifungu vyote vya muswada huu. Baada ya mashauriano ya kina na kupitia kifungu kwa kifungu cha Muswada huu Kamati ilibaini umuhimu wa kufanya marekebisho kadhaa. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imezingatia kwa kiwango kikubwa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ambayo yatawasilishwa na Serikali kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha nia hii njema ya Serikali ya kuanza kutekeleza miradi ya ubia kwa ajili ya maendeleo ya Taifa, Kamati ina maoni yafuatayo ambayo endapo yatazingatiwa yatasaidia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya ubia.

2.1. Mazingira bora ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini

Mheshimiwa Spika, ubia baina ya Sekta Umma na Sekta Binafsi ni uwekezaji kama ulivyo uwekezaji mwingine. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta

Muongozo (Blue Print) wa kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara utakayoongoza uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. Kamati inashauri Serikali kutumia Muongozo huo ipasavyo ili kuhakikisha mabadiliko haya yanakuwa na tija.

2.2. Mfuko wa Uwezeshaji wa Miradi ya Ubia (PPP Facilitation Fund)

Mheshimiwa Spika, ili Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kuandaa Miradi kwa kufanya utafiti wa awali, upembuzi yakinifu na kuandaa maandiko ya awali zinahitajika fedha. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuwezesha mfuko huu ili uweze kukidhi mahitaji ya msingi katika utekelezaji wa miradi ya ubia. Aidha, Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kutenga fedha katika Bajeti zao ili kutekeleza hatua za awali za maandalizi ya miradi ya ubia.

2.3. Uanzishwaji na uendelezaji wa Benki za Uwekezaji na Rasilimali.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu, miradi ya ubia inachukua muda mrefu kurejesha fedha zilizowekezwa katika miradi. Hali hii inasababisha ugumu kwa Sekta Binafsi kupata mikopo kutoka katika Benki za Biashara ambazo muda wake wa urejeshaji mikopo ni mfupi. Hivyo, kuna haja ya Serikali kuona umuhimu wa kuweka mazingira wezeshi ili kuongeza Benki za uwekezaji nchini ili kuchochea miradi ya ubia. Hali ilivyo hivi sasa, nchini ipo benki moja tu ya uwekezaji ya TIB.

2.4. Mafunzo kuhusu utekelezaji wa Miradi kwa njia ya Ubia

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba ili miradi ya ubia iweze kufanikiwa ni lazima kwanza,

kuwe na nia ya dhati ya kuingia ubia ili kuwezesha upatikanaji wa huduma, na pili, kuwepo na uelewa wa kutosha kuhusu uwekezaji kupitia njia ya ubia. Kamati inashauri kwamba ni muhimu kituo cha Ubia (PPP Centre) kuwa na mpango mkakati wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili waweze kujengewa uwezo na hatimaye kuweza kushiriki ipasavyo katika uandaaji, usimamizi na utelekelezaji wa miradi ya ubia.

2.5. Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kupitia Sheria ya Ubia

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 ya muswada inalenga kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 15 (5) cha Sheria ya Ubia ili kuweka masharti ya **uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi**. Hivi sasa kumekuwa na utaratibu wa kuweka maudhui ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwenye Sheria mbalimbali kama vile Sheria ya Madini Na. 14 ya mwaka 2010, Sheria ya Manunuzi ya Umma Sura 410 ya mwaka 2011 na Sheria ya Mafuta Sura 392 ya mwaka 2015. Kamati inaishauri Serikali kwamba, kwa kuwa ipo Sera na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni wakati sasa Serikali ikafanya mabadiliko katika Sera na Sheria ya uwezeshaji Wananchi kiuchumi ili sera na Sheria hiyo izingatie uwezeshaji katika miradi ya ubia.

2.6. Kuimarisha Soko la Dhamana na Mitaji

Mheshimiwa Spika, imeonekana kwamba soko letu la mitaji na dhamana halijaweza kukidhi mahitaji ya mitaji nchini. Hii inasababishwa na muamko mdogo wa wananchi kushiriki katika soko hilo pamoja na uelewa duni. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia taratibu nyingine zitakazoweza kusaidia upatikanaji wa mitaji kupitia masoko ya kimataifa ya uwekezaji. Njia moja wapo ya kufanikisha suala hili ni kutoa unafuu wa kodi kwa mitaji inayopatikana kutoka katika masoko mengine ya kimataifa.

2.7. Mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya PPP kuwekwa katika sheria moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa mabadiliko yote yaliyofanyika katika Sheria ya PPP hayajajumuishwa katika sheria moja. Hivyo basi, kwa kuwa sheria hii inahusu uwekezaji na itatumiwa na watu mbalimbali wa ndani na nje ni vyema ikajumuishwa yaani "*consolidate*" mabadiliko yote yaliyowahi kufanyika kwa nyakati tofauti ili kuwa na rejea moja.

2.8. Kuwajengea uwezo Wataalamu watakaohusika katika uandaaji wa Mikataba ya Ubia

Mheshimiwa Spika, uwekezaji kwa njia ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi bado ni tasnia changa nchini. Hivyo, kuna haja ya kuhakikisha kwamba tunajenga uwezo wa wataalamu watakaoshiriki katika mazungumzo na uandaaji wa Mikataba ili kuhakikisha taifa linanufaika. Aidha, bado kuna haja ya kubadilishana uzoefu na nchi nyingine ambazo zinafanya vizuri katika uwekezaji kwa njia ya ubia.

2.9. Ushirikishwaji wa Waziri wa Sekta katika Mchakato wa Uidhinishwaji wa Miradi ya Ubia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4(5) cha Sheria, ili kuweka sharti kwa Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa kumjulisha Waziri husika kuhusiana na orodha ya Miradi ya Ubia inayopendekezwa kabla ya kuiwasilisha katika Kituo cha Ubia (PPP Centre).

3.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa kuwa Mjumbe kwenye Kamati ya Bajeti na pili niwashukuru wajumbe wa Kamati kwa kunichagua kwa kauli moja kuwa Mwenyekiti. Aidha, napenda

kuwashukuru Wananchi wote wa Jimbo la Kibakwe kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono katika kutekeleza shughuli za maendeleo katika Jimbo la Kibakwe; tuendelee kupendana na kushirikiana kwa maendeleo yetu, **PAMOJA SANA!**.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu, marekebisho haya yamekuja wakati muafaka na utekelezaji wake utaenda sambamba na Muongozo (Blue Print) uliyoandaliwa na Serikali. Vilevile, napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Kamati pia inawashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuweza kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
4. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb

9. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
13. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb
14. Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
15. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
16. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb
17. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
18. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
19. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
20. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
21. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
22. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
23. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb
24. Mhe. Shally J. Raymond, Mb
25. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndugu Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Matamus Fungo, Lilian Masababla na Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha.

George B. Simbachawene, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA BAJETI
11 Septemba, 2018

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwenyekiti kwa maelezo yako na Taarifa ya Kamati. Sasa namuita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Muswada huu, Mheshimiwa Halima Mdee. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya miaka mingi ya kuwa kifungoni, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kutoa Maoni ya Kambi Kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103 *(The Public Private Partnership Amendment Act, 2018). (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi. Kwa heshima kubwa naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kusimama upande wetu sisi Wabunge wa Upinzani tunaofanyiwa hila za kisiasa na Serikali hii kila kukicha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia, kuwashukuru wale wote ambao kwa njia moja ama nyingine wamefanikisha uandaaji wa taarifa hii, hasa wadau ambao wametumia muda wao kupitia Muswada huu na kutoa maoni yao ambayo yamekuwa na msaada sana katika kuchambua hali ya sekta binafsi hapa nchini na kutoa mwelekeo namna ya kujenga sekta binafsi iliyo imara kwa mustakabali mwema wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani katika hotuba zetu mbalimbali na Taarifa za Serikali yenyewe unaonesha kwamba, sekta binafsi nchini inaelekea kuporomoka. Hii ni kwa sababu Serikali imeacha kutekeleza mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ambao ndiyo dira inayotuongoza katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotakiwa kutekelezwa na Serikali kwa kipindi cha miaka mitano yaani 2016/2017 hadi 2020/2021na badala yake inatekeleza shughuli na miradi mingine ambayo haiko katika mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano imeelezwa kwamba, miradi yote ambayo ni ya kibiashara iachwe itekelezwe na sekta binafsi, isipokuwa kama kuna sababu ya lazima kufanya vinginevyo *(commercialy viable projects should be left to the private sector unless there is a strong justification for it to be done otherwise).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hiyo ambayo ni *commercialy viable* imeorodheshwa na gharama za utekelezaji wake, ambayo ni ujenzi wa *SGR,* ujenzi wa Kiwanda cha *Liquidfied Natural Gas (LNG),* Liganga Mchuchuma *Industrial Park,* Mtwara *Petrol Chemical Special Economic Zone* na Bagamoyo *Special Economic Zone. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mpango wa Maendeleo kueleza bayana kuwa miradi hiyo itekelezwe na sekta binafsi, kwa kiwango kikubwa Serikali imeweka pembeni mapendekezo hayo ya Mpango huo na kutekeleza miradi hiyo yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama Serikali ilileta Bungeni sababu za msingi na za lazima za kuinyima sekta binafsi fursa ya kutekeleza miradi hiyo na Bunge likatoa kibali kwa Serikali kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hiki cha Serikali kung'ang'ania kutekeleza miradi mikubwa ya kibiashara na kuiweka kando sekta binafsi, kinyume na maelekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo, kinatoa ushuhuda kwamba, Serikali hii haina nia ya dhati ya kutekeleza Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP).* Ukosefu wa nia hiyo umeendelea kuonekana hata katika vifungu vinavyopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Serikali hii ya Awamu ya Tano umeonesha dhahiri kwamba, sasa tunarudi kule tulikotoka kwenye ujamaa uliokomaa na ukomunisti, ambapo sekta binafsi haikuruhusiwa kabisa kushiriki katika ujenzi wa uchumi. Tunarudi kwenye enzi zile za Mwalimu Nyerere ambazo nyenzo kuu za uzalishaji zilikuwa zikimilikiwa na kuendeshwa na Serikali *(State Controled Economy),* hali iliyosababisha uchumi kudorora na kuporomoka na hali ya wananchi kuwa duni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama Serikali hii ya CCM imebadili Sera zake za Uchumi au laaa! Kwa kuwa, kinachofanyika sasa cha kuitenga sekta binafsi ni kinyume kabisa na kilichofanywa na Serikali za Awamu Tatu zilizopita ambapo tulishuhudia soko huria likipewa nafasi katika ujenzi wa uchumi na kusababisha kuanzishwa kwa Sera ya Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vinavyofanywa na Serikali hii vya kutaka kila kitu kifanywe na Serikali Kuu, si tu kwamba vinazidhalilisha Serikali za Awamu Tatu zilizopita ambazo zote zilikuwa ni za Chama cha Mapinduzi, bali pia vinaonesha udhaifu mkubwa wa kukosa misimamo ya kisera kwa Chama cha Mapinduzi kuhusu namna uchumi endelevu unavyotakiwa kukuzwa na kuendeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ujamaa kushindwa uchumi duniani unaendeshwa kwa nguvu za soko ambapo sekta binafsi ni mdau muhimu. Kulazimisha kutumia mbinu za kijamaa katika zama hizi kwa Serikali kutaka kukumbatia kila kitu ni kujitoa ufahamu na ni jambo ambalo haliwezekani. Kwa lugha ya kimombo wanasema, *trying to run the economy without the private sector is simply an utopian idea. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba, moja ya misingi mikuu ya kujenga uchumi imara ni kuruhusu ushindani wa soko huria, kuruhusu watu

na sekta binafsi kumiliki mali kunakoenda sambamba na kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha sekta binafsi kushamiri, hatimaye kuchangia katika maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa bahati mbaya sana Serikali ya Awamu ya Tano badala ya kuichukulia sekta binafsi kama mdau wa maendeleo inawachukulia kama washindani wa kibiashara, hali inayopelekea sekta hii kukumbwa na mkwamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki tumeshuhudia ongezeko kubwa sana la mikopo chechefu, halikadhalika tumeshuhudia biashara kufungwa kwa kiwango ambacho hakijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu. Huku wafanyabiashara wakilalamikia mfumo wa kodi ambao umekuwa si rafiki kwa wafanyabiashara, hali inayowapelekea watu kutafuta mbinu mbadala kukwepa kodi badala ya kuona fahari kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba marekebisho haya pamoja na mambo mengine angalau yatafungua mlango wa sekta binafsi kuwa chachu ya maendeleo katika nchi yetu. Hili litafanikiwa kama Serikali itaridhia maboresho ya vifungu kadhaa ambavyo kwa mtazamo wetu tunadhani vinaleta mkwamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya Muswada. *PPP* inasimamiwa na nani? Katika Ibara ya 2, Muswada umefanya marekebisho ya kiujumla ambayo yanaeleza ama yanaelekeza yafuatayo:-

"Deleting the words, 'Ministry responsible for finance' wherever it appears in the Act and substuting for it the word 'Ministry'."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Lugha ya Kiswahili, kifungu hiki kimefanya marekebisho ya kiujumla kwa kufuta

maneno, 'Wizara inayohusika na masuala ya fedha' popote pale inapotokea na kuweka neno 'Wizara'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 3 vilevile kimetoa tafsiri ya neno *Ministry* na neno *Minister,* kama ifuatavyo:-

"*Minister means, the Minister responsible for public private partnership and Ministry means, the Ministry responsible for public private partnership.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia vifungu vyote sijaona huyo Waziri mwenye hiyo dhamana ni nani. Ikumbukwe kwamba, sheria tunayoifanyia marekebisho sasa ya *PPP,* ilikuwa chini ya Waziri Mkuu. Bunge tutakuwa ni wa ajabu kama tutatunga sheria pasipokujua nani anayekwenda kuwa msimamizi mkuu wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tabia iliyozuka hivi sasa ya kuondoa madaraka kwa wanaowajibika moja kwa moja kwa Bunge na kuwapa watu wanaowajibika moja kwa moja kwa mamlaka za uteuzi wao. Mfano mzuri:-

(a) Baraza la Mawaziri halijatajwa mahali popote katika Sheria ya Madini, kama ilivyorekebishwa kipindi kile, badala yake wajibu wa kutoa leseni zote za uchimbaji madini umekabidhiwa kwa Tume ya Madini kwa usimamizi wa Waziri wa Madini, angalia Kifungu Kipya cha 19(f) cha Sheria ya Madini. *(Makofi)*

(b) Tume ya Madini ndio yenye uwezo wa kusimamisha au kufuta kabisa leseni yoyote ya madini. Angalia Kifungu Kipya cha 24(m) cha Sheria ya Madini. Itakuwa maajabu ya Tanzania kwa Tume iliyoteuliwa na Rais kufuta leseni iliyotolewa na Baraza la Mawaziri linaloongozwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatarajia kwamba miradi mingi ya *PPP* inaweza kufanyika katika Sekta ya Madini na Nishati na hivyo mbali na Sheria ya *PPP* ni lazima sheria na kanuni za sekta husika zipewe kipaumbele pia. Tukumbuke sheria hizi za rasilimali zetu kwa kiasi kikubwa zinaingiliana na sheria moja haiwezi kusimama yenyewe kama hii ya *PPP* bila kuangalia sheria mama kwenye mradi wa ubia husika kama kifungu cha13 cha Muswada kinachoongeza kifungu kipya cha 25A katika sheria mama kinavyoonyesha. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ingekuwa ni jambo la busara kuifanya Kamati ya Taifa ya uwekezaji kuwa taasisi imara kwani uchumi wa Tanzania unategemea sana ubia na sekta binafsi na fursa bado ni nyingi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 4 ya Muswada inayofanya marekebisho Kifungu cha 4(6), Serikali imefanya marekebisho kwa kuongeza *proviso* baada ya kifungu kidogo tajwa hapo juu kwa kuongeza maneno yafuatayo:-

"Provided that the potential public private partnership complies with the national development priorities."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mahali popote kwenye Muswada ambapo tafsiri ya maneno "*national development priorities"* imetolewa. Kwa kuwa Muswada uko kimya, ni muhimu kwa utekelezaji bora wa sheria, Serikali ikafanya rejea za *instruments* ambazo zinatoa mwongozo ama zinaweka mwongozo wa mipango ya Taifa ya muda mfupi, muda mrefu na wa kati. Ikiachwa hivi hivi, kila kiongozi mpya atakayekuja anaweza kuwa na vipaumbale vyake vipya, matokeo yake tukakuta kama Taifa tunapiga *mark time* kila siku. Sisi tunashauri isomeke:-

"*Provided that the potential public private partnership project complies with the national development priorities as stipulated in the national development plans." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7 cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 7A cha sheria mama

kwa kufuta kifungu cha 7A.1(c) na kukiandika upya na kufuta kifungu cha 7A.(2) na kukiandika upya, pia kufuta kifungu cha (3) na kuweka kifungu kipya, vifungu hivyo vilikuwa vinatoa muda wa siku 15 kwa Kamati ya Kitaalam ya *PPP* jukumu ya la kuidhinisha taarifa ya upembuzi yakinifu na kufanya uchambuzi wa nyaraka za miradi ya wazabuni watakaopendekezwa katika miradi ya *PPP*. Marekebisho ya kuongeza siku hadi 21 kwa kazi iliyokuwa inafanyika kwa siku 15 ni jambo la kujirudisha nyuma sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa ubia ni fursa na mbia makini jambo la kwanza kuliangalia ni muda. Kama tunatunga sheria za kuzidisha muda katika biashara maana yake tunajipotezea fursa sisi wenyewe. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa ni vema muda wa kuidhinisha kama ilivyotumika katika kifungu kipya cha (c), *"consider and approve"* na katika kifungu cha (2), *"approve feasibility studies"* kwa timu mahiri ya wataalam, kazi ya kuidhinisha nyaraka siyo ya kuongeza muda, badala yake ungepungua na kuwa siku 10 za kazi badala ya siku 21 kama zilivyopendekezwa kama dhamira yetu ni ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani kupendekeza siku kupunguzwa lakini bado tunapenda kufahamu endapo siku 21 zilizopangwa kuongezwa zisipofanyiwa kazi ni hatua zipi zitachukuliwa kwa mamlaka iliyoshindwa kuchambua nyaraka na kuzipitisha kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9 cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 10A cha sheria ili kukiwezesha kituo cha ubia kufungua akaunti ya mfuko wa uwekezaji wa *PPP* katika Benki Kuu ya Tanzania badala ya Benki Mahiri ya Uwekezaji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa ni benki ipi itumike katika mradi *PPP* inategemea makubaliano ya pamoja baina ya wabia. Sambamba na hilo, benki mahiri ya uwekezaji ambayo ninaamini ndiyo inayotoa mkopo kwa ajili ya mradi, ni ukweli kuwa ikishakuwa benki mahiri kwa uwekezaji inakuwa na wataalam mahiri wa kusimamia na kushauri utendeji wa jinsi mradi

utakavyoendeshwa ili kuhakikisha fedha zilizowekwa na benki husika zinarejeshwa na faida inapatikana. Hivyo basi, kitendo cha kuweka kwenye sheria kuwa akaunti ya mradi wa *PPP* ni lazima ifunguliwe Benki Kuu haikuzingatia kuwa miradi ya *PPP* ya aina nyingi kulingana na aina ya miradi yenyewe kama vile *Build Operate and Transfer (BOT), Design Build Operate (DBO), Management and Operating, Concessions* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu katika Bunge la Bajeti lililopita kupitia *Finance Bill* tulipitisha sheria ya kuwa na *Treasury Single Account (TSA).* Katika mantiki hii inawezekana kabisa fedha za wawekezaji vilevile zikatumbukizwa kwenye akaunti moja ambayo ni kapu moja la Serikali, ambayo katika taratibu za kiuwekezaji inaweza ikawa ni ngumu kidogo. Kwa hiyo, nahitaji Mheshimiwa Waziri akija atoe ufafanuzi wa kina vilevile kuhusiana na hii kutokana na sheria ambayo Bunge tulipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 10 cha Muswada kinachorekebisha kifungu cha 15 cha sheria mama kuhusu mamlaka ya Waziri katika kutoa msamaha wa kutohusisha ushindani kwenye zabuni ya miradi ya kipekee iliyoibuliwa na sekta binafsi, miradi hiyo imeitwa *unsolicited project*. Kifungu hicho kimetoa masharti mengi na magumu sana kuweza kutekelezwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa miradi hii ndiyo miradi ya ubunifu kutoka sekta binafsi, kwani ndiyo miradi inayoibuliwa na watu wanaoangalia mazingira halisi na kuona fursa, miradi ambayo siyo kila mtu anaweza kuibua. Hii ndiyo miradi inayotofautisha uwezo wa ujasiriamali katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wetu miradi hii ilitakiwa isiwekewe masharti kabisa. Jambo kubwa ni uhusika wa Serikali katika kuhakikisha inaratibu kwa haraka mahitaji ya kisera au kisheria ili miradi hiyo iweze kuanza kwa kuzingatia kwamba miradi mingi ya aina hii inakuwa tayari ina vyanzo vyake vya fedha na siyo vyanzo vya fedha vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kama tulivyosema awali kuwa ni njia mojawapo ya kuizika sekta binafsi kwani masharti hayo yaliyomo kwenye kifungu cha 10 cha Muswada, ni dhahiri kuwa miradi hii ya kipekee inayoibuliwa na sekta binafsi haiwezi kufanyika katika nchi yetu ama ikifanyika, itafanyika kwa mkwamo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *paragraph* inayofuata katika ukurasa wa 11, Serikali imefanyia marekebisho. *Paragraph* ya 12, Serikali imefanyia marekebisho, kwa hiyo, nimeitoa. Nakuja kwenye *paragraph* ya utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya sheria Ibara ya 11A inayokifuta na kuweka kifungu cha 22 yanapendekeza pamoja na mambo mengine, inapotokea mgogoro kati ya Mbia na Serikali, mgogoro husika utatatuliwa na Mahakama za ndani kwa kupitia sheria za ndani, yaani Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na ukweli kwamba tunazipenda na kuziheshimu sana Mahakama zetu, ni ukweli vilevile kwamba *PPP* inahusisha wawekezaji wa ndani na wa nje. Ukirejea vifungu kadhaa vya sheria vya mabadiliko ikiwemo kifungu cha 15 kuna miradi ambayo mbia anagharamia mradi husika kwa asilimia 100 kuanzia *feasibility study* mpaka mradi wenyewe. Mwekezaji yeyote makini anataka kwenda katika Mahakama za Usuluhishi wa masuala ya kibiashara ambazo ziko *neutral*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu wa kutumia Mahakama za ndani pekee kwa watu ambao tumesoma Sheria za Uwekezaji za Kimataifa tunalijua hili na najua Mheshimiwa Mtemi Chenge analijua hili. Utaratibu huu wa kutumia Mahakama za ndani pekee utawafukuza wawekezaji makini wa nje hasa kwa kuzingatia kwamba kuna miradi ambayo inatarajia wawekezaji watumie pesa zao wenyewe kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri wa Fedha ajue, tatizo la nchi hii siku zote siyo kutumia Mahakama za nje. Nchi hii imejikuta ikiingia katika madeni makubwa na kushindwa kesi kutokana na mikataba mibovu. Mikataba inakuwa mibovu Serikali ikifika katikati ya njia inaona haipati inavunja mikataba, tunafunguliwa kesi, tunashindwa kesi kwa sababu ya mikataba mibovu. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri, tushughulike na msingi wa tatizo na siyo kuangalia matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kama ambavyo tumeeleza hapo awali, nchi yetu itasonga mbele pale Serikali itakapoanza kuheshimu taratibu, kanuni na sheria zilizopo na hasa katika kuhakikisha yale yote ambayo imeomba Bunge lipitishe na Bunge likapitisha ili iweze kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PPP* ndiyo suluhisho la nchi yetu kwenda kwenye uchumi wa viwanda na wananchi kuwa na kipato cha kati, lakini kwa mtindo huu ambapo kila mradi ambao ni *economically viable,* basi Serikali inataka itekeleze yenyewe; mifano ni mingi sana kwa kuanzia kwenye sekta ya ujenzi ambapo kandarasi zote za majengo ya umma yanatekelezwa na taasisi ya umma yaani *TBA* na miradi mingine mingi tu. Hivyo, kwa muktadha huo, *PPP* inasimama wapi katika utekelezaji wa miradi ya kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka sasa taasisi hii ambayo jukumu lake kuu ni utunzi wa sheria, iweke maslahi ya Taifa kwanza kwa kuangalia mustakabali wa sheria tunazozitunga katika mawanda ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Tusiangalie sheria hizi kwa mtazamo ule unaoletwa na Serikali tu. Tanzania hii ni ya wote na hata wale ambao hawajazaliwa. Hivyo ni jukumu letu kutunga sheria zitakazotengeneza mazingira mazuri ya Tanzania ya kizazi cha sasa na Tanzania ya kizazi kijacho na siyo Tanzania ya mtazamo wa mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (MB), AKIWASILISHA MAONI YA KAMBI HIYO KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI, SURA 103 *(THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP (AMENDMENT)ACT,2018* - KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2016)

A: UTANGULIZI;

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kusimama upande wetu sisi wabunge wa upinzani tunaofanyiwa hila za kisiasa na Serikali hii kila kukicha.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wale wote ambao kwa njia moja ama nyingine wamefanikisha uandaaji wa taarifa hii, hasa wadau ambao wametumia muda wao kupitia muswada huu na kutoa maoni yao ambayo yamekuwa ya msaada sana katika kuchambua hali ya sekta binafsi hapa nchini na kutoa mwelekeo wa namna ya kujenga sekta binafsi iliyo imara kwa mustakabali mwema wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani unaonyesha kwamba sekta binafsi nchini inaelekea kuporomoka. Hii ni kwa sababu Serikali imeacha kutekeleza mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo ambao ndio dira inayotuongoza katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotakiwa kutekelezwa na Serikali kwa kipindi cha miaka mitano 2016/

17 hadi 2020/21; na badala yake inatekeleza shughuli na miradi mingine ambayo haipo katika Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; imeelezwa kwamba; miradi yote ambayo ni ya kibiashara; iachwe itekelezwe na sekta binafsi isipokuwa kama kuna sababu ya lazima ya kufanya vinginevyo. ***"Commercially viable projects should be left to the private sector, unless there is strong justification for doing otherwise".*** Miradi hiyo ambayo ni ***commercially viable*** imeorodheshwa na gharama utekelezaji wake, ambayo ni ujenzi wa SGR, Ujenzi wa kiwanda cha Liquified Natural Gas (LNG), Liganga Mchuchuma Industrial Park, Mtwara Petrochemical Special Economic Zone na Bagamoyo Special Economic Zone.[1]

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mpango wa Maendeleo kueleza bayana kuwa miradi hiyo itekelezwe na sekta binafsi; Serikali imeweka pembeni mapendekezo ya Mpango huo; na kutekeleza miradi hiyo yenyewe. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama Serikali ilileta bungeni sababu za msingi na za lazima za kuinyima sekta binafsi fursa ya kutekeleza miradi hiyo; na bunge likatoa kibali kwa Serikali kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo!

Mheshimiwa Spika, kitendo hiki cha Serikali kung'ang'ania kutekeleza miradi mikubwa ya kibiashara na kuiweka kando sekta binafsi kinyume na maelekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo; kinatoa ushuhuda kwamba, Serikali hii haina nia ya dhati ya kutekeleza Sera ya Ubia kati ya sekta umma na binafsi (PPP). Ukosefu wa nia hiyo, umeendelea kuonekana hata katika vifungu vinavyopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Utendaji wa Serikali hii ya awamu ya tano umeonyesha dhahiri kwamba sasa tunarudi kule tulikotoka kwenye ujamaa uliokomaa na ukomunisti ambapo sekta

[1] National Five Year Development Plan 2016/17- 2020/21 uk 88,89 ,90

binafsi haikuruhusiwa kabisa kushiriki katika ujenzi wa uchumi. Tunarudi kwenye enzi zile ambazo nyenzo kuu za uzalishaji zilikuwa zikimilikiwa na kuendeshwa na Serikali (State controlled economy).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama Serikali hii ya CCM imebadili sera zake za uchumi au la; kwa kuwa kinachofanyika sasa cha kuitenga sekta binafsi, ni kinyume kabisa na kilichofanywa na Serikali za awamu tatu zilizopita ambapo tulishuhudia soko huria likipewa nafasi katika ujenzi wa uchumi na kupelekea kuanzishwa kwa sera ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, vitendo vinavyofanywa na Serikali hii vya kutaka kila kitu kifanywe na Serikali Kuu si tu kwamba vinazidhalilisha Serikali za awamu tatu zilizopita (ambazo zote zilikuwa ni za CCM) bali pia vinaonyesha udhaifu mkubwa wa kukosa misimamo ya kisera kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) kuhusu namna uchumi endelevu unavyotakiwa kukuzwa na kuendeshwa. Baada ya Ujamaa kushindwa, uchumi duniani unaendeshwa kwa nguvu ya soko, ambapo sekta binafsi ni mdau muhimu. Kulazimisha kutumia mbinu za kijamaa katika zama hizi, kwa serikali kutaka kukumbatia kila kitu, ni kujitoa ufahamu na ni jambo ambalo haliwezekani ***(trying to run the economy without the private sector is simply an utopian idea...”***

Mheshimiwa Spika
Kambi Rasmi ya upinzani inaamini kwamba moja ya misingi mikuu ya kujenga uchumi imara ni kuruhusu ushindani wa soko huria, kuruhusu watu na sekta binafsi kumiliki mali kunako enda sambamba na kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha SEKTA BINAFSI kushamiri hatimaye kuchangia katika maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika,
Ni kwa bahati mbaya sana , serikali ya awamu ya tano badala ya kuichukulia sekta binafsi kama mdau wa maendeleo, inawachukulia kama washindani wa kibiashara hali

inayopelekea sekta hii kukumbwa na mkwamo! Katika kipindi hiki tumeshuhudia ongezeko kubwa sana la mikopo chechefu halikadhalika tumeshuhudia biashara kufungwa kwa kiwango ambacho hakijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu , huku wafanyabiashara wakilalamikia mfumo wa kodi ambao umekuwa si rafiki kwa wafanyabiashara hali inayochochea watu kutafuta mbinu mbalimbali kukwepa kodi badala ya kuona fahari kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika,
Ni Matumaini ya kambi Rasmi ya upinzani bungeni , Marekebisho haya pamoja na mambo mengine angalau yatafungua mlango kwa sekta binafsi kuwa chachu ya maendeleo katika nchi yetu.

B: MAPITIO YA MUSWADA;

PPP INASIMAMIWA NA NANI?

Mheshimiwa Spika,
Katika ibara ya pili, muswada umefanya marekebisho ya kiujumla ambayo yanaelekeza yafuatayo:

'deleting the words "Mininstry responsible for finance" wherever it appears in the Act and substituting for the word ministry"

Kwa lugha ya Kiswahili, kifungu hiki kimefanya marekebisho ya kiujumla kwa kufuta maneno wizara inayohusika na masuala ya fedha popote pale inapotokea na kuweka Neno wizara.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 3, kimetoa tafsiri ya maneno ' ministry' na 'minister' kama ifuatavyo. Minister means the Minister responsible for public private partnership na Ministry means the Ministry responsible for public private partnership.

Nimejaribu kupitia vifungu vyote, sijaona huyo waziri mwenye hiyo dhamana ni nani. Ikumbukwe kwamba sheria tunayoifanyia marekebisho PPP ilikuwa chini ya Waziri Mkuu. Kama Bunge tutakuwa wa ajabu sana kama tutatunga sheria pasipo kujua nani anayekwenda kuwa msimamizi mkuu wa sheria hiyo!

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 3 cha muswada kinachokifanyia marekebisho kifungu cha 3 cha sheria kwa kufuta tafsiri ya maneno " minister" and "ministry" na kuweka upya tafsiri ya maneno hayo, sambamba na hilo ni kufuta tafsiri ya "National Investment Steering Committee", kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 3(b). Aidha, kuongeza tafsiri ya "Small Scale PPP Project"

Mheshimiwa Spika, kuna tabia iliyozuka hivi sasa ya kuondoa madaraka kwa wanaowajibika moja kwa moja kwa Bunge na kuwapa watu wanaowajibika moja kwa moja kwa mamlaka za uteuzi wao.

MFANO MZURI; (a) Baraza la Mawaziri halijatajwa mahali popote katika Sheria ya Madini kama ilivyorekebishwa. Badala yake, wajibu wa kutoa leseni zote za uchimbaji madini umekabidhiwa kwa Tume ya Madini, kwa usimamizi wa Waziri wa Madini. Angalia kifungu kipya cha 19(f) cha Sheria ya Madini.

(b)Tume ya Madini ndiyo uwezo wa kusimamisha au kufuta kabisa leseni yoyote ya madini. Angalia kifungu kipya cha 24(m) cha Sheria ya Madini. Itakuwa maajabu ya Tanzania kwa Tume iliyoteuliwa na Rais kufuta leseni iliyotolewa na Baraza la Mawaziri linaloongozwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatarajia kwamba miradi mingi ya PPP inaweza kufanyika katika Sekta ya Madini na Nishati na hivyo mbali ya Sheria ya PPP ni lazima sheria na Kanuni za Sekta husika zipewe kipaumbele pia. Tukumbuke sheria hizi za rasiliamali zetu kwa kiasi kikubwa zinaingiliana na sheria moja haiwezi kusimama yenyewe kama hii ya PPP bila kuangalia sheria mama kwenye mradi wa ubia

husika kama kifungu cha 13 cha muswada kinachoongeza kifungu kipya cha 25A katika sheria mama.
Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inaona lingekuwa ni jambo la busara kuifanya kamati ya Taifa ya uwekezaji kuwa Taasisi imara, kwani uchumi wa Tanzania unategemea sana ubia na sekta binafsi na fursa bado ni nyingi mno.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 7A cha sheria mama kwa kufuta kifungu cha 7A1(c) na kukiandika upya , kufuta kifungu cha 7A(2) na kukiandika upya, pia kufuta kifungu cha 3 na kuweka kifungu kipya. Vifungu hivyo vilikuwa vinatoa muda wa siku kumi na tano kwa kamati ya Kitaalam ya PPP jukumu la kuidhinisha taarifa za Upembuzi yakinifu na kufanya uchambuzi wa nyaraka za miradi kwa wazabuni watakaopendekezwa katika miradi ya PPP. Marekebisho ya kuongeza siku hadi ishirini na moja(21) kwa kazi iliyokuwa inafanyika kwa siku 15 ni jambo la kujirudisha nyuma sisi wenyewe.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa Ubia ni fursa na Mbia makini jambo la kwanza kuliangalia ni **muda**, kama tunatunga sheria za kuzidisha muda katika biashara maana yake tunajipotezea fursa sisi wenyewe. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa vyema muda wa kuidhinisha, kama ilivyotumika katika kifungu kipya cha "c" ***consider and approve…..*** na katika kifungu cha "2***"…., approve feasibility studies,…*** Kwa timu mahiri ya wataalam, kazi ya kuidhinisha nyaraka sio ya kuongezewa muda badala yake muda **ungepunguzwa na kuwa ndani ya siku kumi(10) za kazi**.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani kupendekeza siku kupunguzwa lakini bado tunapenda kufahamu endapo siku 21 zilizopangwa kuongezwa zisipofanyiwa kazi ni hatua zipi zitachuliwa kwa mamlaka iliyoshindwa kuchambua nyaraka na kuzipitisha kama ilivyopangwa?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 10A cha sheria ili kukiwezesha Kituo cha Ubia kufungua Akaunti ya Mfuko wa Uwekezaji wa Miradi ya PPP katika Benki Kuu ya Tanzania badala ya Benki mahiri ya Uwekezaji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa ni benki ipi itumike katika mradi wa PPP inategemea makubaliano ya pamoja baina ya wabia, sambamba na hilo benki mahiri ya Uwekezaji ambayo ninaamini ndiyo inayotoa mkopo kwa ajili ya mradi. Ni ukweli kuwa ikisha kuwa benki mahiri kwa uwekezaji inakuwa na wataalam mahiri wa kusimamia na kushauri utendaji wa jinsi mradi utakavyoendeshwa ili kuhakikisha fedha zilizotolewa na benki husika zinarejeshwa na faida inapatikana. Hivyo basi, kitendo cha kuweka kwenye sheria kuwa Akaunti ya Mradi wa PPP ni lazima ifunguliwe Benki Kuu hakikuzingatia kuwa miradi ya PPP ni ya aina nyingi kulingana na aina ya miradi yenyewe kama vile; Build Operate and Transfer - BOT, Design -Build – Operate - DBO, Management and Operating, Concessions n.k.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 15 cha sheria mama kuhusu mamlaka ya Waziri kutoa msamaha wa kutokuhusisha ushindani kwenye zabuni ya miradi ya kipekee iliyoibuliwa na Sekta Binafsi, miradi hiyo imeitwa **"unsolicited Project".** Kifungu hicho kimetoa masharti mengi na magumu sana kuweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inaiona kuwa miradi hii ndiyo miradi ya ubunifu kutoka sekta binafsi kwani ndiyo miradi inayoibuliwa na watu wanaoangalia mazingira halisi na kuona fursa, miradi ambayo sio kila mtu anaweza kuiibua, hii ndiyo miradi inayotofautisha uwezo wa wajasiriamali katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wetu miradi hii ilitakiwa isiwekewe masharti kabisa, jambo kubwa ni uhusika wa Serikali katika kuhakikisha inaratibu kwa haraka mahitaji ya kisera au kisheria ili miradi hiyo iweze kuanza, kwa kuzingatia

kwamba miradi mingi ya aina hii inakuwa tayari ina vyanzo vyake vya kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki, kama tulivyosema awali kuwa ni njia mojawapo ya kuizika Sekta binafsi, kwani masharti hayo yaliyomo kwenye kifungu cha 10 cha muswada ni dhahiri kuwa miradi hii ya kipekee inayoibuliwa na sekta binafsi haiwezi kufanyika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 23 cha sheria kwa kuongeza kifungu kipya cha 23A, kifungu hiki kinaitaka PPP Centre kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa kila robo mwaka. Dhana nzima ya kifungu hiki ni kuongeza uwajibikaji kwa taasisi zinazotekeleza miradi. Waheshimiwa wabunge naomba niwakumbushe wakati tunapitisha muswada wa sheria mbalimbali Namba 1 tarehe 28.06.2017, naomba kunukuu;

> *"**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa marekebisho ya Sheria mbalimbali ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 1 juzuu ya 98 tarehe 12 Januari, 2017. Kwa ujumla wake muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Bajeti Sura 439*
>
> ***Mheshimiwa Spika**, ukisoma madhumuni na sababu za kuletwa kwa muswada huu hasa sehemu ya pili ya Muswada ambao inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 katika vifungu vya 47(7), 53(2), 56(1) na 7, 57, 61, 62 na 63 na serikali imeleta marekebisho hayo kwa ajili ya kuiwezesha serikali kuwasilisha Bungeni taarifa ya uhamisho wa fedha, taarifa ya matumizi, taarifa ya utekelezaji, taarifa kuhusu misamaha ya kodi na taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi sita badala ya robo mwaka kama ulivyo utaratibu wa kisheria wa sasa.*
>
> ***Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuweka wazi kuwa haiungi mkono marekebisho yote kwenye Sheria ya Bajeti kwa*

sababu marekebisho haya ya Sheria ya Bajeti yatapunguza mamlaka ya Bunge kuisimamia serikali".

Mheshimiwa Spika, pamoja na uamuzi wa serikali kutaka taarifa ya miradi ya PPP itakuwa ikiletwa bungeni kila baada ya nusu mwaka ni muendelezo wa serikali isiotaka kusimamiwa kwa wakati hivyo itapekelea miradi mingi kushindwa kupata usimamizi wa kutosha wa mara kwa mara na bunge. Kambi rasmi bungeni inaitaka serikali ipitie upya sheria hii ili muda urekebishwe kwa kuwa serikali imejisahau sana na haifanya kazi kwa ufanisi.

Utatuzi wa Migogoro

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya sheria yanapendekeza pamoja na mambo mengine inapotokea mgogoro kati ya mbia na serikali, mgogoro husika utatatuliwa na mahakama za ndani kwa kupitia sheria za ndani.

Mheshimiwa Spika, mbali na ukweli kwamba tunazipenda na kuziheshimu sana mahakama zetu, ni ukweli vilevile kwamba PPP itahusisha wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa Nje. Mwekezaji yeyote makini anataka kwenda katika mahakama za usuluhishi wa masuala ya kibiashara ambazo ziko "neutral"! Utaratibu huu wa kutumia mahakama za ndani pekee utawafukuza wawekezaji makini wa nje hasa kwa kuzingatia kwamba kuna miradi ambayo inatarajiwa wawekezaji watumia pesa zao wenyewe kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, Tatizo sio kutumia mahakama za nje. Nchi hii imejikuta ikiingia katika katika madeni makubwa na kushindwa kesi kutokana na mikataba mibovu. Tushughulike na Tatizo na Msingi na Sio Matokeo!!

C. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeeleza hapo awali, nchi yetu itasonga mbele pale serikali itakapoanza kuheshimu utaratibu, kanuni na sheria zilizopo na hasa katika kuhakikisha

yale yote ambayo imeomba Bunge lipitishe na Bunge likapitisha ili iweze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, PPP ndiyo suluhisho la nchi yetu kwenda kwenye uchumi wa viwanda na wananchi kuwa na kipato cha kati, lakini kwa mtindo huu ambao kila mradi ambao ni **economically viable** basi Serikali inataka itekeleze yenyewe, mifano ni mingi sana, kwa kuanzia kwenye sekta ya ujenzi ambapo kandarasi zote za majengo ya umma yanatekelezwa na taasisi ya umma (TBA),na miradi mingine mingi tu. Hivyo kwa muktadha huo PPP inasimama wapi katika utekelezaji wa miradi ya kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, ni muda mwafaka sasa, taasisi hii ambayo jukumu lake kuu ni utunzi wa sheria, iweke maslahi ya Taifa kwanza kwa kuangalia mustakabali wa sheria tunazozitunga katika mawanda ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Na tusiangalie sheria hizi kwa mtazamo ule unaoletwa na Serikali tu. Tanzania ni ya wote na hata wale ambao bado hawajazaliwa, hivyo ni jukumu letu kutunga sheria zitakazotengeneza mazingira mazuri ya Tanzania ya kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

Halima James Mdee(Mb)
MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO
11 Septemba, 2018

MWENYEKITI: Ahsante, kwa taarifa yako. *(Makofi)*

Endeleeni kupiga makofi tu, nazikata dakika hizo. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naitoa hoja hii kwenu sasa muiamue katika hatua ya kwanza tunaanza na mjadala. Nina orodha ya wachangiaji hapa na Muswada huu tunao leo na kesho, kwa hiyo, mna fursa nzuri ya kuishauri Serikali katika kitu hiki kizuri ambacho kiko mbele yetu. Nianze na watatu wa kwanza. Nianze na Mheshimiwa Ally Saleh (Albeto), atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Kigua na Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ni dakika 10, 10 tu.

MHE. ALLY SALEH ALLY: 10 eeh, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika siku muhimu kwa historia ya kiuchumi ya Tanzania. Ni siku muhimu kwa sababu tulikuwa tunatarajia Muswada kama huu ambao utashawishi sasa mitaji ya binafsi kuja kwa masharti ambayo pengine yatakuwa bora zaidi. Umechelewa kuja lakini maadam umeshafika, basi tutaupokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubali kuwa tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda na Waswahili wanasema kila ngoma ina masharti yake. Ngoma hii ya uwekezaji ina masharti yake. Hatuwezi ku-*dictate* sisi *terms,* lazima tutazame *terms* ambazo zinafanana na ulimwengu ili tuzilinganishe na mazingira yetu, tuzioanishe na tuweze kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda ni kuwa na sheria imara. Ukishaweka misingi ya sheria, basi utafanya vizuri. Uchumi wa viwanda maana yake ni kuwa na sera

ambayo ina mapana, ni *wide looking* na ni *far looking*. Kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani nchi hii siyo tunaoishi sisi tu leo ni pamoja na ambao wataishi miaka mingi baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Zambia ina-*suffer;* kiwanja chake cha ndege kimechukuliwa, shirika lake la umeme limechukuliwa kwa madeni ambayo yamekopwa toka zama za Kaunda. Hali kadhalika, nchi ya Sri Lanka tangu wanapigana wenyewe kwa wenyewe wamekopa kwa Wachina hivi sasa wameanza kufilisiwa. Kwa hiyo, kila mara tukifikiri, tufikiri sisi na wengine wanaokuja ili makaburi yetu yasije yakalaaniwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pamoja na kuwa na mipango imara. Tuna Mpango mzuri wa Taifa ambao unalenga katika kuimarisha nchi hii, lakini cha muhimi pia ni kubadilisha *mindset* za watu wetu. Watendaji wengi wa Serikali hawaendi na wimbi la mabadiliko, hawaendi na mtazamo wa kidunia. Kwa hiyo, hiyo ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ili kuvutia mitaji ni lazima utayarishe umma. Kwa hiyo, haya yote ni maandalizi ambayo yanaweza kutangulia ingawa yanafanywa kwa *phases,* lakini yakikamilika ndiyo maana unaweza kuwa na watu. Leo ukienda Malaysia, China watu wenyewe wanakaribisha uwekezaji, watu wenyewe wanakaribisha mipango ya nchi yao na wanaipokea na wanaifurahia kwa sababu wameelekezwa katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu kubwa ujenzi wa viwanda au uchumi wa viwanda au uwekezaji mara nyingi una njia nyingi. Iko njia ya mikopo na njia ya mitaji ya watu binafsi. Hii ndiyo ambayo sheria hii sasa inaelekeza. Uzuri wa sheria hii sasa inasogeza kwamba itakuwa *centered* pamoja kwamba pengine siyo kila Wizara itakuwa inafanya, lakini imeletwa kwa pamoja, ambapo jambo hili litasaidia kujenga na tutakuwa tunaona taasisi moja inasimamia na uimara wa nchi unaonekana kwa sababu mipango inaweza ikapita katika *system,* ikaonekana na ikatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuvuta mitaji kwa kubakia katika ujamaa ni lazima soko lifanye kazi. Hata Wachina wenyewe ambao mara nyingi wamekuwa ni mfano wetu, wametoka, pamoja na ujamaa wao lakini wakatengeneza *economic zones; Dalian, Guangzhou, Wenzhou, Nantong* na kwingine kwingi. Kutokana na kile, ndipo wakaweza kutengeneza mazingira yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia soko lina masharti yake na uzuri wake. Uzuri wa kuvuta mitaji ya *PPP,* maana yake unapata miradi haraka inakuja kwako, *investment return ni greater* kwa sababu inasimamiwa vizuri. *Tendency i*mekuwa ikionesha, miradi ya kiserikali ina ukakasi mwingi, ina mambo mengi, vichochoro vingi, lakini miradi ikiwa ni ya *PPP investiment return* inakuja haraka. Vilevile unapunguza *risk* inakuwa *transferred* kutoka kwenye Serikali kwenda upande wa *private*. Ikiwa Serikali imeshiriki, basi *risk* itakuwa *50, 50* lakini ikiwa ule mradi umekuwa *funded* moja kwa moja na *private* ina maana *risk* moja kwa moja inakwenda *private* na Serikali inakuwa imeepuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu inasaidia bajeti ya nchi kupumua. Kama una miradi ambayo watu binafsi wamechangia, ina maana pesa zako zinapumua unaweza ukazi-*direct* kwenye mambo mengine. Hapo ndiyo unapokuwa na nafasi nzuri zaidi ya ku-*target* miradi ya kijamii ambayo ni makosa kuikopea *unless* iwe ni muhimu sana kukopea miradi ya kijamii kwa sababu mara nyingi wanataka ile miradi ambayo inarudisha pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi nakubaliana na Kambi ya Upinzani, kwa sababu katika sharti muhimu la uwekezaji ni *predictability*, namna ambavyo unaweza kutabiri. Kwa hiyo, haiwezekani unataka miradi lakini leo unafanya hili, kesho unafanya lile, Mkuu wa Wilaya huyu anafanya hivi, Mkuu wa Mkoa huyu anafanya hivi; huyu ananyang'anya *passport,* huyu anawatia ndani wawekezaji. Kwa hiyo, utakuwa huwezi kwenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana na Kambi ya Upinzani kwamba mambo tuliyotaka, mojawapo ni *time of doing business.* Serikali badala ya kupunguza siku za kupitisha miradi imeziongeza kutoka 15 kwenda 21, hakuna sababu ya msingi. Utaalam upo wa kutosha, kuna watu wa kutosha, kwa nini tutoke siku 15 twende 21? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine ambalo limekuja halina maelezo ya kutosha ni suala la kwamba wafunguaji wote wa miradi hii waweke fedha *BoT.* Hakuna maelezo ya kutosha zaidi ya kwamba tumetangaziwa. Pengine hii ina madhara yake kwa sababu unakwenda kuiweka Benki Kuu ya nchi katika mazingira magumu ya kusimamia jambo ambalo pengine lingeweza kusimamiwa na benki nyingine yoyote ambayo wadau wawili wanaoshiriki katika ule mradi wanaweza kukubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nitalizungumzia kwa undani kidogo ni suala la *unsolicited projects.* Hili nitapenda ni-*declare interest* kwa sababu ya kitu ambacho nimekiona na ndiyo maana nimefurahia kwamba kuna mabadiliko makubwa yanafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 4 anasema kwa sasa sheria haikubainisha vigezo au masharti ambayo yanaweza kuruhusu baadhi ya miradi inayoibuliwa na sekta binafsi *(unsolicited proposal)* kutokushindanishwa. Kwa maana nyingine, katika kifungu cha 10 kinachobadilisha kifungu cha 15, kimetaja hayo masharti ambayo mradi ambao ni *unsolicited* unaweza kukubaliwa. Mengi ya masharti haya, watu hawa wa nje wanaweza wakayakubali, mtu ambaye anatafuta kuleta mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kwa kujua shida ya umeme ya nchi na *alternatives* za umeme, niliiandikia Serikali kwa Wizara inayoshughulika na Nishati kwamba nina mwekezaji ambaye yupo tayari kuwekeza mpaka *one billion Euro* kwa kutupatia nchi hii *1,000 megawatts* ambazo baadaye anaweza akazisogeza kwa mujibu wa mahitaji ya

Serikali. Nimeiandikia Wizara ya Nishati, majibu niliyopata kutoka kwa Katibu Mkuu, anasema kwamba lazima iingie katika *competitive process.* Mimi katika barua ya pili niliyomwandikia, nikamuuliza *competitive process* anashindana na nani? Kwani unao watu wengine ambao wameleta *offer* kama hiyo? *Competitive process* kwa maana ipi nyingine? Maana nimeshindwa kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri Wizara ile ingeniambia mlete mwekezaji aje ajieleze tuone... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Saleh kwa mchango wako mzuri tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Omari Kigua.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niwe mchangiaji wa pili kwenye jambo muhimu sana katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali hususan Waziri wa Fedha kwa kuleta jambo hili la *PPP* ambalo mimi kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nilipata fursa kulizungumzia hapa kwa sababu nilikuwa najua umuhimu wa Muswada huu au nini maana ya *PPP* kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Muswada huu au marekebisho haya ya *PPP* ni kwamba Serikali itafaidika na mambo mengi sana hususan katika huduma za kijamii, kwa maana ya hospitali, barabara na kadhalika. Serikali ina majukumu mengi; inataka ujenzi wa barabara na hospitali, lakini yote haya Serikali isingeweza kuyabeba, imeona ni muafaka sasa hivi kuweza kuruhusu sekta binafsi iweze kushiriki katika mambo haya. Hili ni jambo la kupongeza sana

kwa sababu tutaruhusu Halmashauri zetu, miradi mingi ambayo ilikuwa imekwama, watu wenye uwezo wao sasa waweze kuisaidia Serikali na mambo yaweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia maelezo ya Mheshimiwa Waziri na Kamati hapa, nina mambo machache ya kushauri ambayo pengine wakiona yana maana au yana umuhimu, basi waweze kuyachukua. Nimeona kwamba baada ya kupitia kwenye c*enter* ya *PPP* kwenye uidhinishaji wa fedha, ataidhinisha Waziri mwenye dhamana. Nadhani hili jambo tulitazame sana kwa sababu baadhi ya miradi itakuwa ina fedha nyingi. Nashauri tuone namna ambavyo ikiwezekana Mheshimiwa Waziri apitishe kwenye Baraza la Mawaziri kabla ya kuidhinisha Waziri mwenye dhamana ya fedha peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu hili linakwenda sambamba na kipengele kile ambacho kinaonesha kwamba kuna miradi ambayo ikiletwa sekta binafsi inaweza kupitishwa bila kupitia kwenye *competition.* Sasa hii inaweza ikatoa mwanya kwa Waziri asiyekuwa mwaminifu akaweza kupitisha vitu ambavyo baadaye vinaweza kuwa na sura ambayo siyo nzuri. Naomba ikiwezekana kwenye Muswada huu tuone namna ambavyo Waziri wa Fedha peke yake asipitishe, lazima ipite kwenye *Cabinet.* Nadhani huo ushauri ni muhimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nimepitia kwenye Taarifa ya Kamati ya Bajeti, wao wamependekeza kwamba kifungu cha 4(5) hizi Halmashauri au Wizara kabla hawajapeleka kwenye *center* ya *PPP* ni kwamba lazima taarifa ile apelekewe Waziri wa Fedha. Nadhani hilo halina umuhimu kwa sababu huku tuna wataalam watakuwa wameshapitia na Waziri sehemu yake itamfikia. Kwa hiyo, hakuna sababu hiyo taarifa imfikie Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimeona kwamba hii *PPP center* itakuwa na *role* kubwa sana ya kupitia hii miradi. Ushauri wangu naona hapa wawepo wataalam wabobezi

sana, wenye *negotiation skills* za hali ya juu sana ili isije ikatokea baadaye tukaonekana tulipitisha miradi ambayo haina tija kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kama inawezekana, kwa nini hii *PPP center* isiwe sehemu ya *TIC* kama *department* pale? Kwa sababu naona tunaanzisha idara kama vile kuongeza majukumu na ajira pasipokuwa na sababu. Nadhani dhamira ya Muswada huu ina lengo la kutaka kuipunguzia Serikali majukumu mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kutoa ushauri wangu ni suala la elimu. Elimu katika Halmashauri zetu ni muhimu kwa sababu jambo hili ni geni sana, linahitaji uelewa wa hali ya juu sana. Leo hii hata mtu ukimwambia *Public Private Partnership,* mwingine anaona ni jambo geni sana. Nashauri Wizara yenye dhamana ya jambo hili, basi ianze kuandaa mafunzo ya msingi kabisa kwa ajili ya watu wetu katika Halmashauri na Idara ili wananchi au watumishi hao wawe wana uelewa mpana wa kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kipengele cha kufungua akaunti kwenye Benki Kuu ya Tanzania. Naliona jambo hili kidogo halijakaa sawa, kwa sababu mwekezaji anayetaka kuja kuwekeza mradi hapa Tanzania usimwekee *condition* ya kufungua akaunti Benki Kuu. Nadhani ushauri mzuri zaidi ni kufungua *investment banks,* yaani hizi benki kwa ajili ya miradi ziwe nyingi kwa sababu tunayo moja tu *TIB* ambayo ukiangalia kwa uhakika haifanyi kazi vizuri sana. Sasa kwa sababu dhamira ya Serikali imeamua kukaribisha sekta binafsi, nashauri kwamba Serikali iangalie namna ya kufungua benki nyingi ambazo zitakuwa zinawezesha watu kwa ajili ya uwekezaji katika sekta hii ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kushauri ni kuangalia watu watakaoshiriki katika hii *PPP center* wamekuwa *vetted* kiasi gani na wana uadilifu kiasi gani? Kwa sababu miradi hii itakuwa ni miradi ya fedha za umma. Ukiiangalia dhana ya *PPP* ni kwamba mtu ana

pesa yake, anatoka nje ya nchi anakuja hapa, anataka kujenga barabara au hospitali, lakini miradi ile baada ya miaka 10 maana yake itakuwa ni mali ya Serikali. Sasa ikiwa ni miradi ambayo ina taswira kidogo ya kutokuwa na uaminifu, maana yake gharama ile itakuwa ni gharama ambayo Serikali imeingia. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba watu watakaokuwa wanapitia miradi hii wawe ni watu ambao wana uadilifu wa hali ya juu sana na ni watu ambao wana uzalendo, wenye kuangalia maendeleo mapana ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Omari Kigua.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile Serikali imetoa orodha ya mabadiliko, naomba mnapochangia m-*take into account* kwamba mnayo mabadiliko hayo. Sasa kama nimegaiwa mimi hapa Mezani, naamini na ninyi mnayo. *Assumption* yangu ni *correct?*

WABUNGE FULANI: Tunayo.

MWENYEKITI: Mnayo, haya. Kwa sababu itarahisisha sana.

La pili, sheria hii ipo, ilifanyiwa marekebisho 2014, inafanyiwa tena marekebisho baada ya miaka minne ili kuiboresha zaidi, siyo kwamba tunatunga sheria mpya. Tunaimarisha misingi iliyopo kwenye sheria hiyo ili kuleta ufanisi zaidi.

Nilimtaja Mheshimiwa Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Semesi.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani na moja kwa moja naunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Kwanza kwa wale tuliokuwepo, tunakumbuka Serikali ilikuwa inafanya kila kitu; nakumbuka hata mpaka na kuuza nyama kwenye bucha Serikali ilikuwa inamiliki yale maduka ya nyama. Baadaye ilionekana kwamba Serikali haiwezi kufanya kila kitu. Tulipoingia Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne tukaja sasa na Sera ya *PPP,* maana hii ni ya siku nyingi ili kuiwezesha sekta binafsi ichangie katika maendeleo ya uchumi kwa sababu sekta binafsi ndiyo *engine of growth,* inaajiri watu wengi na inachangia sana mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka hii kama miwili, mitatu nimeona kama hii sera tunachosema ni tofauti na tunachofanya. Kwa mfano, wakati ule *TBA* kazi yake ilikuwa ni miradi mikubwa ya ujenzi. Kazi kubwa ya *TBA* ilikuwa ni ufuatiliaji, tathmini na usimamizi, lakini ghafla awamu hii *TBA* sasa ndiyo inajenga majengo makubwa ndani ya nchi na sekta binafsi tumeiweka kando. Sasa inakuwaje tena tunasahau kwamba sekta binafsi ndiyo *engine of growth* na ndiyo inaleta ajira na Serikali kazi yake kubwa ni usimamizi, ufuatiliaji na tathmini. Naona sasa Serikali imehama tena kwenye jukumu lake hilo inakwenda kwenye utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika miradi mikubwa kwenye Mpango wa Maendeleo kama ilivyozungumzwa kwenye maoni ya Kambi ya Upinzani, miradi mikubwa ya kibiashara katika Mpango wa Maendeleo ilikuwa itekelezwe kibiashara na iachiwe sekta binafsi, lakini ghafla Serikali yenyewe sasa imeichukua hiyo miradi mikubwa, inakopa na inafanya kila kitu wenyewe. Ukiangalia *TBA* kila kitu wanafanya wenyewe; wananunua vifaa, wanajenga na wanatathmini wenyewe, huo siyo utawala bora, inabidi turudi kwenye misingi ya utawala bora*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ninavyoliona kwa Serikali ni usimamizi, tathmini na ufuatiliaji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake

atueleze ni jinsi gani Serikali imejipanga katika kufanya kazi yake kubwa ya msingi ya usimamizi, tathmini na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujui, mimi nasema tunajua tulipotoka; najua tumetoka kwenye uchumi wa kijamaa lakini mpaka sasa hivi sijui tunakwenda wapi? Sijui kwenye uchumi wa soko au hatupo kwenye uchumi wa soko. Tunaomba Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha atuambie tunakwenda wapi? Maana yake kwa jinsi navyoona Serikali inavyofanya kazi sasa ni kama tunarudi tena kule kule tulikotoka kwenye uchumi wa ujamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba inaiwezesha sekta binafsi kwa kuweka mazingira mazuri ili iweze kujiendesha na kuleta maendeleo. Tumeshuhudia jinsi ambavyo biashara nyingi zimefungwa kwa sababu wameshindwa kuendesha shughuli zao za biashara kutokana na mazingira ambayo siyo rafiki katika uwekezaji. Pamoja na miradi mikubwa tunayoizungumzia ya *PPP* lakini bado kuna wafanyabiashara ambao wanahitaji mazingira mazuri waweze kuendesha shughuli zao za biashara ili uchumi uweze kukua na tuendelee kupunguza umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia suala la *PPP,* napenda Mheshimiwa Waziri akija kuhitimishia atuambie ni kwa jinsi gani ameangalia suala la rasilimali watu maana tumeona tumekuwa na mikataba mingi mibovu kwa sababu ya kukosa wataalam wenye utaalam wa kutosha uliobobea katika mambo ya mikataba na mikataba ya Kimataifa. Tumeshuhudia mikataba mingi mibovu ambayo imesainiwa na imetuingiza katika hasara kubwa kwa sababu tumevunja mikataba na sasa tunadaiwa *left, right and center.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Maendeleo na pia katika hotuba ya Elimu ya Juu hakuna mahali popote ambapo nimeweza kuona kulivyoanishwa hizi rasilimali watu tunazozizungumzia tunazohitaji kwenye mikataba. Ni vizuri kuwa na *negotiating pool team* ambayo

imefunzwa vizuri, ipo *very strong* na ambayo itaweza kusimamia masuala ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la fedha tunayo benki moja tu ya *TIB.* Tumeona benki nyingi, nyingine zimeshafungwa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anajua na benki nyingi wamepunguza wafanyakazi kwa sababu shughuli zao haziendi vizuri. Sasa ni jinsi gani Serikali itahakikisha kwamba tunakuwa na benki zaidi ili kuwawezesha watu binafsi kukopa, waingie ubia na Serikali kusudi waweze kuleta maendeleo katika nchi hii? Hayo mambo ni *very serious* na bila kuhakikisha sekta ya fedha ipo madhubuti, hata hili wazo la *PPP* tutalishindwa asubuhi kweupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba sasa wanategemea kwamba Serikali za Mitaa na taasisi binafsi ziweze kutengeneza *proposals* za kuhusisha sekta binafsi katika ubia. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, hivi *Local Government* itapata wapi pesa ya kuandika *proposal?* Maana wamesema watenge kwenye bajeti yao, bajeti gani wakati *property tax* mmechukua, hela za mabango mmechukua na pesa nyingi zimechukuliwa kutoka Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo wote tunajua hazipelekwi. Sasa Serikali za Mitaa itawezaje kujihusisha kweli kwenye *PPP* ikiwa vyanzo vyake vya mapato ni kidogo na inashindwa hata kusimamia huduma za jamii kwenye Wilaya na sekta mbalimbali? Mheshimiwa Waziri aje atueleze kuhusu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea pia katika kuangalia hii *PPP,* maana katika *PPP* tuna *Build Operate and Transfer, Build Operate and Own, Design Build and Operate* na *Joint Venture.* Nadhani ni muhimu sana sasa kwa Serikali kuangalia mambo matatu ambayo nimeshazungumzia. Kwanza *human resources,* pili kuangalia *financial base* ya kuwezesha hivi vitu kufanya kazi na tatu kuhakikisha kwamba

sheria na kanuni zinazingatiwa kwa ufasaha na kwa umakini ili kuwezesha *private sector* kuja ku-*invest* katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, napenda nitumie nafasi hii kutambua mgeni mashuhuri aliyepo katika *Speaker's Gallery.* Tunaye Balozi wa India nchini Tanzania, Bwana Sandeep Arya. Karibu sana Balozi. Ameambatana na Afisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, Ndugu Jemanus Morris. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, nchi yetu na India tuna mahusiano mazuri sana ya miaka mingi. Mahusiano haya katika kipindi cha hivi karibuni, mtakumbuka kupitia bajeti ya Serikali, tuna miradi mingi sana, hasa upande wa maji ambayo imefadhiliwa na Serikali ya India; upande wa Ziwa Viktoria. Mtakumbuka juzi ule mradi wa Dola za Marekani milioni 500 ambao ulikuwa umekwama kwa sababu ya tatizo moja la kisheria ambalo ninyi mlikuja mkalinyoosha. Kwa hiyo, *we are glad to have you with us here and we value and recognize the contribution of your Government to Tanzania and we look forward working with you and your Government.* Karibu sana Balozi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Semesi, atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Mbene.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi. Natambua kwamba Serikali imeyachukua maoni karibu yote ya Kamati yetu ya Bajeti lakini nataka kuongeza mambo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, katika Muswada wetu ukurasa wa 6, kuna *amendment* katika *section 10A,*

Ibara ya 9 ambayo inasema kwamba fedha hizi za *PPP* zitaingizwa katika *a bank account.* Sasa ingependeza hii *bank account* ikaelezewa iko wapi? Itolewe tafsiri kama iko kwenye *BoT,* iko kwenye *commercial banks,* kwa sababu pale walikuwa wameshaji-*commit* kwamba itakuwa kwenye *reputable investment bank,* lakini sasa wameiacha iko *very vague. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni katika Ibara ya 10, ukurasa huo huo wa 6, *amendment of section 15.* Ibara ya 10 iko *specifically* ikiongelea sifa zilizoainishwa za miradi ya kipekee ya uwekezaji kwa njia ya ubia *(unsolicited projects).* Ukiangalia katika hiyo Ibara ndogo ya (a) inasema:-

"*The project shall be a priority to the Government at the particular time and broadly consistent with the government's strategic objectives".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sifa hii iliyowekwa hapa kwa nini unam-*limit* huyu mbia ambaye anataka kuingia ubia na Serikali kwamba huo mradi wake lazima uwe sambamba na *priorities* za *government at a particular time* kwa muda *specific* na *strategic objectives?* Nikakaa nawaza, tuna dira au sera yetu ya kusema kwamba ni uchumi wa viwanda, lakini uchumi huu wa viwanda unaendeshwa na nini? Masuala ya elimu yapo, kilimo kwa upana wake kipo, mifugo, uvuvi na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sekta nyingi ambazo zinakwenda ku-*feed in* kwenye sekta ya viwanda. Sasa huyu mbia kama yuko kwenye wilaya au mkoa fulani, kila wilaya na kila sehemu ina *specific needs* zake na ina *progress* fulani katika sekta fulani, kama ni ya viwanda *at that particular time* tunayoiongelea sasa hivi. Kwa nini sasa unambana huyu mbia unasema, kuwa kwenye *priorities* za hiyo *government? What priorities? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuona katika Bunge hili tunasema *priority* ya mwaka huu ni maji, yaani bajeti

inabeba tu masuala ya maji au bajeti hii mwaka huu tunataka kuona masuala ya kilimo tunavuka yaani iko *too broad.* Kwa hiyo, kwangu naona haina mantiki na haiko sawa, labda wai-*shape* vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ndogo ya (b) pia inasema:-

"*The private proponent does not require Government guarantee or any form of financial support from the Government."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri, tuko wote kwenye Kamati hii ya Bajeti; tulikuwa na *discussion* ndefu sana hapa, lakini bado naona kipengele hiki kipo kama kilivyo, hata kwenye *amendment* sioni chochote. Tunasema tunaingia ubia *(partnership), partnership* maana yake nini? Yaani wewe hutaki *commitment* ya aina yoyote, hutaki *guarantee* ya aina yoyote, *partnership* maana yake nini? Kwa nini *Government* inajitoa asilimia 100 na hapa tunasema ni *Public Private Partnership?* Kuna sisi wananchi, kuna *private sector,* lakini huyu *Government* anasema hapana, mimi siji-*commit* kwa lolote lile. *Where is the partnership in here? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasisitiza hiki kifungu hakijakaa sawa na inaonesha kwamba tunaendelea kuweka mazingira magumu kwa mwekezaji. Yaani wewe hutaki kumsaidia huyu mwekezaji kwenye *issues* tu labda za *land,* utaalamu na vitu vinginevyo, au *finances* za aina yoyote; yaani unajitoa asilimia 100. Kwa hiyo, bado haina mantiki yoyote kuwepo hapa kwa sababu haiendani na hiki kilicho mezani kuhusu *issue* ya *partnership. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya (3) ukurasa huo huo wa 6, Serikali imefanya *amendment* na kifungu hiki kilikuwa kinaongelea kwamba yule mwekezaji aoneshe *commitment* na *commitment* hiyo aoneshe kifedha ili kwamba usilete usumbufu wa aina yoyote, kuonesha *seriousness,* basi *deposit.*

Tulitoka kuanzia asilimia 15, tukaenda 5%, sasa hivi naona inasomeka 3% ya kile anachokikadiria ku-*commit* katika ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha (3A) sasa kinasisitiza kwamba, *the Minister may make regulations prescribing procedure for refund* ya ile *commitment.* Huyu *private sector* anayeingia ubia, hizi *projects* ni za mabilioni ya fedha na fedha hii ya huyu *private sector* haitoki mfukoni, wengi wao ni mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea kipengele nilichokiongelea unasema kwamba hutaki *commitment* ya aina yoyote lakini unataka *guarantee from* huyu mbia; unataka hela, kwamba mpeni 3% unachokikadiria ambacho utakitumia, sijui ni shilingi trilioni 2, shilingi trilioni 3 au shilingi trilioni 20, unataka 3%. Tukabanana kwenye Kamati kwenye suala hili kwamba siwezi tu nikakupa, *for what purpose?* Inaingia kwenye mfuko gani? Una *role* gani pale mpaka uichukue hela yangu ambayo mimi nakwenda ku-*invest* na hela hizi zina riba kubwa kwa sababu ni za mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unatuambia kwamba *the Minister may make regulations.* Sasa kwa *layman* kama mimi kwenye sheria au kwenye hii lugha ya kusema '*may,'* kwa hiyo, ina maana *it is not mandatory.* Unaweza ukajisikia usitengeneze hizo *regulations* ukabaki na 3% ya hela ya mdau, unafanyia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo basi, mimi nina-*propose* kipengele hiki kisomeke *the Minister shall make regulations* na *on top of that* kwa wataalam wanisaidie kwenye lugha hii ya kisheria, siyo tu waseme *shall make regulations* na aseme ni muda gani hizi hela zitakuwa *refunded* ili kusilete ile lugha ya 'kiendacho kwa mganga hakirudi'. Kwa sababu tumeona Serikali yetu ina hako kamchezo ka kuchukua hela za wadau na kutozirejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka niligusie ni katika utaratibu mpya wa uidhinishaji wa miradi ya *PPP.* Ukiangalia hii, iko kwenye taarifa yetu ya Kamati ya Bajeti, ukurasa ule wa 2 kutoka mwisho, kuna *chart* pale, inaonesha kwamba utaratibu wa kwanza unaanza kwa Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa ndiyo wanaoanza *initiation* ya kuandaa maandiko ya miradi na kufanya pembuzi yakinifu. Inateremka mpaka kule chini inasema sasa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji watafanya uidhinishaji wa miradi pamoja na mikataba wakishirikiana kutengeneza ile mikataba pamoja na *AG.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* yangu ya kwanza kwenye hili, hapa wadau wa kwanza inategemeana na huo ubia unaanzia katika *level* ya Wizara au Idara sijui ni ndani ya Wizara au ni Idara katika mamlaka husika au *through* TAMISEMI. Nikawa najiuliza, ametoka kuchangia Mheshimiwa Ruth Mollel akagusia kuhusu hizi *Local Government Authorities,* tunataka tuingie ubia na mwekezaji kwenye *Local Authority* fulani, je, mamlaka hizi kwanza tunajua zina shida ya kifedha, ana uwezo huo wa kufanya kazi na huyu *private sector?* Serikali za Mitaa zina wataalam wanaoweza kufanya hizi pembuzi yakinifu? Kwa hiyo, kuna *issue* hapa ya *resources* za kifedha na *resources* za wataalam, wako sawa kuweza kufanya haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishuka sasa chini kwenye kutengeneza *contracts* kati ya huyu *private sector* na Serikali, pale inasema sasa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji. Mkanganyiko wa kwanza wakati tunauchambua huu Muswada kwenye Kamati tulikuwa tuna shida ya *definitions* za *Minister* na *Ministry,* tulikuwa tuna shida ya mkanganyiko wa *Minister responsible for finance, Minister responsible for investment* na *Minister responsible for PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Muswada huu *definition* ya kwanza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Naomba tu sekunde chache... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Janet Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza nianze kwa kuunga mkono sana Muswada huu ulioko mbele yetu na naipongeza sana Serikali kwa kuleta mapendekezo haya ya mabadiliko ya Sheria hii ya *PPP.* Kwa kweli hii ni sheria ambayo tumekuwa tukiisubiri muda mrefu; tumelalamika sana humu ndani kuzungumzia kwa nini *PPP?* Hatimaye Serikali imesikia na imekuja na mapendekezo ya kuboresha Muswada huu ili sasa uanze kutumika vizuri na kwa njia ambayo inategemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi vilevile kuwa kwa maana hii sasa Serikali imefungua milango zaidi kwa sekta binafsi na imeweka maeneo mbalimbali ambayo sekta binafsi inaweza ikaingia ubia na Serikali katika ngazi ya Serikali Kuu, TAMISEMI na katika sekta nyingine kama za mafuta na kadhalika. Nafikiri hilo ni jambo muhimu sana la kupongezwa, kwanza itatujengea uwezo mkubwa na italeta ufanisi mkubwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo ya nchi yetu na italeta ushiriki mkubwa zaidi wa wananchi kwa sababu tunaona sasa kuwa hata katika ngazi ya Halmashauri kutaweza kuwa na *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imepiga hatua kubwa sana kimaendeleo kwa maana ya *macroeconomic development,* lakini bado tuna masuala makubwa sana ya umaskini na haya yote najua yatakuwa *addressed* kama tutakuwa na *vibrant economy* katika *level* ya Halmashauri zetu. Najua kuwa na *PPP* kutasaidia sana kuweka huru fedha ambazo zilikuwa zinaingizwa na Serikali katika miradi mikubwa

mikubwa ambayo ni ya kibiashara zaidi na itawezesha Serikali sasa kuwekeza zaidi katika huduma za kijamii lakini ambazo pia zinaweza zikafanywa kwa kutumia ubia na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kwangu naona ni faraja kubwa na ninafikiri ni jambo la kuipongeza Serikali sana bila kuangalia historia. Kwa sababu nachoona ni kuwa Serikali imekuwa ikijenga kidogo kidogo uelewa, ufahamu na uwezo wake ku-*engage* na *private sector.* Kwa hiyo, siyo suala la kusema walikuwa wapi, kwa nini hawakufanya hivi, suala ni kuangalia kwa sasa hivi tunakwenda wapi na mwelekeo ni mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nianzie kwenye hili suala la *solicited and unsolicited proposals.* Kwa bahati nzuri safari hii Serikali imekuwa wazi zaidi juu ya *unsolicited proposals* kuwa itazikubali na imeweka na masharti. Siyo Serikali ya Tanzania peke yake inayofanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kidogo nisome kitu hapa nilichokitoa katika semina tuliyoipata hivi karibuni inayozungumzia masuala ya *unsolicited proposals. Unsolicited proposals* zinakubalika lakini kwa masharti, dunia nzima; hata *World Bank* wanasema wao hawaruhusu *unsolicited proposals unless* zinapitishwa katika *rigorous test. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubaya wa *unsolicited proposal* inaweza kuwa ni wazo zuri lakini ni wazo limeletwa na mtu mmoja au nchi moja kutaka kuingia ubia na nchi nyingine, lakini wewe unayeletewa hiyo *proposal* hukuitaka, hukuiitisha lakini ni mtu anakuja kuuza wazo lake kwako. Una kazi ya ziada ya kulifanyia tathmini wazo hilo ili uone kama kweli liko *feasible.* Hiyo moja kwa moja ni kazi na ni gharama kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia pia wazo hilo linaweza kuwa limekuja kwa njia ambayo siyo ya wazi

sana. Faida kubwa itakuwa ni ya yule aliyeleta *proposal* nchi mnaweza msifaidike, sasa hiyo ni lazima muifanyie kazi. Kwa hiyo, nimeshangaa kusikia mtu anasema hapa zile *proposals* mradi sisi hatutoi pesa yetu, basi tuziachie tu ziingie. Hakuna kitu kama hicho duniani, tutakaribisha vitu vya ajabu sana tusipoangalia ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mifano. Afrika Kusini pia hawa-*encourage* sana *unsolicited proposals* na zikija zinapitishwa katika tathmini kama vile ni *proposal* ambayo imekuwa *solicited* ili kuifikisha katika *level* moja; na je, ingekuwa sisi ndio tumependekeza kufanya mradi huu, tungeupitisha jinsi ulivyo? Kwa hiyo, ndugu zangu, nataka tuwe makini sana na hizi *unsolicited.* Nashukuru kuwa Serikali imekubali kuwa itaziangalia na imeona kuwa kuna maeneo mengine inawezekana zikahitajika kwa sababu pengine hakuna mtu mwingine anayeweza kufanya kazi hiyo, lakini hiyo haituondolei ule umuhimu wa kuziangalia kwa makini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kuwa kuna suala zima la *SMEs. SMEs* ni eneo lenye kuleta ajira nyingi sana kwa wananchi na kuongeza kipato kwa wananchi wengi sana na hasa zikifanywa kitaalam. Kama *PPP* itaruhusiwa katika maeneo haya, basi naamini Tanzania tutaona uchumi ukikua haraka sana kwa sababu wananchi wa kawaida katika biashara zao, makampuni au mashirika yao wanaweza sasa kuingia katika ubia na makampuni yanayotaka kufanya shughuli nao. Kwa mfano, kwenye kilimo, usindikaji, viwanda vidogo, teknolojia, masuala ya nishati na vitu mbalimbali ambavyo moja kwa moja vitafanya uchumi wetu ukue haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa sasa ni uwezeshwaji wa kutosha. Lazima wananchi wa ngazi hizo wafahamishwe kwanza maana nzima ya kuingia katika ubia wa namna hii, lakini waelezwe vilevile jinsi gani wao wenyewe wanatakiwa ku-*negotiate.* Wafundishwe vilevile njia bora za

kuendesha hii miradi. Kwa hiyo, nachoona hapa ni kitu ambacho ni kizuri sana kwa Tanzania na moja kwa moja najua kitaleta faida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ethiopia sasa hivi wanaongoza katika uchumi Afrika. Ukienda Addis Ababa sasa hivi ni kama kuna vurugu fulani hivi; huku kunajengwa barabara, huku kunajengwa *flyovers,* huku kunajengwa *EPZs,* huku kunajengwa *dams, all over the place* na vyote ni *PPP.* Ethiopia walikuwa nyuma hivi karibuni tu lakini sasa hivi wamefika mbali, wametumia mfumo huu wa *PPP* na umewaendeleza sana. Kwa hiyo, hata sisi hili jambo siyo geni wala halitakuwa baya kwetu, tujifunze tu jinsi gani ya kusimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla kengele haijalia, nataka sasa niombe rasmi miradi hii yote ya *PPP* kuanzia wakati tunazungumzia kutengeneza maandiko, tuzingatie masuala ya jinsia. Kuna wanawake wengi ambao ni wazalishaji, wafanyabiashara na wana makampuni ya kila aina, naomba wawezeshwe na wawekewe sehemu katika kila hatua ya hii miradi ya *PPP* na wao washiriki, kwa sababu wanaweza na tayari kuna *evidence* kubwa sana kuwa wanawake wengi sana wanashiriki katika masuala haya. Wawekeeni kitengo maalum cha kuwaelekeza jinsi gani ya kufanya haya mambo, nakuhakikishia utaona jinsi ambavyo uchumi utakua kwa ushiriki mkubwa wa wanawake katika masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala la *account.* Limezungumziwa suala la *account* lakini sikuelewa vizuri kama *account* iliyokuwa ikizungumzwa kuwa hela zitawekwa Benki Kuu ni zile tu za upande wa Serikali au ni pamoja na za wale wabia wa sekta binafsi? Kwa sekta binafsi naona inaweza ikawa shida. Kwa hiyo, hilo nafikiri liangaliwe vizuri zaidi, huwezi kuchukua hela za mtu binafsi ukamwingizia kwenye akaunti ya Benki Kuu bila yeye mwenyewe kuwa na ridhaa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbene, malizia kwa kuunga mkono basi.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niliunga mkono tangu mwanzo kabisa, ahsante.

MWENYEKITI: Unga mkono tena.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, tumeanza vizuri. Inaonesha jinsi mlivyo makini, mmesoma Muswada, mmeuelewa, yapo maeneo bado mnauliza, ndivyo inavyotakiwa iwe. Serikali itawapa tu maelezo ya kutosha. Naombeni muwe na hiyo *Schedule of Amendments,* itawasaidia sana katika kuchangia.

Wale wa mchana, niache tu kwa sababu nataka wote muwahi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na wachangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiliwa na Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia machache. Kwanza kabisa, nianze kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kuleta Muswada huu wa *PPP* ambao ni wa muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PPP* itasaidia sana katika kuinua maeneo kama manne. Eneo la kwanza ni kiuchumi, kwa sababu uchumi ukitaka kukua lazima nchi ishirikiane na *private sector*. Kwa sasa hivi naona Mheshimiwa Waziri ameamua jambo la msingi sana, nami sitaki nijikite sana kwenye sheria kwa sababu tulijadili vizuri sana kwenye Kamati, nami naunga mkono asilimia mia moja kwa yale majadiliano ambayo tulikuwa tumefanya kwenye Kamati. Ripoti ya Kamati imeeleza vizuri na hotuba ya Mheshimiwa Waziri imekaa vizuri na sasa hivi tuna matumaini makubwa sana kwamba *PPP* itasaidia sana kuinua uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba lazima sasa Serikali ijipange vizuri kuchagua ile miradi ambayo nchi inaweza ikaingia na *private sector* ambayo italeta manufaa.kuna miradi mikubwa sana na tunalenga kwamba *PPP* siyo kwamba itafanya kila mradi, lazima kuwe kuna miradi ile ambayo ni kipaumbele cha Taifa. Tuna miradi mingi sana, lakini lazima tuangalie ile miradi ambayo inaleta faida. Kwa mfano, tunaweza tukawa tuna wawekezaji wakajikita kwenye kilimo. Taifa zima hili linaweza likawa na wakulima kumi tu, wakaingia katika *PPP* na hao waka-*supply* chakula cha kutosha na Serikali ikatoa *support,* hii itatuletea manufaa sana kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ku-*supply* umeme kwenye vijiji vyetu; Serikali inafanya vizuri sana lakini ni mzigo mkubwa sana. Tukiingia na *private sector* waka-*supply* umeme kwenye nchi hii gharama za uzalishaji wa umeme badala ya Serikali kuingia sasa tutakuwa tumepunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kupunguza madeni makubwa ya kitaifa. *PPP* itapunguza deni badala ya kwenda kukopa na tunasema deni la Taifa linakua kila siku, sasa deni lile litapungua. Badala ya kukopa tujenge miundombinu ya umeme, kuna watu watajitokeza watafanya biashara. Kwa sababu *PPP* ni biashara, mtu atakuja hapa ili apate *profit* ila hawezi kupata faida bila kufanya miradi ambayo inaleta faida kwake. Siyo kwamba yule *private company* apate faida, cha kwanza tunaangalia Taifa letu linanufaika na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nimekifurahia sana ni kwamba itaandaliwa mikataba na wataalam. Hapo ndiyo mahali pa kuzingatia sana. Kwenye mikataba hapa huwa panakuwa na matatizo makubwa sana. Hii *PPP* inaweza ikatuletea faida kubwa au ikatuletea hasara kubwa, itategemea na mikataba itakavyokuwa imeandaliwa. Kwa mfano, sasa hivi nimeona kwenye mpango kwamba tutakuwa *PPP center* ambayo itakuwa inashughulikia sasa kufanya *analysis* ya mikataba yote na kwenye *PPP center* pale wataajiriwa wataalamu. Nimefurahi sana kwenye hotuba ya Waziri amesema kwamba wataandaa wataalamu halafu wataenda kusoma. Kwa hiyo Serikali itasomesha watu. Kweli pale wanatakiwa wataalam ambao wamebobea kwenye sheria na miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni muhimu sana na itasaidia kwa sababu tunaweza tukaingia kwenye *PPP,* kama hakuna wataalam wazuri tukaingia kwenye hasara kubwa sana kitu ambacho kitu hatukutegemea. Tukiwa na wataalam ambao wanafanya *analysis* ya *project* zote kubwa tutapata faida kubwa sana. *Advantage* moja ambayo ni kubwa ni kupunguza deni kubwa la Taifa. Kwa sababu ile miradi yote itajengwa na *private sector* ikishirikiana na Serikali. Hili litakuwa jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hata kijamii, kwa sababu watu wengi sana watapata ajira. Haya makampuni makubwa yatakayokuja kufanya kazi hapa

yatatoa ajira na watakaofanya kazi ni Watanzania. Kwa hiyo, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vilevile kwa mfano, miradi ya barabara, hizi *flyovers* na hapa Dodoma nadhani Serikali ina mpango wa kujenga *flyovers.* Ni jambo zuri sana, miji yote inayokua barabara za *flyovers* ni za muhimu sana, tukiingia kwenye *Public Private Partnership* itasaidia sana. Badala ya Serikali kupeleka hela nyingi basi zile hela inazi-*diverge* inapeleka kwenye mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine wanafikiri *PPP* itajihusisha hata kwenye miradi ile midogo midogo ambayo Serikali ingeweza kufanya kwa kushirikiana na wananchi wa kwa kawaida. Kuna mtu mmoja akawa ananiambia kwamba labda vyoo vya shule vimebomoka *PPP* itafanya siyo hivyo, watu wanatafsiri tofauti. Ni lazima iwe ni ile miradi mikubwa yenye kipaumbele cha Serikali ambayo italeta mafanikio makubwa kwa Taifa, hii itakuwa imesaidia sana. Tukisema *PPP* itasaidia hata ile miradi midogo midogo, sisi tukabweteka, tukasema kuna *PPP* tusifanye, itakuwa siyo sahihi. Lazima tuwe tuna *selective* ya miradi ambayo itatujengea sifa na Serikali itaondoa gharama za kuingiza fedha nyingi sana kwenye hiyo miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapata faida nyingi sana, hata ukienda kwenye utaalam, teknolojia sasa hivi inakua. Kwenye utaalam, wageni watakuja, wataleta ma-*expert,* kwa hiyo, unaweza ukaona wameleta hata mashine nyingine katika *production* ambazo sisi hatuzijui, vijana wetu watajifunza vitu vingi sana. Bahati nzuri hata kwenye viwanda, kuna mashine sasa hivi zinakuja mpya. Sasa ile itasaidia hata kutoa elimu kwa vijana wetu kwa *practical* ili waweze kumudu zile mashine ambazo zimetoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ushirikiano tu wa Kimataifa, nchi kama imeingia mikataba na nchi nyingine, kunakuwa na mahusiano, yale mahusiano yanajenga udugu.

Sasa hivi dunia imekuwa kama kijiji kimoja kwa sababu ya mawasiliano, watu wanatembeleana, wanafanya miradi pamoja, hii inasaidia sana. Tukijifungia hivi, tunasema wale wataalam wa nje wasije hapa tutafanya sisi wenyewe, kiteknolojia itakuwa bado hatujakua. Sasa hivi tutapanuka, kwa mfano, China wakileta miradi mikubwa hapa wakaajiri vijana wetu, watajifunza na tunakuwa na mahusiano mazuri ambayo yanajenga udugu katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, labda nisisitize tu kwamba lazima mikataba iangaliwe kwa makini sana. Ile *PPP center* ambayo itaundwa na Serikali lazima iangalie wataalam ambao watatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba tutakuwa na *Steering Committee* ambayo itapitia ule mchakato uliofanywa na *PPP Center* ili kumpelekea Mheshimiwa Waziri wafanya maamuzi na ile lazima iwe ya wataalam. Hata kama itakuwa ya viongozi wakubwa wamewekwa lazima wawe mtaalam wa kuangalia kwa sababu ile mchanganuo wa miradi ni wa kiufundi sana. Kwa hiyo, ni lazima wawepo wataalam ambao wanaweza wakaangalia vizuri kwamba miradi hii inaweza ikaleta manufaa kwa Taifa letu.

Mheshiimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Peter Msigwa, ajiandae.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Muswada huu naona kama umechelewa lakini ni muhimu sana. Kama tunavyosema, sekta binafsi ni

uti wa mgongo au injini ya maendeleo ya uchumi, basi Muswada huu unakuwa kama mafuta kwenye injini hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unafupisha muda wa kuangaliwa mradi ambao unatakiwa uwe wa *PPP.* Mradi huo unaopendekezwa sasa utapitia hatua nne tu badala ya hatua nyingi ambazo zilikuwepo kwenye sheria iliyopita au sheria inayorekebishwa leo. Mradi huu unaandaliwa na aidha Idara ya Serikali, Wizara au TAMISEMI unapelekwa sasa kwenye kituo cha ubia yaani *PPP Center,* pia mradi huu utapelekwa sasa kwenye Kamati uidhinishaji baada ya kuangaliwa pale chini, juu yake uidhinishaji na baadaye kwa Waziri wa Fedha na mradi pale unakuwa umetekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni njia ya mkato sana na njia ambayo itaeleweka kwa watu wote wanaotaka kuwekeza. Hapo zamani kwenye sheria iliyopo, haikuwa inajulikana mradi utauanzisha upeleke wapi yaani umeanzisha mwenyewe binafsi au Serikali imeuanzisha, hujui yule mbia wa sekta binafsi ataingilia wapi, lakini hata akiiingia itakuwaje baadaye? Tafsiri ya marekebisho haya yanaweka njia bayana kwa watu wote wawili yule wa sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu pia unayo malengo mazuri sana na kwanza ni kuweka masharti kwamba taarifa sasa ziripotiwe kila nusu mwaka yaani *compliance* ya *reporting* kutoka wanaotekeleza mradi. Vilevile marekebisho haya yanaruhusu miradi midogo midogo. Zamani ilikuwa ni vigumu sana mradi mdogo unatupiwa usoni, haufai kabisa, ilikuwa inachukuliwa miradi mikubwa ambayo ilionekana kwamba Serikali inaipenda, lakini pia itakuwa na faida kubwa badala ya miradi midogo ambao wananchi wa Tanzania tulikuwa hatuwezi kushirikiana nao. Sasa kwa kuweka nafasi ya miradi midogo midogo tutaruhusiwa pia watu binafsi kushirikiana na Serikali au sekta za umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti imependekeza mambo fulani muhimu sana. La kwanza, inasema kuwepo na mfuko wa uwezeshaji wa miradi ya *PPP.* Hili halikuwepo huku mwanzoni. Vilevile imependekeza uazishwaji wa benki ambayo itasimamia au itatoa mikopo kwa ajili ya miradi hii ya *PPP* kwa sababu benki za biashara haziwezi kukopesha miradi ya *PPP* ambayo inachukua muda mrefu kuanza kupata faida na benki zinataka kupata faida hiyo haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imependekeza pia mafunzo kwa watu watakaoandika mikata hii. Tumeshuhudia mikataba mingi mibovu imetutia hasara nchi yetu, hatutaki tena kuanza na bahati mbaya ya kubahatisha. Tunataka miradi iandikwe vizuri mikataba yake kusiwe na migongano huko baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea hali halisi ilivyokuwa huko nyuma. Nina mifano ya miradi ambayo ilianzishwa kwa nia nzuri kabisa iwe *PPP*. Kwa kuchelesha miaka mitano au sita Serikali ikapata hasara ya mabilioni. Mradi mmojawapo ni wa daraja Kigamboni. *NSSF* walipoanzisha daraja lile na kuomba tuwe *PPP* na Serikali, na wale ambao, naomba radhi nilikuwa na *conflict of interest,* nilikuwa Mwenyekiti wa Waajiri Tanzania na nilikuwa mdau kwenye daraja lile, Serikali ilijivuta miguu mpaka wafadhili waliokuwepo wakajitoa na baadaye *NSSF* ikatumia nguvu yake kubwa kujenga daraja lile kwa hasara. Bei tuliyopewa mara ya kwanza na mjengaji wa daraja lile ikawa imezidi kwa karibu shilingi bilioni 10, hiyo ni hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ambao umeshindwa kutekelezeka kabisa ulikuwa *NSSF* ingejenga *line* sita za barabara kutoka Chalinze kwenda Dar es Salaam. Tumeandaa upembuzi yakinifu na wataalamu wetu tukaiomba Serikali, Serikali ikasema itangaze mradi ile halafu na wengine wagombee kwa kutumia *document* ambayo sisi tumeiandaa, tukabaki nyuma. Matokeo yake mradi ule

haujatekelezwa mpaka leo. Sasa Serikali inajaribu kuutekeleza pamoja na *NSSF* lakini kwa hasara kubwa kwa sababu bei miaka kumi iliyopita na leo ni tofauti sana. Hii ni mifano ya miradi ambayo Marekebisho ya Sheria ya *PPP* inajaribu kuondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine mkubwa ambao ulishindikana ni wa kujenga Ubalozi wetu huko Nairobi. *NSSF* walitaka pia kujenga Ubalozi wa Nairobi kama mtakumbuka, wakati Mheshimiwa Rais wetu alipopewa hati ya kiwanja kule Nairobi, nasi tuliwapa hati ya kiwanja cha Dar es Salaam. Wenzetu wa Kenya wameshajenga nyumba yao, sasa wanafanya ukarabati sisi kiwanja kinagombewa Nairobi, kwa sababu tunavutana, *PPP* ilikuwa haieleweki. Sasa baada ya marekebisho haya kupita tunajua hatua ya kwanza ni upembuzi, hatua ya pili ni kupokea mradi, utatoka hapo mpaka hatua nne, tunajua mradi unashindikana au unakubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuchangia hayo kwamba sasa marekebisho haya ni kama yamechelewa, lakini tushukuru Mungu yamekuja na tuyapitishie ili yatusaidie. Kama tunavyojua sekta binafsi ndiyo uti wa mgongo wa uchumi, lakini pia ndiyo injini ya uchumi kwa kuunganisha na Serikali tutakwenda mbele haraka na uchumi wetu utakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu sana wa kuleta na kurekebisha baadhi ya vifungu katika Sheria hii ya Ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi faida zilizoko katika kutekeleza haya marekebisho ni nyingi sana tofauti na vile

ambavyo tunafikiria. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaona kwamba tumechelewa au tunabadilisha sera mara kwa mara lakini naomba nigusie maeneo machache kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kuwa na *PPP*, kwanza tunakaribisha mitaji na tukikaribisha mitaji tunaiwezesha Serikali kujikita kwenye maeneo mengine ambayo zaidi yanakuwa ni ya huduma za jamii. Kwa hiyo, kwenye miradi ile ya kimkakati ambayo ni ya kibiashara tutaweza kuisaidia Serikali kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kurekebisha maeneo mbalimbali kwa mfano kwenye kuondoa baadhi ya taratibu na kumpa Waziri mwenye dhamana tumepunguza urasimu. Suala la Waziri kutekeleza moja kwa moja baadhi ya masuala, tunapunguza urasimu. Kwa mfano, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema mlolongo mrefu wa michakato ya uidhinishaji wa miradi ya ubia ambao unaathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa miradi ya *PPP,* maana yake tunapunguza *bureaucracy.* Ukishaondoa *bureaucracy* tutaendana na muda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo ambavyo tayari vimewekwa vitatusaidia sana. Kwa mfano, mijadala ambayo inaendelea ili kutengeneza eneo hilo la miradi mbalimbali kama Liganga na Mchuchuma na *LNG* ya Lindi, tukiweka maeneo haya na kwa kufuata hii sheria tutanufaika kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, marekebisho haya ya vipengele mbalimbali tutakaribisha zaidi wawekezaji na kwa namna nyingine tutaleta uzoefu ambao umetumika maeneo mengine na pia tutaleta teknolojia. Kwa hiyo, tutakuwa na *technology transfer* maana wataalam wa kampuni ambayo inaingia ubia na Serikali wataleta teknolojia ambayo vijana wetu na watumishi wetu watajifunza na tutaweza kui-*capture* kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo pia na maboresho haya niombe sasa kuna kipengele cha Waziri kwamba kwa vile viwango vidogo katika hii miradi *(Small Scale PPP Project)* kwamba Waziri kwa kutumia Maafisa wake Masuuli anaweza akaidhinisha moja kwa moja. Basi tuombe tupate ufafanuzi aidha kama kutakuwa na mwongozo wa kanuni miradi hii midogo ni ya kiwango gani, labda kama katika kiasi cha shilingi au dola ambayo sasa Waziri ataweza kuiidhinisha moja kwa moja bila kupitia kwenye *Steering Committee,* kwa hiyo hiyo tutaomba tupate ufafanuzi wa Serikali katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya ya *PPP* yamepelekea kufanya na mabadiliko ya sheria nyingine kwa mfano Sheria ya Mafuta. Kimsingi katika Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, *National Oil Company* ambayo ndiyo kwa sasa ni *TPDC* inatakiwa ifanye uwekezaji usiopungua asilimia 25 kwa kupata wabia kama hivi. Kwa hiyo, kwa marekebisho haya sasa itaenda kurahisisha katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji na tumeona *TPDC* ina nia ya kusambaza gesi asilia katika majumba na wameanza *Pilot study* upande wa Mikocheni kule Dar es Salaam, hivyo hii itasaidia. Kwahiyo hizi zote *consequential amendments* za Sheria Mbalimbali tunatumainia sasa itaondoa vikwazo na watu kwenye kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Wajumbe wamechangia kwamba Serikali imekuwa ikiwatenga Sekta Binafsi. Hii tunaona siyo kweli kwa sababu kwenye hotuba ya Waziri ameeleza kwamba utekelezaji wa *PPP* umekwishaanza na wengi tumepanda yale mabasi ya mwendokasi, tukiona ile *DART* tayari tunaona ni utekelezaji upande wa *TPDC, CBE* Serikali imeeleza kwamba maeneo hayo inakwenda kuingia kwenye ubia.

Kimsingi siyo kila eneo au aina ya sekta unaweza ukaachia sekta binafsi ifanye. Kwa mfano, masuala mazima ya kiusalama au ya kiafya huwezi ukaachia sekta binafsi. Kwa hiyo, lazima tuzingatie usalama wa nchi na mali zake pamoja na watu wake, kila jambo huwezi ukaachia sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima tuangalie na mazingira ya kuharakisha maendeleo. Kama vile *SGR* tumeanza kwa fedha zetu za ndani likiwa ni lengo kubwa la kuharakisha miradi hii ili tuweze kuitekeleza kuliko kukaa kwenye masharti ambayo yanakuwa hayana tija kwa upande wa wananchi na Serikali kiujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba pia tupate ufafanuzi mzuri, tumeona Waziri mwenye dhamana atasimamia sera, sheria na kanuni kwenye masuala ya *PPP.* Sasa ule ushauri mwingine kama inaweza ikatengenezwa, pia ile *Steering Committee* inaweza ikampa ushauri Waziri katika masuala ya *PPP* hiyo *collaboration* basi kama kuna mahali tume-*over look* basi tutaomba mhusika Waziri mwenye dhamana aweze kutuelezea namna gani tutakuwa na *collaboration* kati ya *Steering Committee* pamoja na Waziri mwenye dhamana ambae anasimamia sera, sheria na kanuni kwenye masuala ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tumeliona katika namna ya kuingia kwenye hii miradi ili tuweze kupata tija zaidi kama kwenye kanuni tuone aina ya uwekezaji na muda ambao mtu ataweza kupata fidia ya uwekezaji alioupata tunapokuwa na *amortisation of investment.* Hebu tuwe na muda ambao utakuwa ni *win win* situation ili kila mtu ambae amewekeza pale nchi ifaidike na yule ambaye anaewekeza nae aweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kitu kikubwa cha kuzingatia tunavyokuwa kwenye *PPP* tuangalie sana masuala ya thamani ya mradi maana tumekuwa na changamoto, baadhi ya watu wanaleta thamani ya juu zaidi tofauti na uhalisia na bei za soko. Yote hiyo ni katika kulenga kujinufaisha yeye mwenyewe ambae amekuja atachukua kingi kuliko kile ambacho sisi tutakuwa tumekilengea. Kwa hiyo, *value for money* tunatakiwa tuzingatie zaidi, tumekuwa na *cases* zaidi, kwa mfano kwenye miradi ya uchimbaji wa madini...

MWENYEKITI: Muda umekwisha Mheshimiwa Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab ajiandae.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kwa utangulizi kabisa kama Wabunge na kama Taifa tunapaswa tukumbuke usemi huu; *"the past is where we have learned the lesson and the future is where we apply the lesson."* Kwenye masuala haya mengi ya mikataba kuna mambo mengi ambayo tumejifunza huko nyuma, ni wajibu wetu baada ya Serikali kuleta muswada huu wote kwa pamoja tungeangalia ni namna gani huko nyuma tumepata masomo ambayo sasa tunapokwenda kuandika miswada mingine inayoletwa kama hii tu-*apply* yale masomo tuliyojifunza.

Kabla sijaendelea ninaunga mkono kwa dhati kabisa hotuba ya Kambi ya Upinzani na mambo mengi ambayo Mheshimiwa Halima ameyazungumza kwenye hotuba na ninaamini Mheshimiwa Mpango atakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo napenda kujiuliza ni kwamba tunapoleta sheria hapa ndani ya Bunge huwa kunakuwa na jambo ambalo tunataka kulitatua, tunataka ku-*solve* nini? Tumekuwa na matatizo gani? Sheria iliyokuwepo ilikuwa na shida gani? Ni kwa nini tunaleta *amendments?* Ni lazima tuwe na majibu hayo kwamba tunataka tutatue nini. Hakuna anayepinga hapa kwamba tunahitaji *PPP,* lakini naiomba Serikali haijatoa *clear definition* ni uchumi wa aina gani tunaotaka kuuendesha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka Awamu ya Kwanza Mwalimu Nyerere ali-*define* ni aina gani ya uchumi, lakini

baada ya Mwalimu Nyerere kushindana na Ndugu Edwin Mtei akaamua kung'atuka, mfumo wa uchumi ukabadilika. Tungependa Awamu ya Tano ituambie ni aina gani ya mfumo wa uchumi inayotaka kutupeleka kama Taifa. Kwa sasa hivi tukiwa wakweli tukianza kuangalia ni kama chombo, ni kama *space ship* ambayo ipo angani haijui inataka kutua wapi, kwa sababu mnatuambia uchumi wa viwanda, mnatuambia *PPP* lakini mambo mnayoyafanya na mnayotuletea hapa hayaendani na *PPP.*

Mheshimiwa Mpango *investors* wote wanapotaka ku-*invest,* wanapokuja katika nchi yoyote huwa wanazingatia vitu vitatu vya msingi na ninaomba utanichambua hapa au utanipinga kama nasema uongo, najua wewe unayajua haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza wanachoangalia ni *contract sanctity. Sanctity* yaani utakatifu, utukufu wa huo mkataba mnaokubali. Wanataka waone ni namna gani hii nchi inaheshimu mikataba tunayokubaliana ili wawe na uhakika wanapokuja kwenye nchi. Neno *sanctity* linatokana na *Latin word,* kitu *holy* (kitakatifu). Kama Taifa lazima tujiulize huwa tunaona mikataba tunayoingia na watu wengine au tunaamua kuivunja kwa vile tunavyotaka? Sasa tunapotengeneza hizi Katiba lazima tujiulize ni kweli huwa tunaona hiyo mikataba ambayo tunafanya au tunafanya kisiasa? Hakuna *investor* yoyote ambae atakuja mahali ambapo hatuheshimu mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati wa makinikia ambayo sasa hivi mmeingia, mmejificha uvunguni Mheshimiwa Lissu alizungumza hapa, alisema *report* ya Osoro ni *rubbish.* Watu walimrushia maneno mengi hapa, mkatangaza kwenye vyombo vya redio, kukawa na kelele nyingi na ngoma nyingi, mkasema tutapata karibu trilioni 425 ziko wapi mpaka leo? Mkavunja mikataba bila utaratibu, bila kuheshimu mikataba tuliyoifanya ambao ni sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima Mdee amezungumza asubuhi hapa, amesema tatizo letu hatuwezi

kuwalaumu hawa wanaokuja humu ndani, ni namna tunavyoandika mikataba wenyewe, halafu tukiandika mikataba tunaanza kuwalaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo *investors* wanaheshimu ni *regulatory framework (clarity),* mfumo mahsusi wa kudhibiti makubaliano ambao bado katika nchi yetu hatufuati hayo mambo, kila mtu anaamua. Mwingine amezungumza hapa asubuhi, anavyo-*behave* Mkuu wa Mkoa wa Simiyu ni tofauti kabisa anavyo-*behave* Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Ni *investor* gani atakayekuja katika nchi kila mtu anatoa matamko yake? Mkuu wa Wilaya anataka achukue kodi, anataka adai kodi, sasa ni *investor* gani atakayekuja atasikiliza mambo kama hayo? Tuna ukosefu mkubwa wa *clarity,* ni namna gani hii mifumo tunaisimamia kama Taifa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni *international arbitration,* ambayo nimeshangaa sana kwenye muswada wako Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango unasema kwamba, unatoa wazo kwamba eti kama ikitokea kutokuelewana basi mahakama zetu ndiyo ziamue. Nikuulize swali Tanzania ni *member* wa *MIGA,* inawezekanaje *member* wa *MIGA* tuwaambie hao *investors* wanaokuja katika nchi yetu waje wafanyie kesi zao kwenye mahakama zetu? Nitaomba uje unijibu hili swali rahisi kabisa, inawezekanaje *member* wa *MIGA* au tumejitoa kwenye *MIGA?* Wanawezaje kuja sasa, unawaambia *investors* ambao wanaleta pesa zao kwa *risk* kubwa halafu unasema tufanye kwenye mahakama zetu! Kwa bahati na Mahakama zetu hizi ambazo mtu anakaa ofisini anapiga simu kwamba funga akina Msigwa miaka mitano, nani atakubali kuleta mitaji yake? Mahakimu na Majaji wanapigiwa simu funga huyo miaka mitano uhakikishe anafungwa Sugu ndani, nani atakuja kwenye mahakama za namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia kwenye Mahakama hizo anaambiwa Jaji Mkuu kwamba hizi kesi zikiisha nitawapa bilioni kadhaa, nani ata-*trust* mahakama za namna hiyo halafu ulete *investment* hapa? Ukiangalia *spirit*

ya Wabunge wengi humu wananong'ona wengine hawataki kusema, *actually* wanaishangaa hata Kamati kuuleta huu Muswada humu ndani, kwa sababu huu Muswada unaua *PPP* na mtuambie kabisa kwamba hamna mpango wa *PPP.* Serikali ya Awamu ya Tano ilitengeneza mazingira mazuri. Mfano mzuri, baada ya ile Sheria ya Rasilimali zetu mambo ya gesi...

MWENYEKITI: Kengele ya pili.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unanitoa kwenye reli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ile Sheria ya Rasilimali ambayo tuliileta hapa tulianza kubadilisha sheria za mchezo katikati ya *game.* Makampuni makubwa, kwa mfano, *Exxon Mobil* iliondoka. Wote mnajua kwamba mojawapo ya watu wa ile Kampuni ni Rex Tillerson huyu aliyekuwa *State Secretary* wa Marekani maana yake mnadhani amepeleka meseji gani kule Marekani kwa ajili ya *investors?* Utasema hao ni Wamarekani, makampuni ya Norway yameondoka, makampuni ya Brazil yameondoka, sasa hao *investors* mnaosema waje wanatoka wapi? Tunapeleka picha gani huko ulimwenguni tunaposema tunaleta hao *investors,* wako wapi? Tunaongea lugha nyingine na tunatekeleza kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo kama Bunge tunatakiwa tujadiliane. Mambo mengi hapa tumeyazungumza wakati mwingine tunatolewa kwa kushikwa na maaskari, vigelegele vinapigwa, mwisho wa siku muda ukifika tunaanza kutoana macho, tunaanza kuoneana aibu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wetu kama Bunge, mimi ningesema, ningekuwa ni Mjumbe wa Kamati ningelazimisha hii sheria irudi kwa sababu kimsingi sheria iliyokuwepo nyuma ni bora zaidi kuliko hii. Kwa hiyo, kwa kifupi, Serikali ya Awamu ya Tano inaturudisha kwenye enzi za ujamaa na kujitegemea, enzi za Awamu ya Kwanza

ambayo mfumo wa ujengaji wa uchumi ulishindwa, sasa mnataka turudi tena kule kwa kisingizo cha Ujamaa kwamba tunapenda watu wakati hatuwezi kuwaajiri tunapoua sekta binafsi, hatuwezi kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani nimezungumza sana kuhusu *Economic Diplomacy* lakini huoni hizi sheria zinaonesha *Economic Diplomacy,* hauzioni *Economic Diplomacy* katika masuala haya. Sasa mnawezaje kutunga sheria ambazo *actually* zinawafukuza *investors?* Ningeomba kama Bunge tuwatendee haki wananchi, kwa sababu mwisho wa siku mtumbwi huu ukitoboka sote tutashuka chini, tutatumbukia wote kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *amendments* zako ulizozileta siungi mkono hoja kwa sababu zinaua *PPP,* hazitatusaidia na Serikali hamtaweza kufanya biashara. Tumetoka huko hata maandazi Serikali ilikuwa inauza, ilishindikana! Tulikuwa tunapanga foleni kwenye maduka ya *RTC,* foleni imeshindikana. Niambieni jambo moja ambalo mmelilete hapa Awamu ya Tano, mmesema mnajali wanyonge, yote yamegota ukuta, lakini mkija hapa wengine mpaka sasa hivi wame-*back off* hawataki kuzungumza lakini huu ndiyo ukweli kwa sababu tunaua sekta binafsi kushirikiana na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza dada yangu hapa kwenye eneo la *unsolicited,* nalichukulia kama mchonga kinyago, *whatever you got the message.* Mimi nalichukulia kama mchonga kinyago. Mchonga kinyago akiliona gogo, wewe unaliona gogo yeye anaona sura ya kinyago, sasa amekuja hapa yeye ameona kinyago, ameona *potential* wewe hujaona, anakuja na hela zake, anataka kufanya *investment* wewe bado unambana, unamsumbua halafu aziweke pesa Benki Kuu, kwa misingi gani, nani ateleta hela zake aweke hapa, mtampata wapi mtu wa namna hiyo? Halafu ni nchi gani inayo *practice* haya mambo mnayoyafanya. Mtupe mfano mmoja ni nchi gani ina-*practice* hayo mabo mnayoyafanya ambayo mnaamua kujifanyia

mnavyotaka *as if investment* inatakiwa iwekwe tu Tanzania. Hawa ma-*investors* tunawagombania, tunawakata waje lakini mnafanya mambo kwa mashinikizo...

MWENYEKITI: Haya muda wako ndiyo huo. Unga basi mkono hoja. Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza jana wakati naandaa hii hotuba nilimsikia Profesa Kabudi akifanya upotoshaji wa kiwango kikubwa na ningependa niweke mambo *clear* kwa ajili ya *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kuna wanasheria wengi tulichangia humu ikaonekana kwamba wengine tukaambiwa kwamba *marks* zetu itabidi zifukuliwe lakini mimi niseme hivi, Kabudi alinifundisha *Family Law* (Sheria ya Familia), *Constitutional Law* nilifundishwa na Profesa Mwinuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kulikuwa kuna upotoshwaji ionekane kwamba Taifa hili kuna *total separation of power.* Tunafahamu kuna mihimili Mitatu. Kuna mhimili wa Bunge unaotunga sheria, kuna mhimili wa *Executive* unao-*enforce* sheria, kuna mhimili wa *Judiciary* unao-*interprete* sheria. Kwa mfumo wetu Tanzania hii mihimili inaingiliana na hii mihimili inachekiana kuna *(checks and balance)* ndiyo maana leo unakuta tuna Mawaziri ni sehemu ya Bunge, ndiyo maana leo unakuta tuna Rais anachangua Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri kusimama na kusema kwenye Serikali kuna Mawaziri watatu tu na kwamba eti fedha ambazo tunazitoa kwa mhimili wa *Judiciary* kama Bunge hatuwezi kuhoji wakati *CAG* anakagua kila hesabu na Bunge tunachambua kila kinachoandikwa na *CAG* na ku-*recommend.* Kwa hiyo, namshauri Profesa Kabudi akasome vizuri Katiba, ajue *separation of powers* zinafanyikaje katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, lakini pili, siyo kwa umuhimu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa unaonaje ukijielekeza kwenye muswada sasa?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekea, naweka mambo sawa kwenye *Hansard*. Jambo la pili...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Si muda wake?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine tumekuwa Mawakili kwa kufanya *Bar Exam.*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hebu naomba utulivu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Profesa Kabudi anajua yeye ameupata uwakili kwa *style* gani kwahiyo tusidhalilishane hapa wakati tunaishi kwenye nyumba za vioo. Nimeongea kulinda heshima ya wanasheria wa jana ambao tulisemwa semwa kiujumla. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Jielekeze kwenye hoja sasa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija hoja ya pili sasa kwenye muswada, nitaanzia pale ambapo Mheshimiwa Msigwa ameishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 11 kuhusiana na utatuzi wa migogoro. Tunasema kwa nia njema kabisa, na tunasema kwa nia njema. *As long as* sheria yetu ya *PPP* inakaribisha na inatambua kutakuweko na wawekezaji wa ndani na kutakuwepo wawekezaji wa nje, lazima hii sheria tuifanyie maboresho ili tuweze ku-*accommodate* hayo makundi mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna anayepinga kwamba *option* mojawapo ya kutatua hiyo migogoro iwe kutumia mifumo yetu ya *arbitration* ya ndani, hakuna anayepinga. Sambamba na hilo lazima kuwe na *option* kuwe na *option* ya hizi sheria zingine ambazo Mheshimiwa Chenge

ulikuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tanzania kama nchi hatuishi *in isolation*, kama nchi tumesaini mikataba ya kimataifa, kama nchi tumesaini *multilateral* na *bilateral agreements* na baadhi ya nchi kuhusiana na masuala ya wawekezaji na nitatoa baadhi ya mifano michache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Tanzania ni wanachama wa *International Centre for Settlement of Investment Dispute,* chombo hiki kinakuwa *funded* na *UN* ama kwa lugha nyingine tunaita *ICSID*. Katika mfumo wetu wa *arbitration* tuna maeneo ambayo tuna *arbitration* na *multilateral agreement* katika *investment protection* kati ya nchi na nchi. Sisi ni wanachama wa *MIGA* amezungumza Mheshimiwa Msigwa hapa. Sisi ni *signatory to the New York Convention on the Recognition and Enforcement of Arbitration Awards*. Kwa hiyo, katika mazingira kama haya ambayo Taifa letu linataka kukaribisha wawekezaji *serious,* kwa sababu hapa hatuzungumzii wawekezaji uchwara. Tunazungumzia wawekezaji *serious* ambaye anataka akija anakuta kuna *neutral ground* kwamba yeye atakuwa salama, lakini vilevile na mbia atakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mahakama yetu kwa mfano, Majaji wanateuliwa na Rais, Rais wetu ndiyo Magufuli huyu! *Chief Justice* anateuliwa na Rais, Rais wetu ndiyo Magufuli, *Principal Judge* anateuliwa na Rais, Rais wetu ndiyo Magufuli, halafu hawa watu ndiyo wanatakiwa wawe wanashusha maelekezo ama kutengeneza *regulations* mbalimbali za mifumo uendeshaji za mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia njema tunaipenda nchi ndiyo, lakini lazima tuwe *realistic* hatuishi kwenye kisiwa. Mwanasheria Mkuu wa Serikali *of all people* unatakiwa umsaidie Rais, Mheshimiwa Kabudi mwalimu wangu wa *Family Law* alitakiwa amsaidie Rais, sasa bahati mbaya na yeye anakuwa sehemu ya upotoshaji. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, kwa heshima zote naomba hata unapomtaja, unatumia *title* yake humu, ni Mheshimiwa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria sasa hivi, ni mwalimu wangu mzuri kweli wa *Family Law*, hawa wanamsaidia kumshauri Rais kwa kiwango gani, kama tumezidiwa tuna watalaam wengi wa sheria ndani ya Serikali tusaidie tujenge nchi hii. Ninachotaka kusema hatuishi na *in isolation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu ikaeleweka vilevile Mheshimiwa Mpango najua una uchungu sana na nchi hii na una uzalendo na ile uliyoipiga Dar es Salaam nilikukubali, ulivyomshughulikia dogo kule Dar es Salaam safi. Ni muhimu ukajua kwamba mgogoro wa *TANESCO* na *Standard Charted* hauna uhusiano wowote na *ICSID* wala *MIGA*. Mgogoro wa *Bombardier* ilitaka kushikiliwa juzi kwa mkataba ambao Rais alivyokuwa Waziri wa Miundombinu aliuvunja kienyeji kampuni ikaenda huko ikafungua mashitaka ikashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa *ACACIA* mnabisha hapa, sisi tupo *ACACIA* anaenda kule na atatuchapa, mtatuambia sisi siyo wazalendo kumbe ninyi ndiyo ambao siyo wazalendo mmeingiza nchi kwenye shida na hamtaki kukubali ukweli. Kwa dhamira njema sawa, mfumo wa *arbitration* ndani ya nchi yetu upo tuuweke, lakini tuweke mifumo mingine tupate wawekezaji mahiri watakaoisaidia nchi, huu uzuri wote ama baadhi ya uzuri robo tatu ama nusu ya hii sheria unavurugwa na hiki kipengele, hiki kipengele ndiyo kinafanya huu muswada unakuwa ni wa hovyo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nilitaka Waziri wa Fedha anisaidie kwenye madhumuni tunaambiwa kwamba muswada huu unapendekeza kwa ajili ya kuwezesha Waziri wa Fedha kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za ubia. Mapendekezo ya marekebisho yanakusudia kurekebisha mfumo wa kitaasisi na kisheria katika usimamizi wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Ukienda kwenye madhumuni Waziri unatajwa, ukija huko kwenye vifungu vingine vya sheria

haupo. Sasa huyu Waziri ambaye kwa tafsiri tunaambiwa anahusika na masuala ya *PPP* hii Wizara ambayo kwa tafsiri tunaambiwa anahusika na masuala ya *PPP* mbona haipo kwenye sheria, lakini kwenye madhumuni ipo, kitu gani kinafichwa? Isije baadae tukaletewa sheria tunaambiwa Waziri wenye dhamana ya TAMISEMI bwana mkubwa mwenyewe namba moja, ndiyo atakuwa ana dhamana ya *PPP*. *(Makofi/Kicheko)*

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64 (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchangiaji ambaye alikuwa anaendelea hapa, huko alikokuwa anatupeleka alikuwa anataka kutupeleka kuvunja Kanuni ya 64(1)(d) na Kanuni ya 64(1)(e). Kama ni hoja mahsusi ingekuwa ni hoja inayohusiana na jambo mahsusi linalohusu Wizara anayeiongoza Wizara ya TAMISEMI. Ukienda kwenye Kanuni ya (d) huwezi ukalitumia jina la Rais katika kujenga hoja ndani ya Bunge kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamini jambo ambalo halina msingi katika uhalisia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mchangiaji kwa dhahiri kabisa alikuwa anataka tu kutumia jina la Rais kulishawishi Bunge hili kufanya maamuzi ambayo si sahihi kabisa na kutupeleka kwenye mjadala ambao kwa kweli hauendani na utaratibu wa kikanuni ambao tunao. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kabisa jambo hili ni muhimu likazingatiwa wakati tunachangia mjadala katika Bunge lako tukufu.

MWENYEKITI: Ahsante, bahati nzuri hana muda tena muda wake umekwisha, lakini alikuwa anaenda kusiko, nadhani mtasaidiwa tu baadae ili msirudie rudie hii *point,* Waziri ni nani? Muswada huu umeandikwa kwa namna ambayo inafanya iwe *neutral*, neno la Waziri kwa sababu anayegawa majukumu haya yaende wapi ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ili kuhakikisha kwamba huko siku za usoni hapatakuwa na mkanganyiko akiamua kuihamisha *portfolio* hiyo, sasa iko Wizara ya Fedha kwa hiyo sasa hivi mwenye *portfolio* hiyo ni Waziri wa Fedha akiamua mwenye mamlaka kuipeleka mahali pengine, huyo ndiye atakuwa ndie Waziri anayehusika na *PPP*, hatutahiji kurejea Bungeni kurekebisha sharia, kwa hiyo mchangie mkijua kwamba Waziri anatajwa na Wizara inatajwa, tunaendelea. Utajifunza tu Mheshimiwa.

Mheshimiwa Balozi Adadi atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa kunipa hii na mimi kuchangia muswada huu ambao ni muhimu sana. Muswada wa marekebisho ya sheria ya Ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu ni muhimu na naona kama umechelewa sana, umuhimu wake unajidhihirisha na miradi ambayo kama tunayo hapa nchini ya ubia wa *PPP* na sekta ya umma. Kama miradi hiyo ipo basi ni michache sana, ndiyo maana marekebisho haya naamini yamekuja ili kuweza ku-*facilitate* kuweza kupata wawekezaji ambao tunaweza kuingia nao ubia na tuweze kuwa na miradi kama hii. Miradi ambayo ipo hapa ni michache sana na mfano ambao unaweza kuutolea siuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mradi wa *DART* wa mabasi upo, lakini ukiangalia Mradi wa Daraja la Kigamboni upo, lakini utaona kwamba imekwenda kwenye sekta ya umma kwa sekta ya umma. Ni muhimu sana

marekebisho haya yameletwa kwa wakati muafaka ili kuweza kuangalia namna gani ambavyo tunavyoweza kuleta wawekezaji waweze kuingia kwenye miradi mikubwa na midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bara la Afrika tu, kwa sababu miradi kama hii iko kote duniani. Nilikuwa nasoma juzi Marekani wana miradi ya *PPP* mingi sana, Ulaya mingi sana na kama hapa Afrika, *South Africa* ndiyo ambayo inaongoza kuwa na miradi mingi na ambayo imekuwa *successful*. Kule wana miradi zaidi ya 400 mikubwa na hii midogo midogo hii kwenye *provinces* zao ambazo ni kama Halmashauri za kwetu hapa. Ukiangalia mikubwa iko zaidi ya 100, kwa hiyo ni nchi ambayo utakuta kwamba wanafanya vizuri sana kwenye mambo haya ya miradi ya *PPP,* ndiyo maana naona kwamba ni muhimu na hata watalaam wetu waende kujifunza *South Africa,* waende kujifunza Mauritius ili waweze kuona namna gani ambavyo miradi kama hii inaweza kufanyika kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi kama hii ambayo imefanikiwa hasa ni kwenye mambo ya *transportation, road tolls*, unakuta ni mingi sana na *telecommunication* na *electricity,* lakini miradi kama ya maji kwenye mambo kama haya imekuwa na bahati mbaya kuweza kufanikiwa. Sasa ni vizuri kwamba, sasa hivi miradi hii na *amendments* hizi zimekuja mpaka miradi mingine ambayo ni midogo kuanzia karibu, unaweza ukatoka *zero* mpaka kwenye milioni 20; kwa hiyo ni vizuri hata Halmashauri zetu zinaweza kuanza kufanya mazungumzo na kuanza kuingia kwenye miradi kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye marekebisho ya sheria utaona kwamba kuanzia kwenye kifungu cha pili mpaka kifungu cha 7C yote hii imezungumzia namna gani ya kuweza ku-*facilitate* miradi hii iweze kufanyika na kuondoa urasimu ambao unaweza kuwa pale na kuleta matatizo. Nimeweza kuleta kitengo maalum ambacho kitaweza kushughulikia *PPP*, kitengo hiki kimetoka kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu ambacho ilikuwa *very dormant* sasa hivi iko pale kwa

Waziri wa Fedha ambayo tunaamini ya kwamba itafanya kazi nzuri sana chini ya Mheshimiwa Waziri, imeondoa urasimu na imejaribu kuweka uwazi kwenye zabuni ili kuweza kuona kwamba zabuni zinafanyika kwa haki na usalama kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo imeweka muda maalum kwenye hivi vipengele vyote vinne ambavyo vinatakiwa vifuatwe, imewekewa muda maalum kwamba wewe *PPP Center* unapewa siku 21, wewe *Steering Committee* umepewa 21, Waziri unapewa siku 21, kwa hiyo ni njia ya kuweza kufanya hii yote iweze kwenda kwa wakati kwamba wawekezaji waweze kufanya kazi yao kwa bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kwamba kuna *solicited contract* pale na *unsolicited*. Kwa hiyo, utaona kwamba hata kwenye upande wa ubunifu wa wawekezaji wao wenyewe ambao wanaweza kubuni miradi yao pia wamewekewa masharti yao ambayo yako *very clear* ambayo tumeyajadili kwa kirefu sana kwenye Kamati na kuona kwamba kwa kweli tunaweza kupata wawekezaji wote *solicited* ambao wataingia ubia na Serikali pamoja na hawa *unsolicited* ambao pia wanaweza wakaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa sana ambalo lipo ni hawa watalaam wetu ambao watakuwa hapo kwenye *PPP Center*. Nchi nyingi sana miradi hii imeshindwa kwa sababu ya *drafting* ya *legal contracts.* Uandikishaji wa mikataba umefanya kwamba miradi hii iweze ku-*fail*, kwa hiyo ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri hili alizingatie kwamba uandikishaji wa mikataba tutakapofika kwenye hatua ya kuandika mikataba ni lazima kupata uzoefu, lazima kuwa na watu wanasheria ambao wamebobea na siyo siri kwamba hata tukipata watalaam kutoka nje, vinginevyo sheria hii/mabadiliko haya yatakuwa hayana umuhimu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uandikishaji wa mikataba, tumepata fundisho kwenye *IPTL. IPTL* mradi ule ulikwenda na ulifanyika kienyeji ingawaje uliweza kusaidia *100 megawatts* ambazo tumeingia mkataba kwa njia ya

kuweka umeme kwa njia ya dizel lakini madhara yake tumeyaona. Kwa sababu mkataba haukufanyika kwa uwazi na umeletea gharama kubwa sana Serikali, ambayo sasa Serikali ilitakiwa ilipe *IPTL* mamilioni ya hela kila mwezi kiasi kwamba mpaka Awamu ya Tano imeamua kuyafunga. Kwa hiyo, suala la uandikishaji wa mikataba, *legal drafting* ni lazima lipewe umuhimu wake wa kipekee vinginevyo mabadiliko haya hayatakuwa na maana yoyote na yataturudisha kule ambako tupo.

Mheshimiwa Mwenyekit, naamini kabisa kwamba kama tutapata *committed people* ambao watakuwa pale kwenye *PPP Center,* wakafanya kazi kwa uadilifu, suala la *corruption* litaondoka, naamini kabisa tunaweza tukapiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi pamoja na hayo, baada ya sheria hii ya mabadiliko haya kupita Mheshimiwa Waziri lazima atangaze sasa *priority* zote ambazo zinatakiwa Serikali inataka ubia na miradi ipi, lazima itangazwe na itangazwe siyo kwenye gazeti tu lakini tumia *media* zote, tangaza miradi yote ambayo unaona ya kwamba sasa hivi Tanzania tuko tayari kuingia kwenye ubia wa *PPP* na miradi ifuatayo ni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana mpaka sasa hivi nchi hii kukosa mradi wa *PPP* kwenye *road toll*, sijatembea kwenye nchi yoyote duniani nikakuta kwamba hakuna mradi wa *road toll* ambao nchi imeingia na nchi nyingine. Marekani wenyewe wanafanya *road toll*, Ulaya kwenyewe kuna *road toll*, sasa hapa kwa nini hakuna *road toll*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunategemea kwamba hii miradi mingine barabara yetu hii ya Chalinze nategemea *SGR* sasa hivi ya Tanga, tangaza mradi wa Tanga wawekezaji wapo watajitokeza mimi nawajua.

Kwa hiyo, naamini kabisa marekebisho haya yakifanyika vizuri tutapiga hatua tena kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu nilitaka kuchangia na nashukuru sana, lakini mapendekezo ambayo tumeyapendekezo ambayo tumeyatoa yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Balozi kwa mchango wako, Mheshimiwa Mashimba Ndaki atafuatiwa na Mheshimiwa Yusuph Hussein.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana, na mimi nichukue nafasi hii kuchangia hoja iliyo mbele yetu, lakini mwanzo kabisa nauna mkono hoja hii iliyopo mbele yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge lako ni kutunga sheria, na sheria ziko mbele yetu, nilikuwa nasihi kwamba tujielekeze katika kutunga sheria ili watu na wananchi wa nchi yetu waone faida ya sisi kuwemo humu ndani, lakini tukianza kukwepa jukumu hili na kulisukuma kwa mtu au kikundi cha watu basi tutakuwa tunakwepa jukumu letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu uliopo mbele yetu ni Muswada ambao *concept* yake haijulikani sana kwa watu wengi, kwa sababu hiyo pengine ndiyo maana tunapochangia humu ndani tunaonekana kama hatuelewi muelekeo vizuri au ni kwa namna gani. Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba hii *Public Private Partnership* ni tofauti sana uwekezaji wake na uwekezaji ule wa binafsi tunaoita *private investment* ni tofauti kabisa, ni tofauti na uwekezaji mwingine ambao umetajwa hapa ambao ni *joint venture* ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Public Private Partnership* ni uwekezaji ambao kimsingi Serikali ilitakiwa kuwekeza, kwa sababu mwenye jukumu la kutoa *public goods* na *public services* ni Serikali, sasa kwa sababu Serikali haiwezi kuwa na rasilimali zote, kutoa *public goods* na *public services* kwa

wananchi wake kwa wakati mmoja, ndiyo maana sasa Serikali imekuja na muswada huu ili kushirikiana na sekta binafsi, lakini sekta binafsi hii itoe *public goods* au *public services*. Kwa hiyo, nia yake ukijaribu kuangalia msingi wake ni kwamba siyo kwa sababu uwekezaji huu unataka kuweka faida, kupata faida kubwa hapana! Lengo kubwa kabisa ni kutoa huduma kwa umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni tofauti na *private investment* ambapo anakuja Ndugu Dangote, Ndugu Mengi, ndugu nani anasema naweka kiwanda mahali fulani, nataka kuzalisha bidhaa fulani kwa kuuza ili nipate faida. Kwa hiyo, iko tofauti kidogo sasa tu napochangia hapa na kuvijumlisha vyote hivi kwamba ni kitu kimoja siyo sahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba hii sheria Serikali inalenga ipate nyongeza ya rasilimali kutoka sekta binafsi ili iweze kuwahudumia wananchi wake vizuri zaidi. Ndiyo maana hata uwekezaji wake unawekewa masharti kwa sababu usitake sana kuwaumiza wananchi wake, ndiyo maana wakati mwingine kwa mfano, kwenye *solicited projects*, Serikali inaweka ruzuku au inachangia pesa ili kusudi mwananchi atakayepata ile huduma asiumizwe, kwa sababu ilikuwa ni jukumu la Serikali kufanya hivyo, lakini kwa sababu ya rasilimali zake kuwa kidogo inaona ishirikiane na huyu wa sekta binafsi atoze pesa kidogo na yeye apate pesa kidogo, lakini ikiwa atatoza pesa kiasi kikubwa wanaweza kukubaliana huko baadae kwamba badala ya kuwatoza hivi wananchi wangu watoze hivi, mimi kiasi hiki nitachangia kwa sababu ni jukumu la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala hili tunataka kulifanya gumu tena kama tulivyolifanya mwaka 2010 na kama tulivyolifanya mwaka 2014 tuliporekebisha hiyo sheria ya mwaka 2010, leo kwa sababu Serikali imekuwa wazi natarajia tungetunga sheria ambayo itavutia upande wa pili wa sekta binafsi iungane na Serikali ili tupate rasilimali za kutosha, lakini naona hapa ni kama watu wana..., sielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu sasa kitu kingine kwamba kwa sababu muswada huu tutaupitisha hapa, ninaomba Serikali iweke mpango mkakati wa namna ya kutambulisha dhana hii ya *PPP* kwa watumishi wake na kwa wananchi kwa ujumla kwa sababu hii ni fursa, hata wananchi hawajui kwamba kuna vitu vinaitwa *PPP* ambapo unaweza ukashiriki na Serikali, ukafanya kitu cha kimaendeleo ukahudumia watu, lakini wewe pia ukafidika.

Naomba sana kwamba uwepo uwezo wa namna fulani ya kuwajengea uwezo watumishi wa Serikali na wananchi pia waweze kufahamu vizuri dhana hii ya *PPP* wakishafahamu waweze kujua ni kwa namna gani wanaweza wakafanya manunuzi ya miradi hii yote ya aina mbili *unsolicited* na ile *solicited,* waweze kujua kwa uwazi kabisa ili waweze kushiriki kikamilifu kufanya kazi na Serikali yao kwa manufaa ya wananchi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye sheria yenyewe kifungu cha 10 ambacho Wabunge wengine pia wamechangia. Serikali inasema kwenye *unsolicited project* kwamba haitatoa *guarantee* kwa mtu ambaye atakuja na wazo lake na anataka kufanya *unsolicited project*. Naungana na Serikali kwamba ni sawa kwa sababu huyu mtu anapokuja na wazo lake alilobuni kimsingi Serikali haikujitayarisha na hilo wazo, ana wazo la kwake mwenyewe na yeye ameshaona fursa wala siyo Serikali iliyoona, ndiyo maana ukijaribu kuangalia masharti yale yanasema mradi ule uwe *unique,* maana yake hakuna mwingne kwenye eneo ambalo mradi huu unataka kuwekwa, huyu mtu asishindane na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na kutotoa *guarantee* lakini hata uhakikisho kwamba wewe na wazo lako hili, Serikali tunakuhakikishia moja, mbili, tatu ili uweze kufanikiwa kwenye wazo lako hili. Sasa nilikuwa naomba Serikali ifikirie kutoa *assurance* ya mtu huyu kwa wazo lake zuri alilokuja nalo pengine wa kutoka hapa ndani au wa kutoka nje, lakini toa *assurance* kwamba miundombinu, kwa mfano umeme, barabara, maji, ardhi, Serikali itamsaidia,

lakini ikimwaacha tu hivi ubunifu wake ule anaweza kukata tamaa na pengine ubunifu ule ungeweza kulisaidia lile eneo ambalo ubunifu wake atauweka au ataisaidia nchi kwa ujumla kwa sababu ubunifu wake ungeweza kugusa mahali pengi pa nchi yetu, badala ya kumwacha tu kwamba sasa wewe endelea na pesa zako na watu wako na kila kitu cha kwako mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ifikirie kutoa *assurance* ni tofauti na kutoa *guarantee,* ni tofauti sana! Naomba kwamba Serikali ifanye hivyo angalau kwa miundombinu au kwa mazingira wezeshi yatakayomwezesha yule mtu akamilishe wazo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye Kifungu cha 5 cha Sheria hii....

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf Hussein na wafuatao wajiandae Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi jioni ya leo nichangie kidogo katika mada iliyopo mbele yetu. Mheshimiwa Waziri Mpango kwa mara nyingine nataka kukusaidia pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama mtanisikiliza na kunielewa, mimi siyo mtalaam wa sheria na sijui sheria, lakini katika mambo ya uwekezaji sidanganyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi humu ndani wamechangia na wanahofu juu ya suala hili kwamba huko mbele litatuletea matatizo, leo tunalitungia sheria na

mimi kwa uzoefu wangu katika uwekezaji hili litaleta matatizo huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana tunatunga sheria leo bila kujua tunataka kuja kufanya nini huko mbele, hatujui undani wa nini tunataka kuja kufanya tunatunga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Omari Kigua mchangiaji wa pili leo alikuwa anachangia nawasilikiliza vizuri anasema hii ni *new idea* na ni kweli suala la uwekezaji kwa nchi yetu ni *new idea* tunaliingiaje. Sasa hapa ndio nataka unisikilize vizuri nikusaidie ukiona utafanya marekebisho ya sheria *falakhala kheri* huko haifai basi twendeni tu tuko katika jahazi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwekezaji ni suala moja kubwa sana na ni lazima uandae miundombinu ambayo utahakikisha unamvutia mwekezaji na wewe mwenyewe unajihakikishia na ile jamii iliyokuzunguka unaihakikishia mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nasema mara zote, ili uwe na uwekezaji wenye tija usio na mashaka hapo mbele lazima kuwe na *triangle*. Serikali ikae na mwekezaji mkae pamoja na jamii mkae pamoja, bila ya hivyo uwekezaji huo baadae utaleta matatizo. Hii migogoro inayozungumzwa yote leo ndani ya nchi hii miradi iliyoanzishwa inaleta migogoro ni kwa sababu hamkukaa, ni upande mmoja uliamua, hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni lazima mu-*identify* hicho mnachotaka kufanya hiyo *PPP,* hiyo miradi muiseme bayana kutoka leo kwamba mradi huu na huu ndiyo tunataka iingie katika hilo. Maana yake nini na hili ndiyo tatizo ambalo Mheshimiwa Rais Magufuli atapata shida sana mpaka wakati mwingine anatamka maneno unamuonea huruma, katika *level* ya yenu ya Uwaziri labda hapo mtakuwa vizuri, lakini Waziri, Katibu Mkuu tatizo la Serikali ya Awamu ya Tano, kuanzia Wakurugenzi kuja chini ndiyo tatizo na hao ndiyo watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *level* yenu ninyi mpaka kufikia Makatibu Wakuu mnapokea vizuri mnafanya vizuri, mnapanga vizuri lakini nyie siyo watendaji. Kuanzia *level* ya Wakurugenzi kuja chini hapa ndiyo penye matatizo na ndiyo hili tatizo ambalo mnalipata katika Serikali ya Awamu ya Tano lazima mpaangalie vizuri hapo katika mkiona na maana hilo chukueni mfanyie kazi, mkiona siyo la maana liacheni tuzame pamoja.*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika suala la uwekezaji na miradi hii ambayo mnaikusudia ni ya *PPP* lazima muwe na bajeti. Kama Serikali mkisha-*identify* hiyo miradi ambayo hii tunataka tuingie ubia, ninyi wenyewe sasa muwe na bajeti ambayo mmeitenga kwamba bajeti hii ndiyo itatupeleka katika hiyo miradi, bila ya kuwa na bajeti ninyi wenyewe kama Serikali mkategemea tu huyo mtu aje hapa, hapo hamuingii ubia na hapo mnanunuliwa na mwisho wa siku tunakwenda katika hayo matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima Serikali ijipange na ndiyo maana nikasema mu-*identify,* haya masuala nimeyasomea Waheshimiwa! Lazima mu-*identify* ile miradi mkisha-*identify* muweke bajeti kwamba kwa uwezo wetu kama nchi miradi hii miwili ndiyo mnataka kuingi katika *PPP* na bajeti yetu sisi ni hii kama Serikali, msipofanya hivyo mkitegemea tu huyu akija mtu mnaenda kuingia katika matatizo kwa sababu yeye akija na fedha yake atawachukua kwa namna anavyotaka yeye.

Kwa hiyo, hilo Waheshimiwa naomba nalo mliweke katika vichwa vyenu muone namna gani mnalitungia sheria.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu kuhusu miundombinu, ameligusia mzungumzaji aliyemalizia kabla yangu, ni lazima ile sehemu ambayo mnataka kufanya hiyo miradi mtangulize kuweka miundombinu, kuwe na barabara hapo, kuwa na maji, kuwe na umeme na miundombinu yote ambayo inahitajika lazima iwepo kabla. Mkifanya hivyo kama Serikali hapo itakuwa tayari hili suala mmelifanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne au la tano ni uwazi. Katika vitu ambavyo tunalaumu ni kwamba hakuna uwazi katika masuala haya, wenzetu hawa wao wana utaalam na ndiyo maana Mheshimiwa Kigua akasema hii ni *new idea,* atakapokuja huyo mwekezaji tayari ana utaalam ana uzoefu ameshafanya, kwetu ni kitu kipya tunataka kukianza sasa, tuna rasilimali tu, sasa anapokuja tayari ana uzoefu, ana utaalam, ana kila kitu, sisi hatuna tunaanza sasa, tunaingiaje na mtu huyo? Ndipo pale niliposema ni lazima mkae ule utatu, kwa sababu pale ninyi mtasema yale yenu na yeye atasema yake kwamba anataka ule mradi wote awazunguke uwe wa kwake, tumeshafanya na hawa tunawajua vizuri sana, wenzetu hawa ni wazuri sana kwenye kuandika ni wazuri sana kwenye kujieleza, sasa kama hakuna uwazi mkazungumza pale halafu mkaweka kitu kimoja basi watatuzidi huko mbele na kama hawakutuzidi matokeo yake baadae ndiyo zinakuja hizo kesi wanakuja kutufilisi, kwa hiyo, lazima kuwa na uwazi katika masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujipanga hivyo, hizi siku kutoka siku 15 hadi siku 21 ni nyingi sana katika suala la uwekezaji, mkisha-*identify* ile miradi mkishaitangaza ina maana wataalaam waliopo chini yenu wafanye kazi sasa, tunataka kiwanda cha maziwa, kwa hiyo, wataalam wanaohusiana ng'ombe, maziwa, majani na nini watoe ushauri sasa pale hapa je tukiwekeza hapa kama Serikali tunataka nini na nini ili sasa mkija mkikaa na huyu mwekezaji ninyi mnajua mnachokitaka, mnatetea hoja zenu, mna-*negotiate* mpaka mnafikia makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivyo tukiingia tu kichwa kichwa tutashindwa, sasa wawekezaji wanapokuja ukimwambia baada ya siku 21 wao wanakata tamaa. Kwa hiyo, tuweke mazingira tujipange tuwe tayari, tujitayarishe kwamba tunataka kuingia katika *PPP* iwe tumejitayarisha, kwa hiyo akija *investors* anataka ku-*join* iwe tuko tayari, kwa hiyo, ndani ya siku tatu, ndani ya wiki moja *hardly* siku 10 tumemaliza biashara shughuli inaanza, iwe tayari tumejipanga vinginevyo Waheshimiwa tunaenda kuingaia katika matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano katika hili, tumeingia kweye biashara ya utalii tu hii tunalalamika kwamba wafanyakazi wengi katika sekta ya utalii au katika mahoteli ni watu kutoka Kenya, kwa nini na Tanzania vijana tunao wamesoma na nini kwa nini hawaajiriwi? Ukiimuuliza *investors* anakwambia hawaajiriki, hasa ukikaa katika mambo hayo unakuta kweli haajiriki, kwa sababu Kenya walijitayarisha kuingia katika biashara, wakawatayarisha vijana wao kuingia katika hiyo biashara, tujitayarishe kabla hatujaingia katika *PPP* tuwe tumejitayarisha, tumejipanga vya kutosha ili tukiingia tuwe tunajua. Changamoto zitakuwepo kibinadamu, lakini tuhakikishe kwamba tumejipanga vizuri na tunaingaia katika kitu ambacho tunakielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ukitaka nikusaidie zaidi katika haya nitakusaidia, nimejifunza vya kutosha, nawafahamu wenzetu namna ambavyo wanakuwa wajanja mnapoanzisha kitu na baadae wanakuzunguka, kwa sababu ni *new idea* kwetu ni lazima tuwe makini sana, nakutakia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbaraka Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie muswada huu muhimu uliopo mbele yetu. Awali ya yote nianze kwa kumpongeza sana mtoa hoja Waziri wetu, Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Philip Mpango kwa kutuletea marekebisho haya ya sheria ambayo kwa kisi kikubwa tumeyasubiri kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sheria hii ilikuja na ikapitishwa Bungeni mwaka 2010 kwa mara ya kwanza, baadae ikaja tena mwaka 2014 kwa ajili ya marekebisho na mabadiliko, leo ipo ndani tena humu Bungeni kwa mara nyingine tena tunaifanyia marekebisho, kwa hiyo, takribani

sasa itakuwa ni kama miaka minane hivi. Mheshimiwa Waziri wakati unasoma hotuba yako uligusia mambo machache/ miradi michache ambayo inaonekana kwamba inaweza ikaitwa labda ni miradi ya *PPP* ukiwemo ule mradi wa Dar es Salaam wa mwendo kasi na mingine inaonekana ipo katika *work in progress*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo haya tu utaona kwamba tulikuwa na sheria pengine ambayo haitoshelezi kwa kipindi cha miaka minane, ndiyo maana mpaka leo tukiulizwa mfano wa mradi wa *PPP* tunabaki kwenye magari ya mwendokasi ya Dar es Salaam ambayo kimsingi na yenyewe nayo kwa asilimia kubwa ni uwekezaji wa Serikali kupitia mkopo ule wa Benki ya Dunia na baadae ile *component* ya kununua mabasi ndiyo ambayo *private sector* imeingia, ukiangalia sana unaona pengine labda siyo *PPP per se.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo pengine baada ya miaka minane ni kitu gani kimepelekea mpaka tunakuwa na miradi michache? Mabadiliko haya nafikiri kwa kiasi kikubwa sana yanajibu hilo swali, tumeona nakushukuru na kukupongeza sana, mmepunguza milolongo, mmepunguza zile sheria ambazo zilikuwa zinaonekana zinawakwaza wawekezaji na sasa tupo tayari kwa ajili ya kuangalia namna gani tunaweza tuka-*implement* hii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na ushauri wa aina mbili katika kuboresha hii sheria, ushauri wa kwanza utakuwa ni wa kiujumla, lakini mwengine utakuwa ni wa kifungu. Ushauri wa kiujumla kwanza, kwanza huko Serikalini kwenye zile *Inter Ministerial Communication* inabidi ziwe *improved,* muweze kuongea, kwa sababu kuna tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati alikuja kuna wakati Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano akasema kwamba inaonekana miradi ya *PPP* pengine siyo miradi ya kuitegemea sana na siyo miradi mizuri. Baadae siku nyingine wakaja wataalam wa Wizara hiyo wakasema kwamba mradi kama ule wa Dar es Salaam - Chalinze kwa sasa siyo

priority tena sasa tunajenga reli ya *standard gauge,* kwa hiyo ule mradi kwa sasa hatuuangalii sana kwenye *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kamati tulishtuka sana kwa sababu katika moja ya miradi ambayo tunaiangalia kwa jicho la huruma sana kuona kwamba ni namna gani *PPP* inaweza kwa Tanzania ikaanza ku-*take place* hasa kwenye masuala ya *transport,* barabara ya Dar es Salaam - Ubungo mpaka Chalinze, lakini inaonekana kulikuwa na hali fulani ya sintofahamu na mwisho wiki iliyopita tu na ndiyo maana nasisitiza ushauri wa kwanza ni mawasiliano Wizara ninyi muongee huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tu nilikuwa naangalia *television* nikamuona Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* anasema kwamba wanajenga barabara ile ya kutoka Ubungo mpaka Kibaha kwa barabara sita, hali kama hiyo unakuta kwamba tayari hiyo mipango ya *PPP* kwa barabara ya Chalinze - Dar es Salaam *express way* tayari imeshakuwa *frustrated,* kwa sababu kipande ambacho kingine ungetarajia kingemvutia zaidi mwekezaji ni kipande cha kutoka Ubungo mpaka pengine Kibaha, Mlandizi mpaka kufika Chalinze, ambako ndiko kuna foleni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inaonekana Serikali inajitwisha tena mzigo ya kutaka kufanya wenyewe wakati huku tayari tuna sheria nzuri ambayo tumeshairekebisha ile. Sasa mimi napata taabu kidogo kwa maana ya kwamba utauuzaje tena huu mradi kwa mwekezaji kutoka kuanzia Kibaha sasa ambako inaonekana Serikali inafanya marekebisho inajenga barabara yenyewe mpaka Kibaha, kuanzia Kibaha sasa ndiyo uanze kuelekea Chalinze sidhani kama unaweza ukampata mtu ambaye atakuwa tayari kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nashauri kwanza wenyewe huko Serikalini mkae, muangalie kipi kinatakiwa kianze, inaonekana Wizara ya Ujenzi inavuta kwake, labda pengine Wizara ya Fedha na ninyi mnavuta kwenu, kama vile hamko katika nyumba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika ushauri wangu ni kuweka *benchmark.* Tumeona kwenye vifungu humu Waziri sasa umepewa rungu, Waziri umepewa mamlaka makubwa sana kwa ajili ya utekelezaji wa hii miradi, utakuwa unakuja kuripoti kila baada ya miezi sita. Nilikuwa nafikiria pengine wewe mwenyewe ujiwekee *benchmark* hata kwenye kanuni hizo, kwamba ikifika baada ya miezi sita basi walau utuletee hata mradi mkubwa mmoja kwa maana ya ngazi hiyo ya Kitaifa. Haiwezekani tumekuwa na sheria kuanzia mwaka 2000 mpaka 2018 sasa hatuna miradi, na sasa hivi tunafikiri tumeirekebisha sheria yetu imeshakuwa nzuri zaidi, bado baada ya miezi sita au mwaka mmoja *down the line* Waziri kama hujaweza kushawishi kuleta miradi mikubwa naanza na hii miradi mikubwa kwanza, kwa sababu utakuwa umeipunguzia mzigo mkubwa sana Serikali, kwa maana ya uwekezaji kwenye reli, kwa maana ya uwekezaji kwenye mafuta, kwa maana ya uwekezaji kwenye viwanda vya kuchataka gesi, kwa maana ya ujenzi wa miundombinu kama barabara, bandari na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya miezi sita, ndani ya miezi 12, pengine miezi 18 kama unakuja tu unatupiga blaa blaa tu hakuna aina yoyote ya uwekezaji ambao umekuja mkubwa ina maana kwamba sheria yako hii ime-*fail* na pengine na wewe mwenyewe hukujipanga vizuri labda uwe muangalifu kwenye hilo. Hilo la kwanza kwenye kuweka hizo *benchmarks* katika *level* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona sheria hii inakwenda kusaidia Halmashauri zetu, kuna miradi mingi sana kule kwenye Halmashauri, Halmashauri zina *struggle,* nazo pia tuziwekee *benchmark* kwa maana ya hao *DCs*, hao *RCs, DEDs* kwamba na wao pia watapimwa kutokana na namna gani wameweza ku-*attrack* hizi *PPP* na uwekezaji kuja ili kuipunguzia Serikali mzigo, kwa maana ya kwamba Serikali sasa itakuwa imepumua katika uwekezaji.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. MBARAKA K. DAU Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona dakika tano?

MWENYEKITI: Kengele ya pili, wewe unatoka Mafia eeh?

MHE. MBARAKA K. DAU Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Umbulla atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Kamala na Mheshimiwa Oran Njenza Manase ajiandae.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa fursa na mimi niweze kuchangia muswada huu muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kwanza nami naomba niipongeze sana Serikali kwa kuleta marekebisho haya kwa nia ya kuboresha, kuimarisha na kuharakisha utekelezaji wa miradi hii muhimu ambayo kwa kiwango kikubwa katika kutekeleza sheria hii naamini itaendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ilianza kitambo siyo kwamba imeanza sasa hivi, sheria hizi pia zilikuwepo lakini kama ambavyo imeanishwa kwenye muswada sheria hizo zilifanyiwa marekebisho, lakini bado hali haikwenda kwa kasi ambayo ilitarajiwa na hivyo muswada huu sasa hivi umerekebisha yale mapungufu yote ambayo yalikuwa kwenye sheria za awali ambazo zilifanyiwa marekebisho na hivyo tunaamini kwamba sheria hii sasa inakwenda kutekelezwa kwa namna ambavyo imekwishaboreshwa, kuharakisha na kuimarisha hatua zote zitakazotumika katika kuidhinisha miradi hii ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi inayotekeklezwa kwa njia ya ubia inahitaji uwiano wa kiutendaji na hivyo kuhitaji sheria, kanuni na taratibu zilizo wazi na zile ambazo zitanufaisha pande zote za ubia, kwa maana ya sekta ya umma na sekta binafsi. Mlolongo wa maamuzi ya kufikia

utekelezaji unapaswa kuwa na muafaka usiokatisha tamaa. Mlolongo wa kufanya maamuzi unakatisha tamaa na hasa kwa upande wa sekta binafsi, kwa hivyo naamini Muswada huu umepunguza kwa kiwango kikubwa huo mlolongo wa kufanya maamuzi ama hatua za uidhinishwaji hivyo naamini kwamba hali itakwenda kuboreka na kwa sababu hatua zile za uidhinishwaji zimepunguzwa kutoka sita hadi tatu, na mradi unapaswa kuidhinishwa ndani ya siku 21.

Mimi nimeshangaa kidogo upande wa wenzetu wa Upinzani kulalamikia kwamba siku 21 ni nyingi sana, lakini hapo hapo wanashauri Serikali iwe makini sana katika kufanya maamuzi ama kuchagua miradi ile ya *unsolicited* kwa umakini zaidi. Siku hizo 21 kama hatua hizo za kuidhinisha miradi hiyo *unsolicited* wanaona kama ni siku nyingi umakini huo utafanyika kwa jinsi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumbuke kuidhinisha *unsolicited projects* nilivyoelewa muswada huu haina maana ya kwamba Waziri anakwenda kuchukua miradi yote ile ya *unsolicited* na kuiingiza kwenye *PPP,* hapana. Nilichoelewa ni kwamba Waziri mwenye dhamana atahakikisha anakwepa ile hatua ya ushindanishi ambayo itachukua muda mrefu kushindanisha hizo *projects* za *unsolicited* na kwa hivyo kutakuwa na mlolongo wa muda mrefu kuhakikisha kwamba miradi hiyo inachelewa. Kwa hiyo, hatua hiyo imefupishwa kwa sababu hakutakuwa na ushindani, hakutakuwa na kushindanishwa ile *unsolicited projects,* lakini umakini unabaki palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba Wizara sasa ya Fedha, Waziri wa Fedha ambaye ndiye Waziri mwenye dhamana atakuwa makini zaidi kuhakikisha kwamba miradi itakayoingizwa kwenye *PPP* ni ile itakayokuwa na manufaa kwa Taifa letu na ambayo italeta tija katika maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Waziri mwenye dhamana ahakikishe kwamba asiwatumie wataalam wale ambao waliokuwa kwenye ofisi yake na naamini kwamba

kuna kitengo mahsusi cha *PPP* ambacho kitakuwa na Wataalam waliobobea watakaoweza kuchagua hiyo miradi ambayo itakuwa na tija, naamini hatua hiyo itakuwa imeshafikiriwa na jinsi ambavyo wenzangu walishashauri kuwe na mafunzo mahsusi, mkakati mahsusi wa mafunzo ambayo utawafanya wale ambao wanafanya shughuli hii wawe na uzoefu na ujuzi wa hali ya juu katika kuhakikisha kwamba suala hili linakwenda kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *transparency* na *commitment* ni suala muhimu sana katika miradi ya ubia. Muswada umeweka sharti la Serikali kutoa *compliance report* kila baada ya robo mwaka. Naamini hii itajenga nidhamu ya bajeti ya Serikali na itahakikisha kwamba fedha zitakazotolewa kwa ajili ya mradi ya ubia zitakwenda kutolewa kwa wakati. Tunalo tatizo sugu la kutotoa fedha za miradi katika hali ya kawaida ya miradi ya Serikali, lakini basi katika hali hii ya miradi ya ubia na kwa hali hii ya kutoa *compliance report* ndani ya robo mwaka, naamini kutakuwa na *transparency* na *commitment* na kuhakikisha kwamba fedha zitatolewa kwa wakati ili miradi hii ianze kwa wakati, iidhinishwe kwa wakati na iweze kwenda kufanya kazi iliyotarajiwa kunufaisha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshiiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni msisitizo wa matumizi ya mwongozo ambao Serikali imejiwekea. Muswada umeeleza bayana kwamba kuna *blueprint* ambayo itakuwa ndio mwongozo mahsusi utakaoweza kuongoza katika kutekeleza miradi hii. Mimi naamini hii itasaidia kurudisha nidhamu ya utekelezaji wa miradi na hivyo naipongeza Serikali kwa mwongozo huu na endelea kusisitiza kuboresha mazingira ya uwezeshaji kwa kutumia *blueprint* ama mwongozo uliojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona muswada pia unaruhusu uidhinishwaji wa miradi midogo ya thamani ya chini kidogo ya bilioni 46 na zaidi kidogo kutoka sekta binafsi. Naamini kwamba Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe mwisho wa siku ingawa pia tunahitaji kuwashawishi wawekezaji wakubwa kutoka nje ya nchi kwa

sababu miradi mikubwa itakayotekelezwa katika nchi yetu mwisho wa siku itabaki hapa na itakuwa na manufaa kwa mfano miradi ya barabara, wawekezaji hawataondoka nayo wala miradi ya afya naamini kwamba itakuwa na manufaa zaidi. Bado wazawa wa ndani ya nchi wanahitajika pia kushiriki katika suala zima la miradi ya *PPP* ili na wenyewe wawe na uzoefu na hali hii ya uwekezaji wandani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni lazima kuvutia wawekezaji kutoka nje na naamini kwamba elimu itakayotolewa itawahamasisha sana wawekezaji kutoka ndani ya nchi na kutoka nje ya nchi pia, lakini kwa hali ya kumudu kwa gharama ambayo imeshushwa ambayo imeainishwa katika muswada huu, ndiyo maana tumeona kwamba huu Muswada unakwenda ukiboresha suala zima la *PPP* katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali halisi tumeona pia Serikali inakwenda kusisitiza uanzishwaji wa benki hizi za uwekezaji na rasilimali. Uwepo wa Benki hizi ni sehemu mojawapo pia ya kuvutia wawekezaji wa ndani, kwa sababu *TIB* yenyewe haitoshelezi, kwa hivyo, naamini uazishwaji wa benki hizi zisisitizwe na ziwekwe imara ili ziweze kutumika kwa ajili ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono waliosema kuwa mkakati kabambe wa kuanzisha mafunzo ya *PPP* ni eneo nyeti.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kamala, Mheshimiwa Njenza na Mheshaimiwa Ally Hassan Omar King ajiandae.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia

mada iliyo mbele yetu, hii mada muhimu sana katika kuboresha Sheria ya *Public Private Partnership* ambayo ni muhimu sana katika ujenzi wa uchumi wa viwanda katika kuweka mazingira mazuri ya kukuza uchumi, na katika kuweka mazingira mazuri kuwezesha Serikali kutumia rasilimali kidogo ilizonazo katika shughuli nyingine za sekta ya umma nakuachia sekta binafsi kujihusisha na masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kueleza kwamba tulitoa ombi wakati fulani hapa Bungeni, kwa kutaka tunapokuwa tuna-*amend* sheria fulani *(Principal Act)* ingekuwa vizuri Waheshimwia Wabunge tupatiwe nakala za hiyo sheria tunayo i-*amend. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tusipofanya hivyo tunaweza kutumia muda mwingi hapa kushauri kumbe unaishauri Serikali kwa sheria ambayo siyo hiyo inayofanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti wewe kama Mwanasheria unafahamu kwamba sheria inapotungwa tunasema tuna *Principal Act*, lakini *Principal Act* hiyo inakuwa inapata mabadiliko ya mara kwa mara na kwa bahati mbaya mabadiliko haya yanapofanyika hayawi *integrated* kwenye hiyo *Principal Act,* hatari iliyopo ni kwamba tunaweza tukamtumia muda mwingi hapa unashauri, una-*amend* kumbe jambo unalo *amend* siyo hilo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali anajua siyo hilo na wanasheria wengine wanajua lakini sisi tuliosomea *general principal in law* kusoma sheria kidogo ya kuwezesha kuongoza, tunajua kwamba watunga sheria ni chombo hiki. Sasa wale wataalam ambao ndiyo wanatunga sheria wanatakiwa wakati wote watushauri vizuri, wasitumie utaalam wao kutupoteza au wasitumie utaalam wao kututegea ili baadae tukitoka hapa tunafikiri tumetunga sheria kumbe hatujatunga lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na *definition* ya *Public Private Partnership*; ukisoma vitabu na makala mbalimbali kuhusu hiki kitu kinaitwa *Public Private Partnership* ni nini, wengine wanakwambia *Private Partnership* ni pale

ambapo *Private Sector* inapowekeza kwa kushirikiana na Serikali. Walio wengi watakwambia siyo hiyo watakuambia *PPP* ni pale ambapo kunakuwepo na *agreement* kati ya *private sector* pamoja na *public* katika kufanya jambo fulani. Kama maana yake ndiyo hiyo basi, wale wanaofikiri kwamba sasa *PPP* maana yake ni kwamba *private sector* aje awekeze halafu na Serikali iwekeze kidogo tuweze kuendelea, unakuwa unafikiria kitu ambacho sicho. Kumbe *PPP* ni pale ambapo Serikali ina *transfer risk* ya ku–*invest, risk* ya *ku-design, risk* ya kusimamia *project, risk* ya ku-*operate.* Haya ni mambo mawili tofauti. Ndiyo maana nasema ni sheria ipi tunayoi-*ammend?* Ingekuwa vizuri tukawa na *principle.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipojaribu kuangalia sheria ambayo ni *principle act* ya *PPP* niliyoweza kupata inasema *Public Private Partnership means investment through private sector participation in a project undertaken in this term,* ndiyo *definition* waliyotoa. Lakini ukienda pengine ukiangalia inasema *it is all about transfer of risk in terms of project design, project management, project operations.* Sasa ndiyo maana nikasema ombi letu la Waheshimiwa Wabunge kupewa *principle act* tunayo-*amend* ni ipi na ni vizuri tukawa tunafanya hivyo, itatusaidia kushauri vizuri Serikali na kujua ni jambo gani tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nililotaka kushauri ni kwamba ukiangalia *PPP* ile *format* ambayo sasa inashauriwa kwamba itatumika itapunguza na ukiritimba tunaambiwa kwamba ukiangalia kwenye Taarifa ya Kamati imetuchorea mchoro pale, kiambatanisho namba moja inaonesha hatua kama moja, mbili, tatu, nne na tano. Ukiangalia hatua hizi zinazooneshwa hapa ni kwamba kuna hatua nyingine pale ambapo inatakiwa wakishamaliza kazi pale kwenye Kamati ya Uidhinishaji wa miradi ya ubia basi wapeleke kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nafikiri utaratibu mzuri tungefanya kama Uganda. Wao walichofanya, ile *committee* inayopitia miradi ya *PPP* na *Attorney General* ni Mjumbe wa Kamati ile, sasa *Attorney General* akishakuwa

Mjumbe wa Kamati ile unapunguza urasimu usiokuwa wa lazima wa watu kufanya kazi chini ya Wizara ya Fedha halafu baadae wakimaliza kazi wapeleke kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili na wao waangalie. Niseme tu kwamba hakuna kuna ofisi yenye ukiritimba mzuri kama ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kurahisisha mambo haya, basi huyu Mwanasheria Mkuu wa Serikali awe mjumbe kwenye Kamati inayoangalia hizi *PPP.* Wanapomaliza kazi pale pale Wizar aya Fedha hakuna tena sababu ya kusema sasa tunasubiri Mwanasheria Mkuu wa Serikali apitie ashauri kwa sababu tunakuwa tunapoteza muda bila ya kuwa na sababu yoyote ile na tunaongeza ukiritimba juu ya ukiritimba na bahati nzuri kwa utaratibu wa nchi yetu tunaye Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini pia tunae na Waziri wa Katiba na Sheria.

Sasa kwa kuwa tunaye Waziri wa Katiba na Sheria basi ni vizuri Mwanasheria Mkuu wa Serikali akafanya kazi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, asione tatizo kukaa na Makatibu Wakuu wenzake wakafanya kazi. Wakimaliza kazi pale wamemaliza tunapiga hatua tunakwenda mbele kuliko kujichelewesha sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kushauri kwenye muswada huu ukiangalia *PPP modals* zinazotumika kote duniani kuna aina tano. Aina ya kwanza inaitwa *design, finance, build, operate and transfer.* Hii ukiangalia nchi nyingi zaidi ya asilimia 9-0 ya miradi inayotekelezwa kuhusu *PPP* ni ile inayotekelezwa kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina nyingine ni *design, finance and operate.* Hii ni asilimia 10 tu ukiangalia kwa ujumla wake ambayo inapitia utratibu huu na inatekelezwa. Kuna nyingine ya *design, build, operate and transfer,* hii ni asilimia mbili tu ya miradi yote, nazungumzia *generally* ya miradi yote ambayo inatekelezwa kwa utaratibu huo. Kuna nyingine wanaita *equity partnership project,* hii ni asilimia moja

tu na nyingine wanaita *facilities, management project* na hii ni asilimia moja. Kwa maneno mengine, sheria yetu hii ingeweza kuwa na nguvu zaidi kama tungejikita zaidi katika kuwezesha utaratibu wa *design, finance, build, operate and transfer* kwa sababu ndiyo umeonekana kufanya kazi maeneo mengi waliyojaribu kutekeleza hii miradi ya *PPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu wa Uingereza, William Hague alikuwa mara nyingi anapenda kusema ukiamini katika kila kitu maana yake hauamini katika chochote. Sasa nasema hivyo kwa sababu ukiangalia ile *Public Private Partnership Act* ambayo tunasema ndiyo *Principle Act,* inataja ni miradi ipi ambayo inaweza ikaingizwa kwenye *PPP* lakini ukisoma ile sheria inataja miradi yote, miradi ya barabara...*(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Hassan King na Mheshimiwa Elibariki Kingu wajiandae.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Muswada huu muhimu sana katika nchi yetu, kwa kweli haya marekebisho yamekuja katika muda muafaka, kama alivyosema aliyenitangulia, ukiziangalia hizi ni *amendments,* marekebisho tu ya sheria, lakini nakumbuka wakati tunachakata haya marekebisho tulipata shida sana kwa sababu kulikuwa na sheria ya mwaka 2010, ikaja 2014 na sheria nyingine mbalimbali. Sasa kuzioanisha zile ilikuwa ni ngumu sana. Ushauri wangu kwa kuanzia katika utungaji wa sheria ili iwe nzuri ni bora kukawa na *consolidation* ya hizi *amendments* zote zikawa kwenye sheria moja. Nafikiri hiki ni ni kitu muhimu sana ambacho kinaweza kuwasaidia mawakili lakini hata taasisi za elimu vilevile ili waweze kufanya *reference* ya sheria ambayo ni sahihi. Nafikiri hiyo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ni kizuri sana katika hii sheria ni namna gani sasa hivi, tunakwenda kuimarisha hii taasisi yetu pamoja na uimarishaji wa kisheria lakini kikubwa zaidi namna gani inamtambua Waziri wa Fedha kuwa yeye ndiyo atalibeba hili jukumu na hilo ndiyo muhimu sana kwa sasa hivi kwa sababu *PPP* haina maana ya kubinafsisha, *PPP ownership* iko kwa Serikali, hai-*transfer* ubinafsishaji. Sasa naona katika mazungumzo hapa nakubaliana na Makamu Mwenyekiti kwamba inawezekana labda ikahitaji elimu pana zaidi kwa ajili ya umuhimu wa Miswada na miundo ya uwekezaji kama hii ili tuweze kutofautisha ni mradi gani utakaokwenda *TIC,* ni mradi gani ambao utakwenda kwenye *PPP Center.* Nafikiri hicho ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna umuhimu mkubwa kwa kuwepo chini ya Wizara ya Fedha, kwa sababu kubwa ya suala la kibajeti. Ukiangalia inawezekana kiharaka haraka tukafikiria kwamba Serikali itakuwa imejiondoa katika kugharamia hizi *PPP.* Mimi naiona hapana, kwa sababu ukiangalia kwenye *stakeholder analysis,* kuna *sponsors* ambao wana-*contribute only* asilimia 30 kama *equity,* asilimia 70 inaweza kutokana na *consortium* ya *lenders* na hao *lenders* wanaweza kutoka nje. Sasa je, hii mikopo kama itakuja Tanzania tutaichukua vipi? Serikali itakuwa na mzigo au itakuwa na *exposure?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba ukiangalia kwa kiasi kikubwa *PPP* wanasema *private partner* ndiye anachukua *risk* kubwa, je, Serikali haina *risk?* Sasa ukiangalia katika nchi zetu kama hizi maskini kwa sababu tunahitaji *PPP* kwa ajili labda ya ku-*finance* miundombinu au *services* mbalimbali ambazo ni muhimu haziwezi ku-*attract investor* binafsi.

Sasa ni namna gani Serikali pale ambapo hii *project* itakuwa haina faida, hatuwezi kuiacha kwa vile bado tunahitaji hizi *FDI's,* bado tunahitaji hizi pesa kutoka nje, bado tunahitaji kupunguza mzigo mkubwa wa Serikali wa kukopa. Sasa ni jinsi gani Wizara ya Fedha iweze kuibeba hizi *projects*

ambazo hazina faida kwa yule mwekezaji. Nafikiri kwa kiasi kikubwa inawezekana nimeangalia kwa haraka ni jinsi gani na sisi kama nchi tukachukua mifano ya wenzetu ambayo kwa kiasi kikubwa wanaangalia *viability gap funding* ambayo inakuwa ni *capital investment* ya Serikali toka pale mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo muhimu sana na nafikiri Wizara ya Fedha iliangalie kwa karibu sana hilo kwamba ni namna gani hizi *exposure* za *capital,* kwa hiyo Serikali ijiandae ya kwamba katika bajeti yake lazima kutakuwa na *element* ya ku-*support* hizi *PPP* achilia mbali ile *facilitation fund.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa sababu *risk* kubwa iko kwa huyu *private partner,* huyu tutam-*compensate* namna gani na hiyo *risk* yake kubwa. Kwa hiyo ni vitu vya kuangalia ni kwamba ile *project* itakapoanza ni namna gani Serikali itahakikisha kuwa malipo yanafanyika kwa muda muafaka ili tuweze kui-*support* ile *project.* Bado nasisitiza ya kwamba umuhimu mkubwa kwenye hizi *project* kwa vile zina-*promote innovation* ambazo ni nzuri sana hasa kwa vijana wetu wanaomaliza vyuo vikuu sasa hivi, ni muhimu sana tukazichukulia kwa haraka ili ziweze kuleta ajira kubwa ziende mpaka huko vijijini, mpaka kwenye Halmashauri ili tuwe na miradi mingi ambayo inaendeshwa na vijana wetu.

Kwa hiyo, *training* ya *PPP* ni muhimu kwa sababu hata wengine pamoja na uzoefu tulionao hizi *PPP* bado hatuzielewi vizuri. Kwa hiyo, kwa vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu wapate elimu ya kutosha ya namna ya kutafuta ajira za wao wenyewe hasa kwa kupitia hizi *PPP. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Oran Njeza kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa King na atafuatia Mheshimiwa Elibariki Kingu.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii kuchangia muswada huu wa marekebisho ya sheria Sura ya 103 ya *PPP,* pia naipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo ni muhimu kwa uchumi wetu na kwa maendeleo ya Taifa letu katika kupokea huduma kwa wananchi wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali pale ilipoleta muswada huu, kuanzia sehemu ya pili mpaka ya saba. Kifungu cha pili mpaka cha saba ambacho kimezungumzia kupunguza urasimu, lakini pia kuimarisha mifumo ya kitaasisi na kisheria katika usimamizi wa miradi ya *PPP.* Naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo ni muhimu tuliangalie wengi hatujaelewa nini hapa kimekusudiwa na ndiyo maana unaweza ukaja ukakuta wengine wanaona kwamba siku zimeongezeka na siyo kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi utaratibu wa urasimu uliokuwepo mwanzo ulikuwa na hatua nyingi lakini utaratibu wa sasa hivi hauna hatua nyingi, hatua zimepungua, majukumu katika kila eneo yameongezeka kwa maana hiyo ndiyo maana pengine imechangia kuja siku 21.

Mimi nilipata bahati kupitia marekebisho yaliyofanyika mwaka 2014 ambapo kule mradi wowote kutoka *PPP Center* unachukua siku 82 mpaka kufikia mwisho, lakini huu wa sasa hivi kutoka *PPP Center* mpaka kufikia mwisho kwa Waziri wa Fedha unachukua siku 63. Kwa hiyo, utaona wazi kwamba siku zile zimepungua ingawa baadhi ya watu wameongea kwamba siku zimeongezeka badala ya kupungua, lakini ukitazama siku hapa zimepungua. Tunalifahamu hilo, sisi ni wanasiasa kuna usemi wa kiarabu unasema *khalifu-tuarafu,* wewe ukitaka kujulikana sana

nenda kinyumena ilivyo. Ukiambiwa *inflation* imeshuka, wewe sema imepanda, ukiambiwa uchumi umekua, wewe sema umeshuka. Kwa hiyo, hayo tumeshayazoea ni ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri wenzangu tukasome katika *part* ya pili ya marekebisho yaliyopita, *establishment and administration of the PPP Center* ambapo imeanza kuanzia *section* ya nne mpaka *section* ya 7B nafikiri tunaweza tukaenda tukaliona hili ambalo nimelisema hapa. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwa kupunguza urasimu, ukipungua urasimu ina maana kwamba mambo yetu yatapata kwenda kwa haraka na zikipungua siku tutafanya kwa haraka tofauti na vile ambavyo tunazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niiombe Serikali katika usimamizi wa masuala haya, kwa sababu imetajwa hapa Waziri wa Fedha, lakini itakuwepo *contracting authority* pengine atakuwepo na Waziri wake. Sasa pamoja na vyeo vyao kwamba vimeshakuwa *defined* kwamba nani atashughulikia, sasa sijui nani ataweza kumfuata mwenzake kwa sababu inawezekana ikawa ni Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Fedha au TAMISEMI na Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, ingekuwa kuna mtu ambaye amezidi, mkubwa zaidi basi angeweza kufuatwa kuliko ambao wako katika *rank* moja inaweza ikatokea sintofahamu katika kulitatua jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kichangia na kuipongeza kwanza Serikali ni pale ilipoleta hiki kifungu cha 9 cha muswada ambacho kimekuja kubadilisha 10A(2) ambacho kinataka kituo cha ubia kufungua akaunti katika Benki Kuu, lakini pia katika kifungu cha 12 ambapo kumezungumziwa masuala hayo ya kuleta akaunti au taarifa za utekelezaji za Mradi wa *PPP Center,* lakini na kile ambacho kinazungumzia kwamba bajeti nayo iwe imekwenda kwa Waziri mhusika. Hapa napongeza kwa sababu ya udhibiti, jambo likiwa tunalitaka ni lazima tuwe na udhibiti nalo na kama hatukuwa na udhibiti nalo ina maana kwamba tunaweza wakati wowote ule kuja

kupoteza faida ambayo tuliitarajia kuipata. Kwa hiyo, naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili kwa sababu naliona limekaa vizuri sasa katika utekelezaji usemi wa waswahili unasema kwamba ada ya mja kunena muungwana ni kitendo, tuje tutende, haya ni mazuri, lakini tusipokuja kufanya ina maana kwamba hakutokuwa na faida yoyote ile, kwa sababu tumeshayaweka vizuri lakini hatutokuja kutenda itakuwa hayaji kuleta mfano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuweka usimamizi na kuripoti kwa Waziri wa Fedha itatutoa mashaka Wabunge. Amezungumza Mheshimiwa Dau pale, huu mradi wa *Dar Express Way* mpaka Chalinze ni mradi ambao Wizara moja ya Serikali inasema kwamba huu mradi umekuwa *dropped* haupo katika *PPP,* lakini Wizara nyingine inakubali kwamba huu upo na unaendelea. Kama ikiwa kuna mfumo huu wa taarifa wa kupashana habari kuangalia *performance* inaendaje itaondoa hii. Hivyo, naishukuru sana Serikali kwa kuliona hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hii *unsolicited project* ambazo tunasema kwamba zitakuwa na sifa ya kipekee, lakini pia Serikali imeweka masharti. Mimi nakubali Serikali ni lazima iweke masharti kwa sababu mara nyingi sana miradi ya aina hii mtu anapokuja akathibitishiwa kwamba bila masharti yoyote kwamba kila kitu amefanikiwa anaweza akatumia hiyo *document/certificate* ambayo amepewa kwenda kukopea nje akachukua mkopo mkubwa halafu akaenda akawekeza kwenye mradi mwingine.

Kwa hiyo, mimi hapa naona Serikali kwamba imefanya jambo la maana kabisa kwa sababu italinda zile *interest* zetu, kama tuna dhahabu zetu haziwezi kuoza chini, zitakuwa zipo bado ni za Tanzania na za Watanzania. Kwa hiyo, naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali lakini pamoja na kutoa ushauri katika hizi *small scale projects*

ambazo zimewekewa kiwango maalum cha fedha. Hapa naipongeza Serikali kwa sababu katika Halmashauri inawezekana tukafanya miradi mingine midogo midogo kwa fedha ambazo Watanzania wanaweza, lakini hapo nachukua ushauri wa Kamati ya Bajeti ambao umesema kwamba ni lazima upatikanaji wa fedha kwa sekta binafsi uwe unaweza kupatikana kirahisi vinginevyo itakuwa hakuna sekta inaweza kuingia, kwa sababu tumesema itaweza kufika kwenye shilingi bilioni 46 kwa sababu hazitazidi shilingi milioni 20 na kushuka chini.

Sasa ikiwa ni hivi ina maana kwamba ni lazima hizi taasisi binafsi ziwe zinaweza kupata mikopo na ushauri mwingine ambao wameshauri Kamati ya Bajeti wa kuimarisha Soko la Dhamana na Mitaji, soko letu la fedha likiimarishwa nalo pia linaweza likachangia na hawa wawekezaji wengine au watu wengine binafsi wanaweza wakakopa na kufanya hiyo miradi na kwa sababu wanakuwa tayari wameshatazama ile *viability* ya hii *project* na pengine wanaweza wakafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo nitoe pongezi za jumla kwa muswada huu kuletwa, kuondosha vile vikwazo ambavyo mwanzo vimetukwaza na sasa hivi vimekaa sawa kwa hiyo, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.*(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Kingu.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndipo tunafikia mwisho wa orodha niliyokuwa nayo kwa siku ya leo, mmefanya kazi nzuri, mmeutendea muswada huu haki. Kama nilivyosema tunaendelea nayo kesho siku ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango atahitimisha hoja yake, wale ambao mna nafasi mtapewa nafasi hiyo kesho ili tumalize muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo hapa, baada ya kusema hayo naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Jumatano Tarehe 12 Septemba saa tatu asubuhi.

(Saa 1.02 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano Tarehe 12 Septemba, 2018 Saa Tatu Asubuhi)